# NGUVU ISIYO YA KAWAIDA

Inachofundisha Biblia Kuhusu Ulimwengu Usioonekana – Na Kwa nini una Umuhimu

Michael S. Heiser

Imetafsiriwa na

Donald V. Mmari

# NGUVU ISIYO YA KAWAIDA

## Inachofundisha Biblia Kuhusu Ulimwengu Usioonekana— Na Kwa nini una Umuhimu

Michael S. Heiser

Kimetafsiriwa na

Donald V. Mmari

*Nguvu isiyo ya Kawaida*

Copyright © 2015 by Michael S. Heiser

*Supernatural* Tafsiri ya Kiswahili

© 2017, Miqlat

Maudhui yote ya tafsiri hii yanaweza kunakiliwa na kusambazwa kwa namna yoyote kwa ruhusa ya mwandishi na mmiliki wa hati miliki. Ruhusa hii inahusu tu tafsiri zilizochapwa na Miqlat.org pekee. Miqlat.org ni shirika lisislo lenga faida la Marekani 501 (c) (3). Ruhusa hii kwa hiyo haihusu tafsiri nyingine yoyote ya lugha hiyohiyo, au lugha nyingine yoyote, iliyochapwa na Lexham Press.

ISBN

Mfasiri: Donald V. Mmari

*Kwa mama na Baba yangu,*

*Ed na Jan Speraw*

*Ambao wangeweza kuiona hii ikija?*

*Nadhani tunajua.*

1 SAMWELI 1:1–28

## Shukrani Kwa kazi halisi ya Kiingereza

Kwa kuwa *Nguvu isiyo ya kawaida (Uhalisia Ajabu)* msingi wake umetokana na kitabu changu cha *Ulimwengu Usiooneka*, Mawazo yaliyoelezwa kwenye shukrani ya kitabu hicho yanafaa hapa, angalau kwa ufupisho.

Shukrani zinatokana na kundi la majadiliano mtandaoni lililoundwa muda mfupi baada ya kuwa nimefanya uamuzi kwamba baraza la Mungu na Ulimwengu Usioonekana wa theolojia ya Biblia zitakuwa kitovu cha huduma yangu ya kitaaluma. Haishangazi, nililiita kundi la kujifunza Baraza la Mungu (Divine Council Study Group). DCSG lilisitishwa mwaka 2004 baada ya kuhitimu kutoka katika mpango wa udaktari na kuanza kazi katika Progamu ya Nembo za Biblia (Logos Bible Software), bali zoezi hilo lilisaidia kuniandaa mimi kuviandika vitabu vyote.

*Ulimwengu Usioonekana* kilianza kama andiko lililoitwa *Hadithi ya jadi ambayo ni Kweli* (*The Myth That Is True*) ambalo nililiandika kwa ajili ya wafuatiliaji waliovutiwa na maudhui ya tovuti na riwaya yangu, *The Façade*. Sehemu kubwa ya mafundisho hayo ilionekana kwanza kwenye makala na baadae blog, wazo likiwa ni kujipa wajibu wa kutoa kitu kila mwezi. Rasimu kamili ya kwanza “Kitabu cha Hadithi,” kama ilivyokuja kufutwa, ilimalizika mwaka 2012. Andiko hilo liliboreshwa kutokana na maoni ya wasomaji. Wachangiaji maalumu wametajwa kwenye shukrani ya *Ulimwengu Usioonekana.*

Nguvu kubwa iliyokuwa nyuma ya chapisho la *Ulimwengu usioonekana*—na, kwa hiyo, *Nguvu Isiyo ya Kawaida*—watendaji watatu katika shirika la Maisha ya Imani (Faithlife Corporation/Logos Bible Software: Bob Pritchett, Dale Pritchett, na Bill Nienhuis. Sio tu kwamba walifanikiwa kulipeleka andiko langu kwenye hatua nyingine, bali pia waliona umuhimu wa toleo lililochujwa kutoka kwenye

maudhui yake. *Nguvu Isiyo ya Kawaida* kwa hiyo ni zao la maono yao.

Mhariri wangu wa *Ulimwengu Usioonekana*, na pia alihariri *Nguvu Isiyo ya Kawaida.* Faida za ujuzi na uzoefu wake zinaweza kupatikana kwenye kila ukurasa. Alimweka mtu aliekaa kwenye benchi kichwani mwangu.

Hatimaye, Ninamshukuru mke wangu, Drenna. Anafanya kila nifanyacho kiwezekane.

## Shukrani Kwa Tafsiri hii

Napenda kuwashukuru wahisani wa Miqlat.org. bila ukarimu wenu, mradi huu wa tafsiri  usingewezekana.

**Yaliyomo**

**SHUKRANI KWA KAZI HALISI YA KIINGEREZA ............... V**

**SHUKRANI KWA TAFSIRI HII ......................................... VI**

**YALIYOMO ................................................................ VII**

SURA YA KWANZA**.......................................................1**

Kuiamini Biblia ...........................................................1

SURA YA PILI**.............................................................6**

Ulimwengu usioonekana: Mungu na Miungu.................6

SURA YA TATU**.........................................................14**

Wafalme wa Zamani na Wajao.....................................14

**SURA YA NNE...........................................................21**

Uasi wa Kimungu .......................................................21

**SURA YA TANO ........................................................30**

Jiografia ya Ulimwengu..............................................30

**SURA YA SITA..........................................................38**

Neno, Jina, na Malaika ...............................................38

**SURA YA SABA ........................................................46**

Kanuni za Ushiriki......................................................46

**SURA YA NANE........................................................54**

Mahali Patakatifu.......................................................54

**SURA YA TISA..........................................................61**

Vita Takatifu..............................................................61

**SURA YA KUMI........................................................70**

Imefichwa katika Uonekano Wazi................................70

**SURA YA KUMI NA MOJA .......................................78**

Dhamira ya Kimungu ........................................ 78
**SURA YA KUMI NA MBILI ........................................ 87**
Ajaye na Mawingu ........................................ 87
**SURA YA KUMI NA TATU ........................................ 95**
Urejesho Mkuu ........................................ 95
**SURA YA KUMI NA NNE ........................................ 103**
Sio wa Ulimwengu Huu ........................................ 103
**SURA YA KUMI NA TANO ........................................ 111**
Washirika wa Tabia ya Uungu ........................................ 111
**SURA YA KUMI NA SITA ........................................ 118**
Kutawala Juu ya Malaika ........................................ 118
**HITIMISHO ........................................ 125**
**MAOMBI YA MSAMAHA ........................................ 129**
**OMBI KUTOKA KWA MWANDISHI ........................................ 133**

# SURA YA KWANZA

## Kuiamini Biblia

### Je, unaamini kweli kile inachosema Biblia?

Kwa baadhi, hilo linaweza kuonekana kama swali lisilokuwa la kawaida kuuliza kwa kitabu ambacho huenda kinasomwa zaidi na wakristo. Lakini sidhani kama ni la ajabu sana. Biblia ina baadhi ya vitu vizuri ajabu ndani yake— vitu ambavyo ni vigumu kuviamini, hususani katika ulimwengu wa sasa.

Sizungumzii kuhusu mambo makubwa, kama vile kuwa Yesu alikuwa Mungu akaja duniani, ambaye baadae alikufa msalabani na kufufuka toka kwa wafu. Na hata sifikirii kuhusu habari za miujiza kama wa kutoka, wakati Mungu alipowaokoa Waisrael toka Misri kwa kuwafanyia njia katika bahari ya Shamu. Wakristo wengi wangesema wanayaamini mambo hayo.Baada ya yote, kama humwamini Mungu na Yesu, au kwamba huamini wangeweza kufanya mambo ambayo ni miujiza, kuna maana gani kusema kuwa wewe ni Mkristo?

Nazungumzia kuhusu mambo yasiyokuwa ya kawaida yanayojulikana kidogo unayoyakimbilia mara kwa mara unaposoma Biblia bali ni mara chache kuyasikia kanisani.

Hapa kuna mfano. Kwenye 1Wafalme 22, kuna habari inayohusu mfalme mwovu wa Israel, Ahabu. Anataka kuunganisha majeshi na mfalme wa Yuda kumshambulia adui katika sehemu inayoitwa Ramoth-gileadi. Mfalme wa Yuda anataka kuona huko mbeleni—anataka kujua nini kitatokea wakishambulia. Hivyo wafalme hawa wawili wanawauliza manabii wa Ahab na wanawapa dole wote. Lakini manabii hawa wanamwambia tu Ahab kile anachotaka kusikia,na wafalme wote wanalijua hilo. Hivyo wanaamua kumuuliza nabii wa Mungu, ambaye aliitwa Mikaya. Anachokisema sio habari njema kwa Ahabu:

> Sikia basi Neno la Bwana; Nalimwona BWANA ameketi katika kiti chake cha enzi, na jeshi lote la mbinguni wamesimama upande wa mkono wake wa kuume na kushoto. BWANA akasema, Ni nani atakayemdanganya Ahabu, ili akwee Ramoth- Gileadi akaanguke? Basi huyu akasema hivi; na huyu hivi. Akatoka pepo, akasimama mbele za BWANA, akasema, Mimi nitamdanganya. BWANA akamwambia, Jinsi gani? Akasema, nitaondoka, na kuwa pepo wa uongo kinywani mwa manabii wake wote. Akasema, Utamdanganya, na kudiriki pia; ondoka ukafanye hivyo. Basi angalia, BWANA ametia pepo wa uongo kinywani mwa manabii wako hawa wote; naye BWANA amenena mabaya juu yako. (1 Wafalme 22:19–23)

Je, Ulishika kile ambacho Biblia inachokuagiza kukiamini? Kwamba Mungu hukusanyika na viumbe wa Kiroho kuamua nini kitokee Duniani? Je, hii ni kweli?

Hapa kuna mfano mwingine, Heshima ya Yuda:

> Na malaika wasioilinda enzi yao wenyewe, lakini wakayaacha makao yao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu. (Yuda 1:6)

Mungu alipeleka kundi la malaika kwenye kifungo chini ya ardhi ? Kweli?

Kama nilivyosema, Biblia ina mambo mengi ya ajabu ndani yake, hasa kuhusu yasiyoonekana, ulimwengu wa Roho. Nimekutana na Wakristo wengi ambao hawana tatizo na mafundisho ya Biblia yenye utata (angalau miongoni mwa Wakristo) kuhusu yasiyo ya kawaida, kama vile Yesu alikuwa nani na alichokifanya, lakini vifungu kama hiki wanavifanya kuwa zaidi ya ugumu kidogo, hivyo wanavipuuza. Nimeona mazoea hayo kwa ukaribu. Mke wangu na mimi tuliwahi kutembelea kanisa ambapo mchungaji alikuwa akihubiri

mfululizo uliolenga kwenye 1 Petro. Asubuhi ambayo alifikia 1 Petro 3:18–22, kitu cha kwanza alichosema baada ya kufika kwenye mimbara ilikuwa, “Tutaruka hii mistari. Ni ya ajabu sana.” Alichomaanisha kwa *ajabu* ilikuwa ni kwamba hiyo mistari ina vitu vya ajabu ambavyo haviingii kwenye theolojia yake. Kama vile:

> Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili ya wasio haki, ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa, ambayo kwa hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri; watu wasiotii hapo zamani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, Safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane, waliokoka kwa maji. (1 Petro. 3:18–20 NIV)

Nani na wapi zilipo roho hizi zilizofungwa? Yule mchungaji huenda hakujua au hukulipenda jibu, hivyo kirahisi tu akaamua kuipuuza hii mistari.

Kama Msomi wa Biblia, nimejifunza hivyo vifungu vya ajabu (na vingi ambavyo vinajukana-kidogo na sehemu za maandiko ambazo zinaeleweka-kidogo) kwa hakika ni vya muhimu sana. Vinafundisha mawazo mahususi kuhusu Mungu, ulimwengu usioonekana, na maisha yetu wenyewe. Amini au usiamini, kama tungekuwa tunaifahamu na kuelewa imemaanisha nini, kwa kadri ya ugumu na kufumba kama ilivyo, ingebadilisha namna tunavyofikiri kuhusu Mungu, kila mmoja, kwanini tuko hapa, na hatma yetu ya mwisho.

Katika barua ya kwanza mtume Paulo aliyoandika kwa Wakorintho, Paulo alikasirishwa na namna waumini katika kanisa lile walivyokuwa wanapelekana kwenye mabaraza kusuluhisha migogoro. Ulikuwa ni upotezaji wa muda na nguvu ya kihisia, alivyohisi, pamoj na mtazamo hasi kwenye imani yao. Akasema, “Hamjui ya kuwa mtauhukumu

ulimwengu? Hamjui kuwa mtawahuku Malaika!" (1Kor. 6:3, ufafanuzi wangu).

**Kuhukumu Ulimwengu? *Kuhukumu juu ya Malaika*?**

Anachokisema Paulo kwenye Msitari huu wenye kufumba kwa pamoja ni vya kusisimua-akili na kubadili- maisha. Biblia inaunganisha shughuli za viumbe wa Kiungu na maisha yetu na matarajio yetu. *Tutauhukumu* ulimwengu wakati fulani. *Tutawahukumu* malaika kama Paulo alivyosema. Zaidi kuhusu hilo baadae.

Sababu ya Paulo kuweza kusema kile alichokisema kwa Wakorintho na kwetu ni kwamba habari ya Biblia ni kuhusu namna Mungu alivyotuumba na kutaka tuwe sehemu ya familia yake ya Mbinguni. Sio bahati mbaya kwamba Biblia hutumia maneno yanayotokana na mahusiano ya kifamilia kama vile kuishi pamoja na kufanya kazi pamoja kwa pamoja kumwelezea Mungu, Yesu, viumbe wa ulimwengu usioonekana, na waumini, *mimi na wewe*. Mungu anataka binadamu kuwa sehemu ya familia yake na ya utawala wake juu ya uumbaji.

Sote tunajua dhana ya *kama ilivyo huko mbinguni, na hapa duniani iwe hivyo.* Imechukuliwa kutoka wazo na hata maneno yanayopatikana kwenye Sala ya Bwana (Mat. 6:10). Toka mwanzo kabisa, Mungu alitaka familia yake ya kibinadamu iishi nae kwenye ulimwengu mkamilifu sambamba na familia ambayo tayari alikuwa nayo kwenye ulimwengu usiionekana, wenyeji wa mbinguni. Hiyo habari lengo la Mungu, upinzani wake toka nguvu za giza, kushindwa kwake, na mafanikio yake ya baadae, ndicho hichi kitabu kinahusika nacho, kama ambavyo ndicho ambacho Biblia inahusika nacho. Na hatuwezi kufahamu mchezo wa habari ya Biblia kama tusipowajumuisha wahusika wote ukijumisha wahusika wasio wa kawaida ambao ni sehemu ya utenzi lakini ambao wanapuuzwa na waalimu wengi wa Biblia.

Washirika wa kusanyiko la mbinguni la Mungu hawako pembeni au kukosa umuhimu au kutohusiana na habari yetu, habari ya mwanadamu, kwenye Biblia. Wanafanya wajibu mkuu. Bali wasomaji wa Bibli wa kisasa mara kwa mara wanazisoma na kupita, bila kuzielewa, njia za kuvutia ulimwengu usio wa kawaida unawasilisha kwa dazeni vipande vinavyofahamika kwenye Biblia. Ilinichukua miongo kuona kile ninachokiona sasa kwenye Biblia na nataka kuwashirikisha tunda la miaka hiyo ya kujifunza

Lakini hebu tusipoteze mwelekeo wa lile swali nililouliza pale mwanzoni. *Je, unaamini kweli kile inachosema Biblia?* Hapa ndipo mpira unapokutana na barabara (nahau ya kiingereza inayo maanisha hatua ambayo wazo linahitaji utekelezaji, kuliweka kwenye matendo '*Hapo ndipo matatizo yanapoanzia*'). Haitakusaidia chochote kujifunza kile ambacho Biblia inasema kweli kuhusu ulimwengu usioonekana na namna unavyoingiliana na maisha yako kama huamini.

Kwenye 2 Wafalme 6:8–23, nabii Elisha yuko kwenye tatizo (tena). Mfalme mwenye ghadhabu anatuma vikosi kuizunguka nyumba yake. Wakati mtumishi wake anashitushwa, Elisha anamwambia, "Usiogope, maana walio pamoja nasi ni wengi kuliko walio pamoja nao." Kabla mtumishi hajapinga, Elisha anaomba, "Ee BWANA, nakusihi, mfumbue macho yake, apate kuona." Mungu akajibu hapo hapo: "BWANA akamfumbua macho yule mtumishi; naye akaona; na tazama, kile kilima kilikuwa kimejaa farasi na magari ya moto yaliyomzunguka Elisha pande zote."

Maombi ya Elisha ni maombi yangu kwako. Mungu ayafumbue macho yako uone, ili kwamba usiendelee kufikiri kuhusu Biblia kwa namna ile ile.

# SURA YA PILI

## Ulimwengu usioonekana: Mungu na Miungu

Watu wanavutiwa na yasiyo kuwa ya kawaida na ubinadamu usio wa kawaida. Fikiri kuhusu sekta ya burudani katika miaka ya hivi karibuni. Maelfu ya vitabu, vipindi vya runinga, na sinema katika muongo uliopita vimekuwa vikihusu malaika, wageni, viumbe hatari, mapepo, mizimu, wachawi, uchawi, misukule, watu wanaogeuka kuwa mbwa mwitu, mashujaa. Sehemu kubwa ya filamu za Hollywood zinazofanya mauzo makubwa sana zinakuwa na uhalisia ajabu (supernatural): the *X-Men*, the *Avengers*, the Harry Potter series, *Superman*, and the *Twilight* saga. Vipindi vya runinga kama *Fringe* na, kwa kweli, *uhalisia ajabu* na Faili za *X*, inawafuatiliaji waliojitolea hata muda mrefu baada ya kurekodi vipande vya mwisho vya sinema. Na kweli, Je, vitu hivi havijawa mashuhuri wakati wote katika hadithi, katika vitabu, katika sanaa?

### Kwa nini?

Jibu moja ni kwamba vimekuwa sehemu ya kukwepea kawaida. Vinatupa ulimwengu wenye kufurahisha na kusisimua zaidi ya tulionao.  Kuna kitu kuhusu wema dhidi ya uovu, vinavyokuzwa kwa viwango vikubwa ambavyo hutuogofya. Mapambano ya kishujaa ya mashujaa wa dunia ya kati (Gandalf, Frodo, and company) against the Dark Lord dhidi ya bwana wa giza Sauron katika Bwana wa Mapambano (*The Lord of the Rings* trilogy) kimevutia wasomaji wengi (na sasa waenda kwenye filamu) kwa zaidi ya nusu karne sasa. Kadri wazimu mwingine wa kidunia unapoongezeka, ushindi unakuwa wa kushangaza zaidi.

Kwa kiwango kingine, watu wanavutiwa na ulimwengu mwingine, kama kitabu cha mhubiri kinavyoweka, Mungu "ameweka umilele ndani ya mioyo yetu" (Mh. 3:11). Kuna kitu fulani kuhusu hali ya mtu ambacho hutafuta kitu kilicho nje ya

uwezo wa mwanadamu, kitu cha Kimungu. Mtume Paulo aliandika kuhusu shauku hii pia. Alifundisha kuwa inatokana na kuwa hai katika ulimwengu aliouumba Mungu. Uumbaji hubeba ushahidi kwa muumba, na hivyo kwa ulimwengu ulio juu ya tulionao (Rum. 1:18–23). Kwa kweli, Paulo alisema msukumo huu ulikuwa na nguvu sana kwamba ulipaswa kukandamizwa kwa makusudi (m. 18).

Na bado hatuonekani kufikiri juu ya hadithi za mtiririko wa matukio ya Biblia kwa namna sawa na tunavyofikiria hadithi zetu wenyewe za uhalisia ajabu kwenye vitabu, sinema, na masimuliz ya ushujaa. Kuna sababu za hilo, na zinaenda mbali zaidi ya kutokuwa na athari maalumu. Kwa baadhi, Wahusika wa Biblia ni wa kawaida sana au wazee. Hawajihisi kuwa na nguvu au ushujaa. Baada ya yote, hawa ni watu walewale na hadithi zilezile ambazo tumekuwa tukizisikia toka Shule ya jumapili kama watoto. Halafu kuna kizuizi cha kitamaduni. Ni vigumu kwetu kutambua na kile kinachoonekana kama gwaride lisilo na mwisho la wachungaji wa kale na watu wavaao mavazi, kama walivyo waigizaji kwenye kanisa lako wa tamthilia ya kuzaliwa.

Lakini nafikiri sababu kubwa zaidi ya kwa nini sayansi ya kubuni au burudani ya kimungu inakamata hisia zetu kirahisi zaidi ni namna tulivyofundishwa kufikiri kuhusu ulimwengu usioonekana wa Biblia. Kile nilichokisikia makanisani kwa miaka hakipotei tu—inafanya miungu kuwa kitu kisichovutia. Na kibaya zaidi, mafundisho ya kanisa yanavipunguza visivyooneka, ulimwengu wa kimungu, kuvifanya visiwe na nguvu.

Mengi ya yale Wakristo wanayofikiria kuwa kweli kuhusu ulimwengu usioonekana hayako hivyo. Malaika hawana mabawa. (Makerubi hawahesabiki kwa sababu kamwe hawaitwi malaika na sio wanadamu. Malaika wakati wote wana umbo la kibinadamu) Mapepo hayana pembe na mkia, na hayapo hapa kutufanya tufanye dhambi (tunafanya hivyo sisi wenyewe). Na

wakati Biblia inaelezea kupagawa pepo katika njia sahihi ya ajabu, uovu mwerevu una vitu vingi hatari vya kufanya kuliko kutufanya kama wanasesere nje ya watu. Na juu ya hilo, malaika na mapepo ni wahusika wadogo. Kanisa kamwe halionekani kuwafikia wavulana wakubwa na agenda yao.

## Miungu ni Halisi

Nilikuuliza katika sura ya kwanza kama *kweli* unaamini inachosema Biblia. Fikiria kuhusu jaribio hili la kushtukiza.

Biblia inasema Mungu ana kikosi kazi cha viumbe wa kimungu ambao wanatekeleza maamuzi yake. Kinatambulika kama, Mkutano wa Mungu, Baraza, au Mahakama ya Mungu (Zaburi 89:5–7; Dan. 7:10). Moja ya mistari wazi zaidi kuhusu hili ni Zaburi 82:1.Tafsiri ya habari njema inaliweka vizuri: "Mungu anasimama katika kusanyiko la Mungu; Katikati ya miungu anahukumu."

Kama ukiufikiria, huo ni mstari wa kushangaza! Nilipoutazama kwa mara ya kwanza kwa kweli ulinishtua. Lakini kile mstari unachomaanisha ni ambacho kwa uwazi na urahisi umesema. Kama mstari mwingine wowote, Zaburi 82:1 inatakiwa kueleweka katika muktadha wa kingine chochote ambacho Biblia inachosema—katika hili, kile inachosema kuhusu miungu na jinsi neno hilo linavyotakiwa kutafsiriwa.

Neno halisi la Kiebrania lililotafsiri "miungu" ni *elohimu*. Wengi wetu tumeifikiria *elohimu* kwa muda mrefu kwa maana moja tu—kama moja ya majina ya Mungu Baba—kwamba inaweza kuwa vigumu kwetu kulifikiria kwa maana yake pana. Lakini neno linamaanisha mwenyeji yeyote wa ulimwengu wa kiroho usioonekana. Hii ndiyo sababu utalikuta likitumika kwa Mungu mwenyewe (Mwanzo 1:1), mapepo (Kumb. 32:17), na kwa binadamu wafu katika maisha baada ya kifo (1Sam. 28:13). Kwa Biblia, kiumbe chochote ambacho anuani ya nyumbani kwake ni ulimwengu wa roho ni *elohimu*.

Neno la kiebrania halimaanishi vitu ambavyo Mungu pekee ndiye ana uwezo navyo.Biblia inamtofautisha Mungu kutoka kwenye miungu mingine kwa njia nyingine, sio kwa kutumia neno *elohimu*. Kwa mfano, Biblia inawamuuru miungu kumwabudu Mungu wa Biblia (Zaburi 29:1). Yeye ni muumba wao na Mfalme (Zaburi 95:3; 148:1–5). Zaburi 89:6–7 (GNT) inasema, "maana ni katika mbingu awezaye kulinganishwa na BWANA? Ni nani afananaye na BWANA miongoni mwa malaika? [1 Wafalme 8:23; Zaburi. 97:9]. Umetukuka sana juu ya miungu yote." Waandishi wa Biblia wako wazi sana kuhusu Mungu wa Israeli kutokuwa na wa kulingana naye—yeye ni "Mungu wa miungu" (Kumb. 10:17; Zaburi 136:2).

Viumbe hawa katika "baraza la walio watakatifu" ni wa kweli. Katika sura ya kwanza ya kitabu hiki, nilinukuu kifungu ambacho Mungu alikutana na majeshi ya mbinguni kuamua namna ya kuachana na Mfalme Ahabu. Katika kifungu hicho, wanachama wa kundi hili la mbinguni waliitwa roho. Kama tunaamini ulimwengu wa roho ni halisi na unakaliwa na Mungu na viumbe wa kiroho aliowaumba (kama vile malaika), tunapaswa kukubali kuwa kikosi kazi cha Mungu cha kiungu, kilichoelezewa kwenye mistari niliyonukuu hapo juu na mingine mingi, pia ni kweli. Vinginevyo, tunauabudu kwa midomo tu uhalisia wa kiroho.

Na kwa kuwa Biblia inatambulisha wanachama hawa wa baraza la kimungu kama roho, tunajua miungu sio tu sanamu za mawe au mbao. Sanamu hazifanyi kazi ya Mungu katika baraza la mbinguni. Ni kweli kuwa watu katika ulimwengu wa zamani ambao waliabudu miungu adui waliitengeneza miungu hiyo. Lakini walijua miungu waliyoitengeneza kwa mikono yao wenyewe haikuwa nguvu halisi. Miungu hiyo iliyotengenezwa ilikuwa tu ni vitu ambavyo miungu yao ingevikalia kupokea sadaka na kuwapa maarifa wafuasi wao, ambao wanafanya matambiko kukusanya miungu ije kwao na kuchukua makao katika miungu.

### Muundo wa Baraza na Kazi zake

Miungu wa Zaburi 82:1 wanaitwa "wana wa Aliye Juu Sana [Mungu]" baadae katika zaburi hiyo (m. 6). "Wana wa Mungu" wanatokea mara kadhaa katika Biblia, mara nyingi katika uwepo wa Mungu (kama kwenye Ayubu 1:6; 2:1). Ayubu 38:7 inatuambia walikuwepo kabla Mungu hajaanza kuiumba dunia na kumuumba mwanadamu.

Na hicho ni cha kufurahisha. Mungu anawaita hawa viumbe wa kiroho wanawe. Kwa kuwa aliwaumba, lugha ya "kifamilia" inakuwa na maana, kwa namna sawa na unavyowaita uzao wako kama watoto wako wa kiume na wa kike kwa sababu ulishiriki katika uumbaji wao. Lakini mbali na kuwa Baba yao, Mungu pia ni mfalme wao. Katika ulimwengu wa zamani, wafalme mara nyingi walitawala kupitia familia zao pana. Ufalme ulipitishwa kwa warithi. Utawala ulikuwa ni kazi ya familia. Mungu ni Bwana wa baraza lake. Na wanawe wana nafasi inayofuata ya juu kabisa kwa nafasi ya uhusiano wao na yeye. Lakini kama tutakavyojadili katika kitabu hichi chote, kitu fulani kilitokea baadhi yao walikosa uaminifu.

Wana wa Mungu pia ni wafanya maamuzi. Tunajua kutoka 1Wafalme 22 (na vifungu vingine vingi) ambapo kazi ya Mungu ilihusisha kuzungumza na historia ya mwanadamu. Wakati Mungu alipoamua kuwa ulikuwa ni wakati wa mwovu Ahabu kufa, aliliacha hilo mikononi mwa baraza lake kuamua jinsi hilo lingetokea.

Mkutano wa baraza la Mungu katika Zaburi 82 na 1 Wafalme 22 sio hizo pekee zinazo husiana na sisi katika Biblia. Michache kati yao iliamua hatma ya himaya au falme.

Katika Daniel: 4, Nebukadreza, mfalme wa Babeli, aliadhibiwa na Mungu kwa kuchanganyikiwa kwa muda. Hukumu yake ilishushwa chini kwa "agizo la Aliye Juu" (Dan. 4:24) na "na agizo la walinzi" (Dan. 4:17). *Walinzi* ni neno lililotumika kwa viumbe wa kiungu wa baraza la Mungu. Lina

maanisha jinsi walivyokuwa waangalizi mambo ya wanadamu muda wote; kamwe hawakulala.

Matukio haya ya Kibiblia ya vikao vya baraza la Mungu yanatuambia wajumbe wa baraza la Mungu *wanashiriki* katika utawala wa Mungu. Katika angalau baadhi ya mambo, Mungu huagiza anachotaka kifanyike bali huwapa wawakilishi wake wa kiungu uhuru wa kuamua namna au njia.

Malaika wanashiriki katika baraza la Mungu vile vile. Katika lugha asilia za Biblia, neno lililotafsiriwa *malaika* katika Agano la Kale na Jipya kwa kweli lina maana ya *mtume* (mtumishi). Neno *malaika* kimsingi ni maelezo ya kazi. Malaika wanatoa ujumbe kwa watu. Tutajifunza zaidi kuhusu malaika na kazi zao—vile vile na kazi nyingine za wajumbe wa Baraza la Mungu—baadae kwenye kitabu.

## Kwa nini Hili ni Muhimu

Majibu yako kwa kila kitu ulichosoma katika kitabu hiki hadi hatua hii yanaweza kuwa kitu kama, "Mambo ya kuvutia sijawahi kuona hilo katika Biblia kabla. Lakini maelezo haya yote yana athari au matokeo gani, kama ipo, kwa maisha yangu ya kila siku na namna kanisa langu linavyofanya kazi?" Na jibu ni kuwa, ukweli ulioelezwa kwenye kitabu hiki una kila kitu cha kufanya kwa uelewa wetu wa Mungu ni nani, na namna tunavyohusiana naye, na kusudi letu duniani ni lipi. Kusaidia kufafanua hilo, nitahitimisha kila sura na kipengele kama hiki ambacho kinaelezea athari au matokeo ya kuweka kwenye matendo ukweli wa sura hiyo.

Katika sura hii, tumejadili namna Biblia inavyoelezea utawala wa Mungu kiulimwengu na ni ufahamu gani maelezo hayo yanatupa kwa Mungu na, hatimaye, namna Mungu anavyohusiana na sisi.

Kwanza, kazi ya familia ya Mungu ya mbinguni ni mfano wa namna anavyohusiana na familia yake ya kidunia. Tutalijadili hilo zaidi kwenye sura ijayo, lakini hapa kuna mfano: unaweza kuwa umekuwa ukishangaa kwa nini hata hivyo Mungu anahitaji baraza. Mungu hapaswi *kuhitaji* msaada kufanya chochote, hata katika ulimwengu wa roho. Yeye ni Mungu! Lakini Biblia iko wazi kwamba huwa anawatumia viumbe wadogo kufanya mambo.

Yeye *hahitaji* baraza la Mungu, lakini yeye huchagua kutumia yeyote. Na hatuhitaji sisi wala. Kama angechagua, Mungu angeweza tu kusema kwa sauti kubwa kwa watu wote wanaohitaji injili, kumtia moyo kila mmoja anakokuhitaji ili kumgeukia, na kuliita hilo jema. Angeweza kuwashawishi watu kuwapenda wengine kwa kuweka sauti yake vichwani mwao. Lakini hakufanya hivyo. Badala yake, anawatumia watu—wewe na mimi—kufanya kazi itendeke.

Pili, Mungu angeweza tu kupangilia matukio kufanya kila kitu kigeuke namna anavyoyataka. Lakini hakufanya hivyo. Katika habari ya Mfalme Ahabu, Mungu anawaachia wasaidizi wake wa mbinguni waamue namna ya kutekeleza maamuzi yake. Kwa maneno mengine, anawaacha watumie uhuru au mapenzi yao. Inatuambia kuwa sio kila kitu kinakuwa kimepangwa. Na hiyo ni kweli sio tu katika ulimwengu usioonekana—ni kweli pia katika ulimwengu wetu.

Katika Biblia, ulimwengu usioonekana una mpangilio. Mungu ni mtendaji mkuu (CEO). Wale wanaofanya kazi kwa ajili yake ni familia yake. Wanashirikiana utawala. Wanashiriki katika namna kampuni inavyoendeshwa.

Cha kushangaza vyakutosha, Biblia inasema namna hiyo hiyo kuhusu wanadamu. Awali kabisa katika Edeni, Mungu alimuumba mwanadamu aitawale dunia pamoja naye. Mungu aliwaambia Adamu na Hawa, "Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha" (Mwanzo 1:28GNT). Adamu na Hawa

walikuwa watoto wa Mungu—familia ya Mungu kidunia. Mungu alitaka kuishi nao na kuwafanya washiriki katika kuufanya ulimwengu wote kama Edeni.

Hilo ni wazo linalofahamika kwa wasomaji wengi. Kisichokuwa wazi sana ni kwamba Adamu na Hawa hawakuwa wajumbe pekee wa familia ya Mungu katika Edeni. Familia yake ya kiungu pia ilikuwa pale. Edeni ilikuwa mahali ambapo Mungu aliishi—na ambapo Mungu anaishi, hivyo na familia yake. Tunafikiri kuhusu mbinguni kama mahali ambapo tutaishi na Mungu na malaika wake—familia yake ya kiungu. Hivyo ndivyo ilivyokusudiwa kuwa toka awali, na ndivyo *itakavyokuwa*. Sio bahati mbaya kwamba Biblia inaishi na mbingu kushuka duniani katika Edeni mpya, ya kimataifa (Uf. 21–22).

Kuielewa hatma yetu, tunapaswa kurejea nyuma hadi kwenye wakati ambao Familia mbili za Mungu zilikaa sehemu moja. Tunapaswa kurejea nyuma katika bustani.

# SURA YA TATU

## Wafalme wa Zamani na Wajao

Tulikuwa na utangulizi mfupi kuhusu baraza la Mungu la mbinguni—familia yake isiyoonekana na nguvu kazi. Kuna mengi zaidi kuhusu hayo yote—tunahitaji kutazama, hususani, kwa namna wahusika wakuu kama vile Yesu na Shetani wanavyoingia kwenye picha. Lakini kabla hatujarejea kwenye kile kinachoendelea kwenye ulimwengu usiionekana, tunahitaji kufikiri kwa njia nzuri kuhusu sisi wenyewe. Utawala wa Mungu kwenye ulimwengu wa kiroho usioonekana kupitia baraza lake ni mfano au kielelezo cha utawala wake duniani-kile wanatheolojia wanachoita Ufalme wa Mungu. Haya yote yalianzia kwenye Mwanzo, katika bustani ya Eden.

### Edeni— Ofisi ya Nyumbani ya Mungu

Ni kitu gani huwa unakifikiria kwanza unaposikia "bustani ya Edeni"? Watu wengi niliowahi kuzungumza nao wanafikiria Adamu na Hawa. Edeni ilikuwa makao yao. Hapo ndipo Mungu alipowaweka (Mwanzo. 2:15–25).

Lakini pia Eden ilikuwa *nyumbani kwa Mungu*. Ezekieli anaielezea Edeni kama "Bustani ya Mungu" (Ezek. 28:13; 31:8–9). Hakuna cha kushangaza, hasa. Kinachoweza kuwa cha kushangaza ni kwamba baada tu ya kuiita Edeni "Bustani ya Mungu," Ezekieli anaiita "mlima mtakatifu wa Mungu" (m. 28:14). Kwenye dini nyingi za kale, bustani za kifahari, na milima isiyofikika zilidhaniwa kuwa nyumba za miungu. Biblia inatumia maelezo yote ya Edeni. Edeni ilikuwa ni makao ya Mungu na, kwa hiyo, ndipo alipofanyia mambo yake. Yalikuwa makao yake makuu, au ofisi ya nyumbani.

Na alipo Mungu, na Baraza lake lipo nae.

### Sura ya Mungu

Moja ya mistari muhimu sana kwenye Biblia inatufahamisha kuwa Mungu na Baraza lake walikuwa katika Edeni. Kwenye Mwanzo 1:26 Mungu anasema, "Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu" (LEB, Msisitizo unaongezwa). Mungu anatangaza dhamira yake kwa kundi. Anaongea na nani? Jeshi lake la Mbinguni— Baraza lake. Hazungumzi na wanachama wengine wa Utatu, kwa sababu Mungu hawezi kujua kitu wao wasijue! Na hapa kundi analozungumza nalo linajifunza kile Mungu alichoamua kufanya.

Tangazo ni rahisi kulielewa. Ingekuwa kama mimi kuwaambia marafiki, "Tupate sambusa!" *Tufanye hiki!* Iko wazi vyakutosha. Lakini kuna kitu kingine hatutakiwi kukikosa. Mungu kwa kweli halitumii kundi katika kufikia maamuzi yake.

Tofauti na vikao vingine vya baraza la kimungu tulivyokwisha viona, washiriki wa baraza la Mungu hawashiriki katika maamuzi haya. Wakati mtu anapoumbwa kwenye msitari unaofuata (Mwanzo. 1:27), Mungu pekee ndiye anayeumba. Uumbaji wa mtu ni kitu ambacho Mungu alikifanya mwenyewe. Tukirejea nyuma kwenye mfano wangu wa sambusa, kama ningelifuatilia tangazo langu kwa kumpeleka kila mmoja kwenye eneo la Sambusa na kusisitiza kulipa, ningekuwa mimi ndiye ninafanya kazi yote. Hicho ndicho tunachokiona kikiendelea hapa.

Inaleta maana kwamba Mungu pekee ndiye aliyekuwa akiwaumba wanadamu. Viumbe wengine wa Kiungu wa baraza lake hawana uwezo huo. Lakini hii inazalisha upekee mwingine. Kwenye Mwanzo 1:27, watu wameumbwa kwa sura ya *Mungu* ("Mungu alimuumba mtu kwa sura *yake*," LEB, msisitizo unaongezwa).

Nini kilitokea kwa “sura yetu” kutoka msitari wa 26? kwa kweli, hakuna. Mbadilishano kati ya “ sura yetu” na “sura yake” kwenye Mwanzo 1:26–27 inaonyesha kitu fulani cha kuvutia. Kauli ya Mungu—“Na tufanye mtu kwa sura yetu”—inamaanisha yeye na wale anaozungumza nao wanakitu flani kinachofanana. Haijalishi ni kitu gani, wanadamu pia watakuwa nacho maadamu Mungu aliwaumba. Sio tu kwamba tuko kama Mungu kwa namna Fulani, bali pia kama Viumbe wa kiungu wa baraza lake .

“Kitu” hicho kinaelezewa kwa maneno “sura ya Mungu.” Tafsiri bora ya Mwanzo 1:26 ingekuwa kwamba Mungu alimuumba mtu kwa sura yake. Kuwa mtu ni kuwa sura ya Mungu. Sisi ni wawakilishi wa Mungu, tukizungumza hivyo.

Sura ya Mungu sio uweza tuliopewa na Mungu, kama vile akili. Tunaweza kupoteza uwezo, lakini hatuwezi kupoteza hadhi ya kuwa sura ya Mungu. Hiyo isingehitaji kuwa mtu! Kila mtu, toka kutungwa mimba hadi kifo, wakati wote anakuwa mtu na wakati wote anakuwa sura ya Mungu. Hii ndio sababu maisha ya mtu ni matakatifu.

Tunamuwakilishaje Mungu? Tuliona kwenye sura iliyopita kwamba Mungu anashiriki mamlaka yake pamoja na viumbe wa kimungu watenda kazi wasioonekana. Anafanya vivyo hivyo na wanadamu duniani. Mungu ni mfalme mkuu wa wafalme wote wanaoonekana na wasioonekana. Anatawala. Anatumia mamlaka hayo na familia yake kwenye ulimwengu wa roho na ulimwengu wa watu. Tuko hapa kushiriki kwenye mpango wa Mungu kuufanya ulimwengu kile anachotaka na kuufurahia pamoja nae .

Hatimaye Mungu alituonyesha namna ya kufanya hivyo. Yesu ni mfano wa mwisho wa kumuwakilisha Mungu. Anaitwa sura ya Mungu asiyeonekana (Kol. 1:15) na alama halisi ya Mungu (Ebr. 1:3). Tunapaswa kumuiga Yesu kwa sababu hiyo (Rum. 8:29; 2 Cor. 3:18).

### Mabaraza Mawili, Hatma Moja

Kuna pigo katika haya yote natumaini unaelewa. Wanadamu kimsingi ndio utawala wa Mungu—baraza lake—*duniani*. Tuliumbwa tuishi kwenye uwepo wa Mungu, na familia yake ya mbinguni. Tuliumbwa tumfurahie na kumtumikia milele. Awali, hilo lilikusudiwa kutokea duniani. Eden ndipo mbingu na dunia vilikutana. Mungu na wanachama wa baraza lake walichukua nafasi sawa na wanadamu.

### Lakini kwa mwisho gani?

Mungu aliwaambia Adamu na Hawa, "Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale...kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi" (Mwanzo 1:28). Hili lilikuwa ni jukumu la sura ya Mungu. Wangemtumikia Mungu kama mawakili-wa kifalme juu ya uumbaji. Kazi ya ubinadamu ilikuwa ni kuongeza kasi duniani na kuieneza Edeni kwenye sayari yote kukuza ufalme wa Mungu. Kazi hii ilikuwa kubwa mno kwa watu wawili, hivyo Mungu alitaka Adamu na Hawa kuzaa watoto.

Kama tunavyojua, Adamu na Hawa na kizazi chao walishindwa. Ubinadamu ulifanya dhambi. Kama hilo lisingetokea, dunia ingebadilishwa hatua kwa hatua kuwa Edeni ya ulimwengu wote. Tungekuwa na maisha ya milele kwenye sayari iliyofanywa kuwa kamilifu, tukiishi na Mungu na familia yake ya kiroho.

Mungu aliupenda ubinadamu, hivyo aliwasamehe Adamu na Hawa. Lakini kutoka wakati huo ubinadamu uliosalia unabaki kwenye nyayo za Adamu na Hawa. Sote tunatenda dhambi na kustahili mauti bila Mungu kuingilia (Rum. 6:23). Tu wafu na, kwa hiyo, wadhambi. Tunahitaji wokovu.

Wazo la Mungu la kututaka tujiunge na familia yake ya Kiungu, kuwa sehemu ya baraza lake na kuishi kwenye uwepo

wake, inatusaidia kuelewa baadhi ya mambo ya ajabu inayosema Biblia.

Inaelezea kwanini Biblia inawaita waumini "wana wa Mungu" au "watoto wa Mungu" (Yohana 1:12; 11:52; Gal. 3:26; 1 John 3:1-3). Inaelezea kwanini waumini wanaelezewa kama "wamepokewa" kwenye familia ya Mungu (Gal. 4:5-6; Rum. 8:14-6). Inaelezea kwanini tunasemekana kuwa "warithi" wa Mungu na ufalme wake (Gal. 4:7; Tito 3:7; Yakobo 2:5) na "washirika wa asili ya Kimungu" (2 Pet. 1:4; tazama pia 1 Yohana 3:2). Inelezea kwa nini, baada ya Yesu kurejea, anasema atawapa waaminio"kula ya mti wa uzima, ambao uko kwenye Paradiso ya Mungu" (Uf. 2:7). Inaelezea kwanini aliahidi kushiriki kuyatawala mataifa pamoja nasi (Uf 2:26-28), hata kiti chake cha enzi chenyewe (Rev. 3:21). Tunasonga *mbele* kupitia maisha haya kurejea Edeni. *Mbingu zitarejea duniani.*

*Hicho* ndicho tutakachokuwa tukifanya baada ya maisha haya kutawala kwenye Edeni ya ulimwengu wote. Tutakuwa tukifurahia kile ambacho Adamu na Hawa walikusudiwa hapo awali kusaidia kuzalisha. Maisha ya milele sio kupiga vinubi na kuimba 24/7. Inahusu kugundua na kufurahia uumbaji usio na kasoro kwenye utimilifu usiofikirika pamoja na Mungu mwenyewe, Yesu aliyefufuka, na wenzetu ambao ni sura ya mungu, watu na miungu.

## Kwanini hii ni Muhimu

Inaweza isionekane hivyo, bali mawazo mengi ya kubadilisha maisha yanatokana na hiki. Kuishi kwa kufahamu kwamba maisha yetu yanamuwakilisha Mungu na kuendeleza mipango yake hata kama hatuuoni huo mpangoingebadili namna tunavyoikabili kila siku.

Mpango halisi wa Mungu ilikuwa kuufanya ulimwengu wote kuwa kama Edeni. Mungu alitaka wanadamu washiriki kuendeleza utawala wake mzuri juu ya dunia yote, kama

ilivyokuwa Edeni. Aliwaambia Adamu na Hawa wazae watoto na kuwa mabwana na mawakili wa uumbaji (Mwanzo. 1:26-28). Amri hiyo haikusahaulika baada ya anguko. Kwa hakika, ilirudiwa baada ya matukio mabaya ya gharika (Mwanzo. 8:17; 9:1). Ingawa Edeni ilipotea, Mungu anakusudia irejeshwe. Hatimaye, utawala wake ufalme wake utarejea katika ukamilifu wake wakati Yesu atakaporejea na Mungu kuumba mbingu mpya na nchi (ile iliyo, kwenye Ufunuo 21 na 22, inaonekana zaidi kama Edeni). Kwa wakati huu, tunaweza kueneza kweli ya Mungu na injili ya Yesu kila mahali. Tunaweza pia kumuwakilisha Mungu kwa kila tunayekutana nae na kila mahali. Sisi ni mawakala wa Mungu kuirejesha Edeni hapa na sasa, tukiitazamia siku ambayo Yesu atauleta mpango huu kwenye kilele.

Kufikiri kwa uwazi kuhusu sisi wenyewe kama Mawakala wa Mungu sura yake inamaanisha *maamuzi tunayofanya yana umuhimu.* Wakristo, hawajapotea tena dhambini, wanaweza kutimiza mpango wa Mungu kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Tuko hapa kueneza uzuri wa maisha na Mungu na kuwaambia watu wanaohitaji injili namna wanavyoweza kuufurahia pia. Maisha yetu yanaingiliana na watu wengi. Kumbukumbu ya wale wanaopata mavuno kupitia maisha yao na kupitia watu wote ambao wanagusa maisha yao. Sisi ni ishara ya Maisha pamoja na Mungu au bila Mungu. Hakuna nafasi ya kati.

Kufahamu kwamba watu wote ni sura ya Mungu inapaswa ituwezeshe kuyaona maisha ya mtu kuwa kitu kitakatifu kama yalivyo. Hii inapita maamuzi makubwa ya maadili ambayo yanahusika na maisha na kifo. Kile tulichojifunza kina athari zaidi kwenye namna tunavyo tazamana kila mtu na mwenzake na kuhusiana kila mtu na mwezake. Ubaguzi wa rangi hauna nafasi kwenye ulimwengu wa Mungu. Uonevu haukubaliani/ hauendani na kumwakilisha Mungu. Matumizi mabaya ya madaraka nyumbani, kazini, au serikalini sio vya Kimungu. Sio namna ambayo Mungu alijihusisha na wanawe pale Eden,

hivyo havina nafasi kwenye namna tunavyojihusisha na wenzetu ambao ni sura ya Mungu.

Mwisho, kumuwakilisha Mungu inamaanisha kila kazi inayomtukuza ni wito wa *Kiroho*. Kila jukumu halali linaweza kuwa sehemu ya kuupeleka ulimwengu wetu kuelekea Edeni na kuwabariki wenzetu ambao ni sura ya Mungu au sivyo. Mungu hawatazami watu walio kwenye huduma kuwa ni watakatifu zaidi au maalumu kwa sababu ya kazi yao. Mungu anajali namna ambavyo kila mmoja wetu anavyomuwakilisha pale alipo. Ama tunasimama kinyume cha giza, tukishiriki maisha ambayo Mungu anataka kila mmoja ayashiriki au hatufanyi hivyo. Fursa hiyo haihitaji kuwa ya kushangaza; inahitaji tu kuchukuliwa.

Kama mpango wa Mungu pale Edeni ulivyokuwa wa kuvutia, maono hayo yalikufa kwa kasi inayolingana. Mungu *pekee* ndiye mkamilifu. Uhuru mikononi mwa viumbe wasio wakamilifu hata wale wa kimungu yanaweza kuwa na matokeo yenye maafa.

# SURA YA NNE

## Uasi wa Kimungu

Nilihitimisha sura iliyotangulia kwa wazo kwamba nia huru mikononi mwa viumbe wasio wakamilifu, kwamba ni wa kiungu au wanadamu, inaweza kuwa na matokeo yenye maafa. Hiyo ni kauli inayopunguza uzito. Baadhi ya majanga kwenye sura za mwanzo za Biblia, yote yanayohusisha wanadamu au viumbe wa kiungu, yanaelezea kwa undani.

Kumbuka kwamba Mungu aliamua kushirikisha maamuzi yake kwa wote, viumbe wa Kimungu kwenye ulimwengu wa Roho na wanadamu duniani. Hiyo ilikuwa nyuma ya maneno ya Mungu, "Na tumfanye mtu kwa sura yetu" (Mwanzo. 1:26, msisitizo umewekwa) na ukweli kwamba baadae Mungu alimwumba mtu kwa sura yake. Viumbe wa kiroho na wanadamu ni sura ya Mungu. Tunashiriki mamlaka yake na kumuwakilisha kama watawala washirika.

Kwa upande mmoja, huo ulikuwa ni uamuzi mzuri. Uhuru au hiari ni sehemu ya kuwa kama Mungu. Tusingeweza kuwa kama yeye kama tusingekuwa nao. Bila uhuru au hiari, dhana kama vile Upendo na kujitoa dhabihu hufa. Kama umeandaliwa tu "kupenda" hakuna uamuzi ndani yake. Sio wa kweli. Maneno na matendo yaliyoandikwa sio halisi. Katika kilifikiria hili linanirejesha nyuma kwenye mwisho wa filamu halisi ya Nyota wa Vita, *Kurejea kwa Jedi (The Return of the Jedi).* Roho ya Obiwan Kenobi inamwambia Luka baba yake, Darth Vader, "ni mashine zaidi sasa kuliko mtu" Na bado, mwishoni, tunakuta kuwa hilo sio kweli. Vader anamuokoa Luka kutoka kwa mfalme kwa kuyagharimu maisha yake mwenyewe. Hakuwa tu mashine iliyopangiliwa. Maamuzi yake yalitoka moyoni, utu wake—kwa hiari yake mwenyewe.

Lakini kuna sehemu iliyofichika kwenye maamuzi ya Mungu. Kuwapa Uhuru viumbe wenye akili inamaanisha wanaweza na watafanya makosa au kuasi kwa kudhamiria. Na hili kulikuwa na uhakika wa kutokea tu, kwa kuwa kiumbe

pekee kilicho kikamilifu ni Mungu. Yeye pekee ndiye angeweza kutumainiwa. Hii ndiyo sababu mambo yalikwenda mrama pale Edeni.

### Matatizo katika Paradiso

Fikiri kuhusu mpangilio wa Edeni. Adamu na Hawa hawakuwa peke yao. Mungu alikuwepo pamoja na Baraza Lake. Edeni ni makao makuu ya Mungu/wanadamu ya kuitawala sehemu nyingine za dunia (Mwanzo. 1:26–28) kuyaeneza maisha ya Edeni kwenye sehemu iliyosalia ya sayari. Lakini mshiriki mmoja wa baraza hafurahii mpango wa Mungu .

Kama tu tulivyoona kwenye Mwanzo 1, kuna dondoo kwenye Mwanzo 3 kwamba Edeni ni makao ya viumbe wengine wa Kimungu. Kwenye msitari wa 22, baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, Mungu anasema: "Basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya" (msisitizo umewekwa). Maneno haya ni sawa tu na maelekezo tuliyoyaona kwenye Mwanzo 1:26 ("sura yetu").

Tunajua sifa kuu ya Mwanzo 3, yule nyoka, hakuwa nyoka kweli. Kwa hakika hakuwa mnyama. Hakuna jitihada ya kumweka nyuma ya kioo katika hifadhi ingekuwa yenye ufanisi, na asingekuwa amedhihakiwa. Alikuwa ni kiumbe wa kimungu. Ufunuo 12:9 inamtambulisha kama Mwovu, shetani.

Baadhi ya wakristo wanadhani, kulingana na Ufunuo 12:7–12, kwamba kulikuwa na uasi wa malaika muda mfupi baada ya uumbaji:

> Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake walipigana na yule joka, yule joka nae akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. Yule joka akatupwa Yule mkubwa nyoka wa zamani aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye. (Ufunuo. 12:7–9LEB)

Lakini vita iliyoelezewa mbinguni hapo, inahusishwa na kuzaliwa kwa Masihi (Ufunuo 12:4–5, 10LEB):

Na Yule joka akasimama mbele ya Yule mwanamke aliyetayari kuzaa, ili azaapo, amle mtoto wake. Naye akazaa mtoto mwanamume, yeye atakayewachunga mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Na mtoto wake atanyakuliwa hata kwa Mungu, na kwa kiti chake cha enzi ....

Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema,

"Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake, kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu mchana na usiku.

Biblia haitoi ishara yoyote kuwa, kabla ya matukio ya pale Edeni, sura yake yoyote wanadamu au miungu walikuwa wakipinga maamuzi ya Mungu au walikuwa na uasi. Hali ilibadilika kwa kasi katika  Mwanzo 3.

Kosa la Yule Joka ni kuwa kwa hiari yake alichagua kukataa mamlaka ya Mungu. Tunaweza kusema, Mungu alikuwa amedhamiria kuwa Adamu na Hawa wajiunge na kazi ya familia. Wangeieneza Edeni duniani. Lakini adui hakuwataka pale. Alijiweka yeye kwenye nafasi ya Mungu. Alisema moyoni mwake, "Nitapanda mpaka mbinguni nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu. Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano" (Isaya. 14:13NLT).

Aliwaka tamaa. Kwa kuwa udanganyifu wa nyoka ulipelekea Adamu na Hawa kutenda dhambi, alifukuzwa kutoka kwenye makao ya Mungu (Ezek. 28:14–16) na kutupwa duniani "na kutupwa chini" katika lugha ya Kibiblia (Isaya. 14:12) mahali ambapo mauti hutawala, ambapo maisha hayadumu . Badala ya kuwa bwana wa uzima, akawa bwana wa mauti, kitu kilichomaanisha kuwa adui mkuu sasa alikuwa na madai juu ya watu wote tangu matukio ya Edeni yaliyomaanisha kupoteza

hali ya kutokufa kimwili. Wanadamu sasa wangehitaji kukombolewa ili wawe na maisha ya milele na Mungu kwenye Edeni mpya.

Anguko (lililokusudiwa) ulikuwa ni mlolongo wa laana. Laana juu ya nyoka inahusisha unabii kidogo. Mungu alisema uzao wa Hawa na ule wa Nyoka utakuwa na uadui: "Bwana Mungu akamwambia nyoka… Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake" (Mwanzo. 3:14–15 LEB). Je, wazao wa Hawa ni akina nani? Ubinadamu. Na uzao wa nyoka ni nani? Vyema, hilo ni la kufikirika zaidi. Mtume Yohana anatupa mfano—kama wa viongozi wa Kiyahudi waliomchukia Yesu. "Nanyi ni wa baba yenu Ibilisi," Yesu aliwaambia (Yohana 8:44). Yesu alimwita msaliti wake, Yuda, shetani (Yohana 6:70). Uzao wa nyoka ni yeyote anayesimama kinyume na mpango wa Mungu, kama yeye alivyofanya.

## Uzao Mbaya

Haikuchukua muda mrefu kwa matatizo zaidi kuibuka. Mmoja wa wana wa Adamu na Hawa alikuwa mwuaji. Kaini alimwua Habili, akionyesha kuwa alikuwa "wa Yule mwovu" (1 Yohana 3:12). Kadiri idadi ya watu ilivyoongezeka katika habari ya biblia, na uovu nao uliongezeka (Mwanzo. 6:5).

Sasa linakuja kosa lingine lisilo la kawaida ambalo, ingawa haliwezi kujadiliwa sana kwenye mahubiri ya jumapili asubuhi, lilikuwa na athari kubwa katika kueneza uovu duniani. Wakati huu kulikuwa na muasi zaidi ya mmoja. Uovu mbaya unaenezwa kupitia ubinadamu kwenye Mwanzo 6:5 inaunganishwa na habari ya kwenye Mwanzo 6:1–4 kuhusu wana wa Mungu kuwazaa watoto wao wenyewe wa kimwili ambao wanajulikana kama wanefili.

Biblia haisemi zaidi kwenye Mwanzo kuhusu kilichotokea, bali vipande vya habari hii vinajionyesha kwingine kwenye Biblia, na kwenye mila za kiyahudi nje ya Biblia, waandishi wa

Agano Jipya walijua vyema na walinukuu kwenye maandiko yao.

Kwa mfano, Petro na Yuda wameandika kuhusu malaika walioasi kabla gharika (2 Petro. 2:4–6GNT; tazama pia Yuda 5–6).baadhi ya vile wanavyosema vinatoka kwenye vyanzo vya Kiyahudi nje ya Biblia. Petro na Yuda wanasema wana wa Mungu waliofanya kosa hili walifungwa chini ya ardhi kwa maneno mengine wako kifungoni kuzimu hadi nyakati za mwisho. Zitakuwa sehemu ya hukumu ya mwisho ya Mungu, kitu ambacho Biblia inaita "Siku ya Bwana."

Vyanzo vya Petro na Yuda vinajulikana vyema kwa wasomi wa Biblia. Mojawapo ilikuwa ni kitabu kilichoitwa Henoko 1. Kilikuwa maarufu kwa Wayahudi wa wakati wa Yesu na Wakristo kwenye kanisa la kale, ingawa hakikuchukuliwa kuwa kitakatifu na chenye uvuvio. Lakini Petro na Yuda walidhani kuwa baadhi maudhui hayo yalikuwa na umuhimu wa kutosha kujumuishwa kwenye nyaraka walizoziandika.

Vyanzo hivi vinabashiri kuwa wana wa Mungu huenda walitaka "kusaidia" ubinadamu kwa kuupa maarifa ya kimungu, na wakapuuzwa, au walitaka kumuiga Mungu kwa kutengeneza sura zao wenyewe. Pia vinajumuisha maelezo kuwa mapepo yalitoka wapi. Mapepo ni roho zilizosalia baada ya vifo vya wanefili waliouawa kabla na wakati wa gharika. Zinazunguka duniani zikisumbua wanadamu na kutafuta kuwa na miili tena. Kwenye vitabu vya Biblia vinavyofuata baada ya Mwanzo, wazaliwa wa wanefili wa Mwanzo 6:1–4 wanaitwa Waanaki (wana wa Anaki) na Waemi (Hesabu. 13:32–33; Kumb. 2:10–11). Baadhi ya hawa Waemi wanajionyesha katika ulimwengu wa wafu chini ya ardhi (Isaya. 14:9–11) kule ambapo nyoka alitupwa chini. Waandishi wa Agano Jipya baadae waliita hiyo sehemu Kuzimu.

Mawazo haya yanatuonyesha kwamba waandishi wa awali wa Kiyahudi walielewa tishio la Mwanzo 6:1–4. Wana wa Mungu

walikuwa wakijaribu kuirekebisha Edeni, mahali ambapo miungu na wanadamu kwa pamoja walikaa, kwa namna yao wenyewe. Walidhaniwa kujua vyema kuliko Mungu kile ambacho kinapaswa kutokea duniani, kama tu adui halisi alichokuwa nacho. Mabadiliko ya mpango wa Mungu kurejesha utawala wake yanaishia kuifanya hali ilyokuwa mbaya kuwa mbaya zaidi.

Sio tu kuwa sehemu ya Mwanzo 6:1–4 ni mwangwi mbaya wa uzao ya nyoka kudhamiria kupingana na Mungu ulikuwa ni utangulizi wa mambo mabaya yajayo. Nyakati za siku za Musa na Joshua, baadhi ya wapizani waliokabiliana nao wakati wakijaribu kuidai nchi ya Ahadi ilikuwa ni koo za majitu zilizotawanyika katika nchi (Kumb. 2–3). Haya majitu yalikuwa na majina kadha wa kadha. Kwenye Hesabu 13:32–33 wanaitwa wana wa Anaki (Waanaki). Wanasemekana kuwa wana waishio wa wanefili uzao wa wana wa Mungu tuliowaona nyuma katika Mwanzo 6:1–4. Agano la kale linatuambia Wana wa Israeli walikuwa wakipigana na maadui hawa wenye miili mikubwa mpaka wakati wa Daudi. Alimuondoa Goliathi (1 Sam. 17), na baadhi ya watu wake waliwaua watu wa Goliathi na hatimaye kuhitimisha tishio lao (2 Sam. 21:15–22).

## Kwa nini hili ni Muhimu

Laana ya kinabii juu ya Nyoka na makosa ya kiungu yaliyofuata ni hatua za awali za kile watheolojia wanachoita vita ya kiroho mapambano dhidi ya wema na uovu, vita ndefu dhidi ya Mungu na watu wake. Ni vita inayopiganwa kwenye uwanja wa mapigano wa ulimwengu wa aina mbili: unaoonekana na usioonekana.

Kama vile hizi habari zilivyo za ajabu, zinafundisha somo la muhimu: Mungu alikuwa na ushindani wa kiungu lilipokuja suala la hatma ya mwanadamu. Bado anao hata sasa. Upinzani kwa mapenzi ya Mungu kwa dunia na kwa ubinadamu ni hai na mzuri, kote kwenye ulimwengu wa roho na kwa wanadamu.

Bali Mungu ana mipango yake mwenyewe ya namna mbingu na dunia vitaunganishwa tena. Kuingiliwa kwa uadui hakutaenda bila kuadhibiwa. Ubinadamu ni wa thamani sana. Mipango ya Mungu mwenyewe kwa familia yake ya wanadamu haitabadilika au kupinduliwa.

Vifungu hivi pia vinafundisha somo chanya. Wakati vita dhidi ya Mungu inaweza kuonekana toka nyuma kabisa kwenye maamuzi ya Mungu kuumba sura yake, wanadamu na miungu, ambao watashiriki sifa yake ya uhuru, Mungu sio chanzo cha uovu.

Hakuna kipengele chochote ndani ya Biblia ambacho Mungu aliwaruhusu wale ambao ni sura yake kukipuuza, au kwamba kutokutii kwao kulikwisha pangwa. Ukweli kwamba Mungu anajua yajayo haimaanishi kuwa ilikwishapangwa. Tunajua hilo kwa hakika kutokana na vifungu kama 1Samweli 23:1–14, kinachotuelezea kuhusu wakati Daudi alipouokoa mji uliozungushiwa ukuta wa Keila toka kwa wafilisti. Baada ya vita Sauli alifahamu kuwa Daudi yupo kwenye mji huo. Sauli alikuwa ametafuta kumuua Daudi kwa muda kwa hofu kubwa kwamba Daudi angechukua kiti chake cha ufalme. Sauli alituma jeshi kwenda Keila, akitumaini kumpata/kumtegea Daudi ndani ya kuta za mji. Wakati Daudi aliposikia kuhusu mpango wa Sauli, alimuuliza Mungu:

> "Je, watu wa Keila watanitoa, nitiwe mkononi mwake? Je! Sauli atashuka, kama mtumwa wako alivyosikia? Eeh Bwana, Mungu wa Israel, nakusihi umwambie mtumwa wako."
>
> Naye Bwana akajibu, "Atashuka... Ndiyo, watakusaliti." (1 Samweli 23:11–12NLT)

Ndipo Daudi akafanya kile ambacho yeyote kati yetu angefanya alitoka nje ya mji kwa haraka kadri alivyoweza. *Na hiyo inatuelezea kwa nini Mungu kufahamu matukio yajayo haimaanishi yameshapangwa.* 1Samweli 23 Mungu aliyajua

matukio hayo mawili ambayo kamwe hayakufanyika. Kwamba Mungu alijua kuwa kutakuwa na uasi wa kimungu na kushindwa kwa mwanadamu haimaanishi kuwa *alivifanya* vitu hivyo vitokee. Kufahamu jambo kabla haihitaji kuwa limepangwa.

Tunapaswa kuyatazama matukio ya anguko kwenye mwanga huu. Mungu alijua kuwa Adamu na Hawa watashindwa. Hakushangazwa. Anajua mambo yote, halisi na yanayowezekana. Lakini ukweli kwamba Mungu angeweza kuona kabla kuingia kwa uovu na uasi kwenye ulimwengu wake, kwa pande zote za wanadamu na uasi wa kimungu ambao ulishawishi ubinadamu kuasi, haimaanishi alisababisha itokee.

Tunaweza na tunapaswa kuutazama uovu tunaokutana nao kwenye maisha yetu wenyewe na nyakati zetu kwa namna hiyo hiyo. Mungu alitangulia kuliona anguko na alikuwa tayari na mpango wa kurekebisha. Pia alijua kuwa tutazaliwa wadhambi na kushindwa (mengi- hebu tuwe waaminifu). Lakini hakupanga huko kushindwa. Tunapofanya dhambi, zinapaswa kuwa dhambi zetu. Tunafanya dhambi kwa kuwa tunachagua hivyo. Hatuwezi kusema Mungu alitaka hivyo, au kwamba hatukuwa na chaguo/namna kwa sababu ilishapangwa.

Lakini Mungu alionyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi “Kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu,tulipokuwa tungali wenye dhambi” (Rum. 5:6–8). Alitupenda licha ya kujua tungefanya nini. Hakutupa tu uhuru wa kutenda dhambi, bali pia alitupa uhuru wa kuiamini injili na kuishi kwa ajili ya Yesu.

Mungu pia anajua na tunajua, kwa uzoefu kwamba mambo mabaya hutokea kwa watu, na hata kwa Wakristo. Uovu upo duniani kwa sababu watu (na viumbe wa kimungu) wana uhuru wa kufanya uovu. Mungu wetu sio uungu potofu unaopanga mambo mabaya au unaotaka makosa mabaya na dhambi

vitokee ili baadhi ya mipango mikubwa ifanye kazi vyema. Mungu hauhitaji uovu, kipindi. Mipango yake itasonga mbele licha ya kuwepo uovu ikiushinda na hatimaye kuuhukumu.

Tunaweza kuuliza kwa nini Mungu asiuondoshe uovu sasa hivi. Kuna sababu: kwa Mungu kuuondoa uovu angepaswa kuwaondoa walio sura yake, wanadamu na miungu, ambao sio wakamilifu kama yeye alivyo. Hiyo ingetatua tatizo la uovu, lakini ingemaanisha kwamba wazo halisi la Mungu, kuwaumba mawakala wengine wa kiungu na wanadamu waishi na kutawala pamoja nae, lilikuwa ni kosa kubwa. Mungu huwa hafanyi makosa.

Tunaweza pia kutamani kwamba Mungu asingewapa wanadamu uhuru, lakini tungelikuwa wapi basi? Katika kuchagua kutupa uhuru, Mungu hakutaka kutufanya watumwa wasio na akili au roboti. Hiyo ni mbadala wa kuwa na nia huru.lakini kwa kuwa uhuru ni sifa ambayo tunashiriki na Mungu, bila kuwa nao kwa hakika tusingeliweza kuwa sura ya Mungu. Mungu siyo roboti. Alitufanya kama yeye mwenyewe. Na hilo halikuwa kosa pia. Mungu alilipenda mno wazo la ubinadamu kiasi cha kutokuwepo nafasi ya kufanya maamuzi mbadala. Na kwa hiyo alipanga njia ya kuukomboa ubinadamu, baada ya uovu kuingia ulimwenguni, kuihuisha Edeni, na kufuta kila chozi, (Ufunuo 7:17; 21:4).

Kuangalia kwetu vita vya muda mrefu dhidi ya Mungu kunaendelea. Mungu anao mkakati wa vita. Bali hali inaenda kuwa mbaya zaidi kabla hajafanya hatua yake ya kwanza.

# SURA YA TANO

## Jiografia ya Ulimwengu

Makosa ya Kiungu tuliyoyatazama kwenye sura iliyotangulia yalikuwa na kitu kinachofanana. Wote ulikuwa ni uasi wa kimungu uliolenga kuvuruga mpango wa Mungu kwa ubinadamu na urejesho wa utawala wake. Katika sura hii tutatazama katika uasi mwingine, ambao uliasilishwa na watu.

Uasi huu ulileta shida ambayo sisi sote bado ni sehemu yake, na shida hiyo inahusisha viumbe wa kiungu. Mapambano makubwa ya mkakati wa Mungu wa urejesho yaligeuka kuwa ubaya ambao hatimaye Yesu pekee atakaporejea ndiye atakayeutatua.

### Mnara wa Babeli

Habari ya mnara wa Babeli (Mwanzo. 11:1–9) ni moja ya mambo yanayofahamika sana na wakati huo huo linaloeleweka kidogo sana katika matukio ya Biblia. Watoto wanajifunza kwenye shule ya jumapili kama wakati ambao Mungu alizichanganya lugha za wanadamu za dunia.

Baada ya gharika, Mungu alirudia agizo alilokuwa amelitoa kwa Adamu na Hawa la kujaza dunia. Alikuwa anajaribu kuanza kueneza hamasa ya utawala wake kupitia ubinadamu. Kwa mara nyingine, haikufanikiwa. Watu walikataa. Uasi mioyoni mwao, walikuwa na wazo zuri zaidi, au walifikiri hivyo. Waliamua kujenga mnara ili *kuepuka kutawanyika* (Mwanzo. 11:4). Mantiki inaoneka isiyo ya kawaida. Hakika, mnara wa kushangaza ungewafanya wawe maarufu (Mwanzo. 11:4), lakini hilo lingezuia vipi kutawanyika katika dunia?

Jibu lipo katika mnara. Wasomi wa Biblia na wataalamu wa masalia ya kihisoria wanajua Babeli ya kale na miji iliyojengwa kuzunguka mnara inayoitwa Ziggurats (miji iliyojengwa kwa Piramidi). Lengo la ziggurats lilikuwa ni kutoa mahali ambapo

watu wangekutana na miungu. *Zilikuwa sehemu za kanda za hekalu.* Badala ya kuufanya ulimwengu kuwa kama Edenikueneza maarifa na utawala wa Mungu kila mahali watu walitaka kumshusha Mungu katika eneo moja.

Huo haukuwa mpango wa Mungu, na hakufurahishwa. Hivyo taarifa yake tena kwa wanachama wa baraza lake "Haya, na tushuke huko, tuwachafulie usemi wao" (Mwanzo. 11:7 GNT, msisitizo umeongezwa). Mungu alifanya hivyo, na wanadamu wakagawanyika na kutawanyika. Tukio hili linaelezea jinsi mataifa yaliyooredheshwa katika sura iliyotangulia ya Mwanzo 10 yalivyotokea.

Hiyo ni habari ambayo wakristo wengi wanaifahamu. Sasa kwa wasichojua.

## Miungu na Mataifa yake

Mwanzo 11 sio kifungu pekee kinachoonyesha kilichotokea katika Mnara wa Babeli. Kumbukumbu la torati 32:8–9 linaelezea kwa njia hii:

> Yeye aliye juu alipowapa mataifa urithi wao, alipowabagua wanadamu, aliweka mipaka ya watu kwa kadiri ya hesabu ya wana wa Israeli. Maana, sehemu ya Bwana ni watu wake, Yakobo ni kura ya urithi wake.

Baadhi ya tafsiri za Biblia zina "wana wa Israel" badala ya "wana wa Mungu" kwenye sentensi hiyo ya kwanza. Lakini *Israeli hawakuwepo katika wakati huo wa Mnara wa Babeli.* Mungu alimuita tu Abramu baada ya Babeli (Mwanzo. 12). "Wana wa Israeli" haiwezi kuwa sawa. "Wana wa Mungu" ni istilahi (neno) iliyokutwa kwenye vitabu vya Bahari ya Shamu, maandiko ya kale zaidi ya Biblia. Toleo la kiingereza (ESV) linayo kwa usahihi.

Maneno ni muhimu. Wakati Mungu alipogawanya mataifa, *yaligawanywa miongoni mwa wana wa Mungu.* Mungu alitoa

mataifa kwa wanachama wa baraza lake la Kimungu. Haya ni maelezo ya Biblia ya kwa nini mataifa mengine yalikuja kuabudu miungu mingine. Mpaka Babeli, Mungu alitaka uhusiano na ubinadamu wote. Lakini uasi pale Babeli ulibadilisha hilo. Mungu akaamua kuwaachia wanachama wa baraza lake la kimungu kutawala mataifa mengine

Mungu alikuwa ameuhukumu ubinadamu. Hata baada ya gharika wasingeendelea na mpango wa ufalme aliouanzisha katika Edeni. Hivyo Mungu aliamua kuunda taifa jipya, "sehemu" yake kama Kumbukumbu 32:9 inavyosema Israeli. Alifanya hili, akianza na wito wa Abramu, katika Mwanzo 12, sura inayofuata tu mara baada ya habari ya Mnara wa Babeli.

Ugawaji wa Mungu wa mataifa kwa miungu wengine unaunda Agano lote la kale. Kwa vipi? Sehemu iliyosalia ya Agano la Kale inahusu Mungu wa Israeli na watu wake, waisrael, katika mgogoro na miungu ya mataifa mengine na watu walioishi kati yao.

Hiyo haikuwa dhamira halisi ya Mungu. Ndiyo, alichofanya Babeli kwa mataifa ilikuwa ni hukumu, lakini Mungu kamwe hakutaka kuwa mataifa yaachwe milele. Wakati Mungu alipofanya agano lake na Abramu, aliweka wazi kuwa "Familia zote duniani zitabarikiwa" kupitia Abramu na uzao wake (Mwanzo. 12:3NLT). Mungu alikuwa anapanga kuyarejesha mataifa katika familia yake wakati fulani.

Paulo aliyajua haya yote. Katika mahubiri yake kwa wanafalsafa wa kipagani huko Athene alisema:

Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao, ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa-papasa, wakamwone, ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu . (Mdo 17:26–27NLT)

Kupitia Musa, Mungu aliwaonya watu wake yeye mwenyewe wasiabudu "jeshi la mbinguni" (Kumbukumbu. 4:19–20), maelezo haya yanapatikana kila mahali kwa wanachama wa baraza la Kimungu (1Wafalme 22:19). Mdo 17:26–27 inaweka bayana kwamba kusudi la Mungu ilikuwa angalau mataifa yangeendelea kumtafuta.

Lakini miungu iliyokuwa imewekwa juu ya mataifa haya iliingilia mpango huu kwa njia mbili.

Tuliona awali katika Zaburi 82:1 kwamba Mungu alikuwa amewakusanya miungu wa baraza. Zaburi nzima inatuambia kwa nini. Miungu ya mataifa ilikuwa imetawala mataifa kwa uonevu au dhuluma kwa njia ambazo zilikuwa kinyume na mapenzi ya Mungu wa kweli na kanuni za haki. Mungu aliwashutumu mapema tu kadri mkutano ulipoanza: "Hata lini mtahukumu kwa dhuluma, na kuzikubali nyuso za wabaya?" (Zaburi. 82:2 NLT). Baada ya kuwapiga kwa mistari miwili zaidi kwenye dhulumu zao, Bwana alionyesha namna miungu ilivyokuwa imeshindwa kuyasaidia mataifa kuondoka gizani na kuitafuta njia ya kumjia Mungu wa kweli: "Hawajui wala hawafahamu, hutembea gizani, misingi yote ya nchi imetikisika" (Zaburi. 82:5 NLT).

Chakusikitisha, Waisraeli walijeruhiwa kwa kuabudu miungu "asiyowapa yeye" (Kumb. 29:26; angalia pia 32:17) badala ya kumtafuta Mungu wa kweli. Majibu ya Mungu yalikuwa ya haraka na yenye ukali (Zaburi. 82:6–7): "Mimi nimesema, ndinyi miungu, na wana wa aliye juu, Nyote pia. Lakini mtakufa kama wanadamu, mtaanguka kama mmoja wa wakuu" (NLT).

Miungu ingepoteza hali yao ya kutokufa (Zaburi. 82:7) na kufa kama wanadamu. Tunajua kutokana na vifungu vingine kuwa hukumu hii ni kitu kinachohusiana na nyakati za mwisho (Isaya 34:1–4). Mwishoni mwa Zaburi 82, mwandishi anamatumaini ya siku ambayo hatimaye Mungu atajitwalia

mataifa kuwa urithi wake. Kama tutakavyoona baadae, atapata anachokitaka katika Agano Jipya.

Kumbukumbu la Torati 32 Mtazamo wa Ulimwengu

Kwa sababu ya mtazamo wa ulimwengu wa Kumbukumbu la Torati 32, *jiografia katika Biblia ni ya ulimwengu.* Ardhi yaweza kuwa takatifu, ikimaanisha imetolewa kwa ajili ya Yahweh, au ni uwanja wa mungu mwingine. Mtazamo huu wa ulimwengu unaonekana kwenye maeneo mengi kwenye Biblia. Kwa mfano, katika Agano la Kale kitabu cha Danieli kinaelezea mataifa ya kigeni yanayotawaliwa na "wakuu" wa kimungu (Dan. 10:13, 20–21). Mfano mwingine: Wakati Daudi alipokuwa akimkimbia mfalme Sauli, alilazimika kutoka Israeli na kwenda eneo la wafilisti katika 1 Samweli 26:19, Daudi akalia, "Wamenifukuza leo, nisishikamane na urithi wa Bwana, wakisema, Enenda, katumikie miungu mingine" (GNT). Daudi hakuwa anabadili miungu. Pia hakuwa anakataa kuwa Mungu alikuwepo kila mahali. Bali Israeli ilikuwa ni ardhi takatifu, sehemu ambayo ilikuwa inamilikiwa na Mungu wa kweli. Daudi alikuwa amekwama kwenye himaya au milki ya mungu mwingine.

Hadithi yangu maarufu ya Agano la Kale ambayo inayoleta hoja hii inapatikana katika 2Wafalme 5. Naamani alikuwa Jemedari wa jeshi la shamu. Pia alikuwa mkoma. Baada ya kufuata maelekezo ya Elisha kujiosha mwenyewe mara saba katika mto Yordani, kimiujiza aliponywa ukoma. Naamani alimwambia Elisha, "Najua ya kwamba hakuna Mungu duniani mwote, ila katika Israeli" (5:15). Nabii hakupokea malipo yoyote, hivyo Naamani kwa unyenyekevu akaomba apewe mzigo wa udongo wa baghala aende nao nyumbani. *Udongo*? Kwa nini kuomba udongo? Kwa sababu udongo ule ulikuwa wa Mungu wa Israeli. Ulikuwa mtakatifu.

Haikuwa ajali (bahati mbaya) tunapoona aina kama hiyo ya kuwaza kwenye Agano Jipya. Paulo anatumia istilahi kadhaa

kwa viumbe wa kimungu wenye chuki (Eph. 1:20–21; 3:10; 6:12; Kol. 1:16; 2:15): wakuu, mamlaka, nguvu, viti vya enzi. Ina nini kinachofanan? Zote zilikuwa ni istilahi zinazofahamika vyema zilizotumika kuelezea tawala za kijiografia.

Mtume Paulo aliandika nyaraka mbili kwa kanisa la korintho akizungumzia baadhi hali alizokuwa amezisikia. Kwenye waraka wa kwanza, aliwaambia viongozi wa kanisa kumfukuza mtu aliyekuwa anaishi katika dhambi ya zinaa isiyotubiwa (1Kor. 5:1–13). Kwa ujasiri, aliandika kwamba walitakiwa "kumtolea shetani mtu huyo" (1 Kor. 5:5). Ni kwa namna gani lugha hii inaleta maana yoyote?

Kauli ya Paulo, inakuwa na maana tu dhidi ya mtazamo wa ulimwengu wa jiografia ya ulimwengu wa Agano la Kale. Katika theolojia ya Agano la Kale, "sehemu" ya Yahweh ilikuwa Israeli na nchi aliyokuwa anawapa Israeli ya Kanaani. Uwepo wake ulitakasa ardhi—kuifanya takatifu. Awali, uwepo wa Yahweh ulikaa hekaluni. Wakati Israeli walipopumzika na kuweka kambi, sanduku la Agano liliwekwa katikati, kuifanya kambi ya Israeli kama ardhi takatifu. Baadae, baada ya Israeli kuchukua makazi katika Kanaani, uwepo wa Yahweh ulikuwa hekaluni, ukiitakasa nchi ya Ahadi kama ardhi takatifu—Yahweh na watu wake walikuwa nyumbani. Sasa, uwepo wa Yahweh unakaa ndani ya waumini—sisi ni hekalu la Mungu (1 Kor. 6:19; 2 Kor. 6:16; Rum. 8:9). Hiyo ina maanisha waamini, mwili wa Kristo, ndio watu wapya wa Mungu, Israeli mpya. Paulo anabainisha wazi katika Wagalatia 3:

> Wana halisi wa Ibrahimu, kwa hiyo, ni wale wanaoweka imani yao kwa Mungu....
>
> kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Yesu Kristo. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Hapana myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote

mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu. Na kama ninyi ni Wakristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi.. (Gal. 3:7, 26–29NLT)

Hivyo waamini na sehemu ambapo waamini wanapokusanyika ni ardhi takatifu, dhambi lazima ifukuzwe. Kama vile tu ardhi kuzunguka kambi ya Israeli na mataifa yaliyowazunguka chini ya utawala wa miungu wengine ilivyokuwa inachukuliwa kama ardhi isiyo takatifu, hivyo hivyo katika nyakati za Agano Jipya na sasa ulimwengu ulikuwa ardhi isiyo takatifu. Hivyo agizo la Paulo la kumtoa mwamini asiyetubu kwa ulimwengu, utawala wa Shetani. Kutolewa kutoka kanisani ilikuwa ni kurejeshwa katika eneo lisilo takatifu. Hapo ndipo dhambi inapopastahili.

## Kwa nini hili ni Muhimu

Jiografia ya ulimwengu ambayo ni matokeo ya hukumu ya Mungu kwa mataifa ya Babeli ni kuharibu mapambano ya Israel. Iliweka pia ngazi ya injili. Habari njema ya kazi ya Yesu msalabani ni kwamba watu wa Mungu sio Wayahudi peke yao tena bali wote wanaomwamini Yesu. (Gal. 3). Kadri wanafunzi wanavyoenda katika ulimwengu, utawala wa Shetani unabadilishwa na kuwa eneo la Mungu. Ufalme wa Mungu unaenea, na kujitwalia tena utawala wa mataifa.

Funzo ni kwamba ulimwengu *huu* sio makao yetu. Giza limeifunga dunia. Wasioamini kimsingi ni mateka wa majeshi ya kiroho. Wanaihitaji injili ili kuwekwa huru. Na usisahau: Ni injili ambayo ni silaha yetu. Hatujapewa mamlaka ya kukabiliana na mamlaka na nguvu moja kwa moja. Hakuna kipawa cha kiroho cha kiasi hicho tulichopewa na mitume. Bali kuieneza injili kwa uaminifu kutabadilisha wimbi. Wito mkuu ni mpango wa vita wa Kiroho. Tutajifunza zaidi kuhusu hilo kwenye sura zijazo.

Funzo jingine: tunapaswa kutazama kila kusanyiko la waamini wa kweli kama ardhi takatifu. Muonekano wa nje,

majengo, na ukubwa wa kusanyiko havihusiki kwa Mungu. Chenye maana ni kwamba, walipo wawili au watatu wamekusanyika, Yesu yupo kati yao (Mat. 18:20). Sehemu ni takatifu. Kila kusanyiko, haijalishi ni dogo kiasi gani au halijulikani, lipo kwenye mstari wa mbele wa vita ya kiroho. Kila kanisa lina kazi hiyo hiyo. Nguvu za giza hazitashinda.

Tutaliangalia tena wazo la jiografia ya ulimwengu tutakapoingia kwenye huduma ya Yesu. Kwa sasa, mstari wa mapambano umeshachorwa. Mataifa ya ulimwengu yamehukumiwa na kunyang'anywa urithi na Mungu. Ni wakati wake wa kuanza upya na kuchonga sehemu yake mwenyewe na watu wake.

# SURA YA SITA

## Neno, Jina, na Malaika

**K**atika sura ya mwisho tulijifunza kuhusu jiografia ya ulimwengu wa Biblia. Kwa kukabiliana na uasi wa wanadamu kwenye mnara wa babeli, Mungu aliyaacha mataifa. Aliyatoa/aliyagawa kwa wanachama wa baraza lake la mbinguni, wana wa Mungu (Kumbkumbu. 32:8–9). Kuziba nafasi ya mataifa yaliyoachwa-sasa, angeumba watu wapya, taifa lake mwenyewe. Wangekuwa mawakala wake kuhuisha ufalme wake duniani. Lakini kazi hiyo ingethibitisha kuwa mapambano mabaya, kwa vile miungu mingine na watu wa maeneo yao wangekuwa maadui wakubwa wa Israeli na Mungu.

Watu wapya wa Mungu wangeanza na mtu aliyeitwa Abramu, ambaye jina lake baadae angebadilisha kuwa Ibrahimu. Mara baada ya hukumu pale Babeli, Mungu alimtembelea.

### Ibrahimu akutana na Neno

Wakristo wengi wanafahamu Mungu alipomtembelea Ibrahimu Mwanzo 12. Mungu anamwambia Ibrahimu aondoke nyumbani kwake na kwenda mahali ambapo hajawahi kupaona. Mungu anaahidi kumuongoza. Anamwambia Ibrahimu atakuwa Mungu wake na kumpa ahadi maalumu ya Agano. Atamuwezesha Ibrahimu na Sarah kupata mtoto, ingawa wote ni wazee. Kutoka huyo mtoto watakuja watu wengi watu ambao wataunda familia mpya ya Mungu. Kupitia wao mataifa yatabarikiwa.

Huwa tunafikiri tukio hili la Ibrahimu kukutana na Mungu ilikuwa ni sauti toka mbinguni au katika kichwa cha Ibrahimu. Au pengine Mungu aliendа katika ndoto. Biblia iko wazi kwamba Mungu alifanya kitu hicho kwa manabii na watu

wengine. Lakini hicho sicho kilichotokea kwa Ibrahimu. Mungu alifanya kitu kikubwa zaidi. Alikuja kama mtu. Yeye na Ibrahimu walizungumza ana kwa ana.

Tunapata dokezo la hili katika Mwanzo 12:6–7. Biblia inasema Mungu alimtokea Ibrahimu. Sura au milango mitatu baadae, Mungu anatokea tena (Mwanzo. 15:1–6). Wakati huu Mungu anakuja kwa Ibrahimu kama "Neno la Bwana" katika *maono.* Hii haikuwa sauti kichwani, kwa kuwa "Neno" alimtoa Ibrahimu nje na kumuonyesha nyota na kumwambia kwamba uzao wake ungekuwa hauhesabiki (Mwanzo. 15:5).

Mungu alimtokea Ibrahimu kama mtu katika matukio mengine (Mwanzo. 18). Alifanya hivyo hivyo kwa Isaka (Mwanzo. 26:1–5), mwana aliyeahidiwa na Mungu,na Yakobo mwana wa Isaka (Mwanzo. 28:10–22; 31:11–12; 32:24–30).

"Neno" au sauti ya Mungu kama njia ya kumwelezea Mungu katika mfumo wa mwanadamu inajitokeza kwenye maeneo yasiyotarajiwa. Moja ya matukio yangu ninayoyapenda linapatika katika 1Samweli 3. Mtoto Samweli aliendelea kusikia sauti ikimuita usiku wakati alipokuwa akijaribu kulala. Hatimaye Eli, kuhani aliyeishi na Samweli na ambaye Samweli alimtumikia, aligundua ilikuwa ni Mungu. Katika mstari wa 10, Mungu alimjia tena Samweli: "Bwana akaja, akasimama, akaita vile vile kama kwanza 'Samweli! Samweli' " (GNT). Tunajua huyu alikuwa Mungu katika mfumo wa mwanadamu kwa sababu maelezo yanaonyesha akisimama, na kwa sababu mwishoni mwa sura ya (1Samweli. 3:19) inasema "Neno la BWANA" lilikuwa na mazoea ya kuendelea kumtokea Samweli.

Nabii mwingine ambaye "Neno la Bwana" lilimjia katika mfumo wa mwili wa mwanadamu alikuwa Yeremia. Katika Yeremia 1, ambapo anaitwa kuwa nabii, Yeremia anasema "Neno" lilimjia. Yeremia alilitambua "Neno" kama Mungu

mwenyewe. Bwana akamgusa *kwa mkono wake.* (Yeremia. 1:1-9).

## Mungu katika Umbo la Mwanadamu

Mungu kutokea kama mtu ni utaratibu katika Agano la Kale, mbali nyuma kabla ya ujio wake kama Yesu wa Nazareti. Wakati ukifikiri kuhusu hilo, linaleta maana. Mungu ni tofauti kabisa na sisi. Vidokezo vya Biblia kwamba hakuna mwanadamu anaweza kumwona Mungu, utukufu wa uwepo wa kweli, na akaishi. Wakati ambapo wahusika walipomwona Mungu dhahiri walitarajia kufa (Mwanzo 32:30; Kumbukumbu 5:24; Waamuzi 6:22-24). Hawakufa kwa sababu Mungu alichuja uwepo wake kupitia kitu ambacho akili ya mtu ingeweza kuelewa—moto, wingu, na mara nyingi zaidi kuliko Wakristo wengi wanavyojua, mtu.

Katika maeneo mengi, Muonekano wa Mungu katika umbo la mwanadamu unaelezewa kama "Malaika wa Bwana." Malaika ni mhusika anayefahamika. Kwa mfano, alimtokea Musa katika mwali wa moto uliotoka katikati ya kijiti (Kutoka 3:1-3). Mungu katika kijiti aliahidi kumtumia Musa kuwaongoza watu wake kutoka Misri. Mungu alikuwa amemtokea Yakobo waziwazi katika ndoto huko Betheli (Mwanzo. 28:10-22), ambapo alikuwa ametambulika kama Bwana (Yahweh). Baadae malaika wa Mungu alimjia Yakobo katika ndoto nyingine na kumwambia wazi kwamba yeye alikuwa ndiye Mungu yule yule aliyekutana naye awali huko Betheli (Mwanzo 31:11-12).

Walimu wengi wa biblia wanasita kumtambulisha malaika huyu kama Mungu mwenyewe. Bali kuna dalili kadhaa dhahiri kuwa ndiye. Pengine ya muhimu zaidi ilitokea muda mfupi baada ya Mungu kumpa Musa sheria. Wakati waisraeli wanajiandaa kwa safari ya kwenda nchi ya ahadi, Mungu anamwambia Musa:

Tazama, mimi namtuma malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengezea. Jitunzeni mbele yake, mwisikize sauti yake, wala msimtie kasirani maana hatawasamehe makosa yenu, kwa kuwa jina langu limo ndani yake.

Lakini ukiisikiza sauti yake kweli, na kuyatenda yote ninenayo mimi, ndipo mimi nitakuwa ni adui wa adui zako na mtesi wa hao wakutesao (Kutoka. 23:20–22)

Huyu sio malaika wa kawaida. Malaika huyu anaweza kusamehe dhambi (au asisamehe). Malaika huyu ana jina la Mungu ndani yake. Maelezo hayo ni ya ajabu lakini ya muhimu. "Jina" ilikuwa ni njia ya Agano la kale ya kumwelezea Mungu mwenyewe, uwepo au Roho wa Mungu. Kwa mfano, Isaya 30:27–28 inatoa jina la Bwana kama mtu —kama Mungu mwenyewe:

Tazama, jina la Bwana linakuja kutoka mbali sana,

linawaka kwa hasira yake, kwa moshi mwingi sana unaopaa juu;

midomo yake imejaa ghadhabu;

na ulimi wake ni moto ulao;

na pumzi yake ni kijito kifurikacho.

Hata leo Wayahudi waangalifu wanamwita Mungu kwa kusema *ha-shem* ("jina").

Namna nyingine ya kujua huyu Malaika alikuwa Mungu katika umbo la mwanadamu ni kwa kulinganisha Kutoka 23:20–22 na vifungu vingine. Malaika aliyekutana na Musa kwenye kichaka kinachowaka, Malaika mwenye jina la Mungu ndani yake, kwa hakika waliwatoa waisraeli toka Misri hadi nchi ya Ahadi (Waamuzi 2:1–3). Lakini pia Bwana alifanya hivyo (Joshua 24:17–18) Na uwepo wa Mungu mwenyewe (Kumbukumbu 4:37–38). Bwana, Uwepo, na Malaika wa

Bwana ni njia tofauti za kutaja kitu kimoja: Mungu. Lakini Malaika ni umbo la mtu.

Moja ya vifungu katika Biblia vinavyofanya hoja hii iwe ya lazima pia kimefichika sana. Watu wachache ndiyo wameigundua. Ni eneo la kifo cha mauti. Kabla hajafa, Yakobo anataka awabariki wana wa Yusufu. Katika Baraka yake anakumbuka matukio katika maisha yake. —baadhi ya kukutana kwake na Mungu. Anaanza Baraka yake kwa namna hii (Mwanzo 48:15–16):

> Mungu ambaye baba zangu, Ibrahimu na Isaka, walienenda mbele zake, yeye Mungu aliyenilisha, maisha yangu yote, hata siku hii ya leo, naye malaika aliyeniokoa na maovu yote ...

Kisha, kwa kiasi kikubwa, katika mstari wa 16 anaomba, "Awabariki vijana hawa" (NIV, msisitizo umeongezwa). Hakusema, "Wawabariki vijana hawa," kama anazungumzia watu wawili, Mungu na Malaika. Anawaunganisha pamoja katika maombi: Na awabariki vijana hawa.

Hasa ya kuzingatia zaidi ni Waamuzi 6, wito wa Gidion. Pale wote Bwana na Malaika wa Bwana wanapatikana *katika eneo moja* (Waamuzi 6:22–23). Hata katika Agano la Kale, Mungu alikuwa zaidi ya nafsi moja, na moja ya hizo nafsi ilikuja kama mtu.

## Yesu: Neno, Jina, na Malaika

Maelezo ya Mungu tuliyokwisha kupitia hadi sasa yanapaswa kuwa yanafahamika—haya yote ni matoleo ya Agano la Kale ya namna gani Agano Jipya linazungumza kuhusu Yesu.

Ibrahimu alikutana na Neno, Mungu katika umbo la mwanadamu. Katika Yohana 1:1, mtume anaandika: "Hapa mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Katika msitari wa 14, Yohana

anasema huyu Neno “alifanyika mwili akakaa kwetu.” Wakati Myahudi wa karne ya kwanza akisoma injili ya Yohana, akili yake itampeleka kwa Mungu mwenyewe. Kwa hakika, hata Yesu alidai kuwa Ibrahimu “aliiona siku yake” na kwamba alikuwepo kabla ya Ibrahimu (Yohana 8:56–58).

Musa alikutana na Malaika wa Bwana, Mungu katika umbo la mwanadamu, katika kichaka kinachowaka moto na baadae. Malaika aliwatoa Israeli toka Misri hadi nchi ya ahadi. Lakini Yuda aliandika katika waraka wake mfupi, “Tena napenda kuwakumbusha, ijapokuwa mmekwisha kujua haya yote, ya kwamba Bwana, akiisha kuwaokoa watu katika nchi ya Misri, aliwaangamiza baadae wale wasioamini (1:5). Malaika alikuwa Mungu katika umbo la mwanadamu. Malaika alikuwa nafsi ya pili ya Utatu ambaye angezaliwa baadae na Bikra Maria.

Uwepo wa Mungu, jina, ulimfanya Malaika huyu kuwa tofauti na wengine wote. Kuna nyakati, katika Agano Jipya, Yesu anamzungumzia Mungu Baba kama Jina. Katika maombi yake kwenye bustani ya Gethsemane,kabla tu ya kukamatwa kwa ajili ya jaribu ambalo lingepelekea kusubishwa kwake, Yesu aliomba: “Na sasa, Baba, unitukuze mimi pamoja nawe, kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe kabla ya ulimwengu kuwako Jina lako nimewadhihirishia watu wale ulionipa katika ulimwengu.... Nami niliwajulisha jina lako. ” (Yohana 17:5–6, 26). Alimaanisha nini kwenye kauli hiyo ya mwisho? Yesu alikuwa hasemi, aliwafanya watu walijue jina la Mungu. Walikuwa Wayahudi. Walilijua jina la Mungulilikuwa ni Yahweh. Walikuwa na Agano la Kale. Wangeweza kulitazama jina la Mungu kwenye maelfu ya mistari. Wakati Yesu aliposema amelidhihirisha jina Mungu kwa watu, alimaanisha alikuwa amemdhihirisha *Mungu mwenyewe* kwa watu. Alikuwa Mungu mbele ya macho yao. *Alikuwa ni jina aliyefanyika mwili.*

## Kwanini Hili ni Muhimu

Tumetoka mbali vyakutosha katika somo letu kupata msingi wa kibiblia wa ardhi. Hadithi zote za Biblia unazozijua zimefanyika katika mazingira ya vita vya kiroho vikubwa katika ulimwengu usioonekana. Ni mgongano wa mshindi- chukua-wote wa miungu.

Katika mtazamo wa Kibiblia wa ulimwengu usioonekana, Mungu ana maadui wakubwa, miungu mingine aliwaumba ambao walikuwa waaminifu kwake lakini wakaiendea njia yao wenyewe. Miungu hii iliyoasi ndiyo Paulo anaielezea kama nguvu za giza, wakuu wa giza, mamlaka, na falme au viti vya enzi vya ulimwengu usioonekana (Efeso. 6:11; Kol. 1:16). Bado vipo hapa. Hakuna chochote katika Agano Jipya kinachotuambia viliondoka. Wanaishi kupinga utawala wa Mungu na kumkosesha kuungana milele na familia yake anayoipenda ya wanadamu kupitia injili.

Moja ya hizi nguvu za giza ni bwana wa mauti. Ana madai ya haki kwa wanadamu, tangu udanganyifu wake kwa Adamu na Hawa uliopelekea kupoteza kutokufa. Na hilo lilikuwa lengo lake—uharibifu wa watu wa Yahweh. Ndicho hicho ambacho wana wa Mungu waliokuwa wapinzani walikuwa nacho akilini wakati Waisraeli walipoingia Kanaani: Ua au uuawe kuwazuia watu wa Mungu wasiimiliki nchi. Mara Israeli walipoingia katika nchi, lengo la nguvu za giza lilibakia lile lile, bali mkakati wao ulibadilika: Washawishi watu wa Mungu katika kuiabudu miungu mingine, na kisha Yahweh atawaondoa kwetu. Na hicho ndicho kilichotokea. Mungu aliwapeleka watu wake uhamishoni.

Lakini nguvu za giza zilijua kitu kingine zaidi: Yahweh hatauacha mpango wake. Laana kwa muasi halisi iliyotolewa awali, siku moja mzaliwa wa Hawa, ambaye angebadilisha kushindwa kwa mwanadamu katika Edeni, angelikuja. Walijua katika hatua Fulani huyo aliyeahidiwa angelitokea—ingawa

kama Paulo alivyotuambia hawakujua kwa hakika kile Mungu alichokuwa anapanga (1 Kor. 2:6–8; Efeso. 3:10; 6:12). Hiyo ni kwa sababu ilikuwa siri, kwa makusudi ilifichwa kwa wote na Aliye Juu.

# SURA YA SABA

## Kanuni za Ushiriki

Hadithi yetu hadi sasa: Mungu aliyatupilia mbali mataifa na watu wao pale Babeli. Miungu wadogo waliokabidhiwa kwao wakachukua madaraka (Kumbukumbu 32:8–9). Wakati Mungu alipoanza upya na Ibrahimu, ilikuwa wazi kuwa alipanga kuyarejesha mataifa kupitia hamasa ya Israeli (Mwanzo. 12:3). Lakini miungu ya mataifa ingelazimishwa kuachia mamlaka yao na ibada (Zaburi 82:6–8). Hii ilimaanisha mgogoro—Kote katika ulimwengu unaoonekana na usioonekana. Mara tu ilipokuwepo Israeli, ilikuwa kwenye mila za miungu

### Yahweh ni Nani?

Haichukui muda katika hadithi ya biblia kwa Israeli kuhitimisha katika nafasi dhahiri. Habari ya Yusufu (Mwanzo 37–50) inaelezea kwanini Israeli walienda Misri. Uaminifu wa Mungu ulibadili madhara aliyokusudiwa na ndugu zake kuwa wokovu wa Israeli kutokana na njaa (Mwanzo. 46:3–4; 50:20). Kwamba Mungu hakuwaambia Israeli kuondoka Misri moja kwa moja pia ilikuwa ni kwa makusudi. Mungu alijua Farao aliyemheshimu Yusufu angekufa na nafasi yake kuchukuliwa na adui (Kutoka 1). Alikuwa ameona kuwa Misri watawafanya Israeli kuwa watumwa (Mwanzo. 15:13–16). Pia alijua kuwa angewaokoa Israeli wakati utakapotimia (Mwanzo 46:4).

Lakini kwa nini kusubiri? Mungu wakati wote ana sababu nzuri ya mateso. Hatuwezi tu kuona wakati wote. Kwa muktadha huu, ingawa, maandiko yanaweka bayana.

Baada ya Musa kutoroka Misri na kujipatia makao huko nyikani, Mungu alimuita katika kichaka kinachowaka (Kutoka 3:1–14) ampeleke tena Misri. Maagizo yake yalikuwa rahisi: Mwambie Farao “Awaachilie watu wangu waende” (Kutoka.

5:1). Farao alikuwa na mawazo mengine. Alikuwa ni mungu katika mwili katika Misri, alama ya utukufu wake na nguvu. Hangeruhusu Mungu asiyeonekana wa wachungaji wa kiebrania kumwambia nini cha kufanya. Hata hakujua kama Mungu wa Musa alikuwa wa kweli. Alijibu kwa dhihaka, “BWANA ni nani, hata niisikilize sauti yake, na kuwapa Israeli ruhusa waende zao?” (Kut. 5:2).

Alikuwa amekaribia kupata jibu—lile ambalo lingemuumiza. Mungu alikuwa amemweka. Mungu alikuwa amemwambia Musa, “Nitaufanya mgumu moyo wake, naye hatawapa ruhusa hao watu waende zao” (Kutoka 4:21). Mungu alikuwa na vita vya kupigana. Baada ya kuwa wamewakandamiza Waisraeli kwa karne nyingi, ulikuwa ni wakati wa Misri na miungu yake kuadhibiwa. Ugumu wa Farao ulikuwa sehemu ya mpango huo. Biblia inatuambia mapigo yalilengwa kwa miungu ya Kimisri —hasa lile la mwisho, vifo vya wazaliwa wa kwanza. (Kutoka 12:12; Hesabu 33:4), ambalo liligeuka kuwa shambulio la moja kwa moja kwa nyumba ya Farao: “Hata ikawa, usiku wa manane BWANA akawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, tangu mzaliwa wa kwanza wa Farao aliyeketi katika kiti chake cha enzi, hata mzaliwa wa kwanza wa mtu aliyefungwa katika nyumba ya wafungwa, na wazaliwa wa kwanza wote wa wanyama.” (Kutoka 12:29).

Farao alikuwa amemdhihaki Mungu, na meza zilikuwa zimegeuzwa kwa kasi. Kama ambavyo Paulo aliliweka baadae, “Msidanganyike Mungu hadhihakiwi, kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna.” (Gal. 6:7). Kupigwa Misri kulitoa njia ya kuachiliwa kwa Waisraeli toka Misri na kulikuwa na athari iliyokusudiwa. Watu kutoka mbali kama Kanaani walisikia kuhusu kipigo Mungu alichowapiga Misri na miungu yake (Josh. 2:8–10; linganisha na Kutoka 15:16–18; Josh. 9:9). Yethro, Kuhani wa Midiani, mkwewe Musa, alihitimisha somo wakati Musa aliporejea: “Sasa najua kuwa Bwana ni mkuu kuliko miungu yote” (Kutoka 18:11LEB).

Sio ajabu tena kwamba Musa, kwenye upande wa pili wa Bahari ya Shamu, anauliza swali la kejeli akimdhihaki Farao na jeshi lake lililoangamia: *Katika miungu ni nani aliye kama Bwana*? (Kutoka 15:11).

Mara baada ya kutoka Misri kupitia Bahari ya Shamu, Waisraeli walijua kule walikokuwa wanapelekwa. Walikuwa wanaenda kukutana na Mungu wao katika makao yake ya mwishoni ya duniani na makao makuu, Mlima Sinai.

Kwa kweli, Waisraeli hawakujua sana kuhusu Mungu. Biblia haikuwepo *kabisa* wakati wa kutoka. Uelewa pekee waliokuwa nao Waisraeli kuhusu Mungu waliupata kupitia hadithi walizozisikia kutoka kwa wazazi wao, toka kizazi hadi kizazi. Kusoma hadithi kwenye Biblia sasa, tunaweza kuona wazi kile Mungu alichokuwa anakitaka. Waisraeli walikuwa na Mengi ya kujifunza. Sinai lilikuwa ni darasa.

Israeli —Familia ya Mungu na Wawakilishi wa Kidunia.

Wakati Musa alipokuwa amesimama mbele ya Farao, kabla ya kutoka, alimwambia Bwana alikuwa ana ujumbe: "Israeli ni mwanangu mimi, mzaliwa wa kwanza wangu... mpe mwanangu ruhusa aende, ili apate kunitumikia" (Kutoka 4:22–23LEB). Wazo hilo la Mungu kuwa na mwana—katika hili, akimaanisha wazao wote wa Ibrahimu—ni muhimu. Inaturejesha nyuma kwenye uumbaji wa Mungu wa Adamu na Hawa.

Mungu alitaka familia ya wanadamu. Alitaka kuishi kwenye uumbaji wake, duniani, na watu aliowafanya. Alitaka familia yake isiyoonekana na familia yake ya wanadamu kuishi nae na kumtumikia. Alitaka watu waongezeke na Dunia yote iwe kama Edeni. Lakini Mungu alipouacha ubinadamu kwenye mnara wa Babeli, hakuwa na watoto— hadi alipomuita Ibrahimu. Israeli ilikuwa familia mpya ya Mungu. Ulikuwa ni wakati wa kurejea kwenye mpango wa awali. Kama Adamu na Hawa walivyokuwa sura ya Mungu, Israeli wangetimiza jukumu hilo sasa.

Kurudi Sinai ilikuwa ni kwenda nyumbani. Hata baraza la mbiguni lilikuwepo pale, likitazama kadiri mpango wa Mungu ulivyokuwa ukiwekwa kwenye matendo. Walikuwa mashuhuda wa Agano Jipya kati ya Mungu na watu wake— sheria.

### Sheria ya Mungu—Iliyotolewa na Baraza la Mungu.

Je ilikushangaza wakati niliposema baraza la mbinguni lilikuwepo pale Sinai wakati Mungu alipotoa Amri Kumi? Kama ulishawahi kuona filamu kuhusu kutoka na safari ya kuelekea Sinai, hukuwaona malaika. Lakini Biblia inasema walikuwepo pale. Na hata inasema walitoa sheria ya Mungu. (Mdo 7:52–53; Ebrania. 2:1–2).

Pia inasema Sheria iliandikwa "Kwa kidole cha Mungu" (Kumb 9:9–10). Lugha hiyo inapaswa kufahamika—Mungu katika umbo la mwanadamu. Mungu alikuwepo Sinai,akionekana kama mtu, kama tu katika hadithi za kwenye Mwanzo kuhusu Malaika wa Bwana. Yeye na jeshi lake la mbinguni walitoa sheria kwa Musa na kwa Israeli.

Baada ya utoaji wa sheria, Musa, Haruni, wana wa Haruni, na watu sabini miongoni mwa wazee wa Israeli walimwona Mungu wa Israeli katika umbo la mwanadamu. Wakati huu walikutana kwa chakula (Kutoka 24:9–11). Kama ilivyokuwa katika chakula cha mwisho cha jioni wakati wa Yesu kilivyopiga muhuri agano jipya la damu yake, chakula hiki kilikuwa cha kusherekea Agano jipya na Israeli katika Sinai—Sheria.

Mungu aliwapa sheria Israeli kwa hiyo wangekuwa watakatifu (Walawi. 19:2). Alitaka Israeli watengwe na watu wengine, watofautishwe na kila mmoja kama familia yake yeye mwenyewe. Kama Mungu alivyo tofauti kabisa na miungu wengine na kila kitu cha kidunia, hivyo watu wa Mungu wanahitajika kuwa tofauti na watu wengine.

Utakatifu ulimaanisha nini? Kulikuwa na wazo gani nyuma yake? Utakatifu haukumaanisha kuwa wa ajabu. Utakatifu

ulikuwa ni kutambulishwa na Bwana, kujitoa kwa Mungu na kufurahia mambo yote mema katika maisha yale yanayokuja kwa kuwa sawa na Mungu. Mungu alitaka Israeli iyavutie mataifa mengine ili yarejee kwake (Kumbukumbu 4:6–8; 28:9–10). Hii ndiyo sababu Biblia inaiita Israeli "ufalme wa makuhani" (Kutoka 19:6) na "na nuru ya mataifa" (Isaya 42:6; 49:6; tazama pia 51:4; 60:3). Taifa zima lilirithi nafasi ya Ibrahimu kuwa Baraka kwa mataifa yote (Mwanzo 12:3).

### Kuamini Uaminifu

Kuwa sawa kwa Mungu ni njia nyingine ya kuzungumza kuhusu wokovu. Lakini licha ya kile ambacho tumekuwa tukifundishwa katika shule ya jumapili, wokovu haukuja kwa Israeli kwa kuzitii sheria, kwa kufuata sheria. Kwamba ni katika Agano la Kale au Jipya, wokovu kamwe haupatikani, au hata kustahili. *Unatolewa* kwa Neema ya Mungu kutokana na Imani.

Israeli pia, kama ilivyokuwa kwetu tuliozaliwa baada ya kifo cha Kristo na kufufuka walipaswa kuwa na imani. Walitakiwa *kuamini* Mungu wao alikuwa Mungu wa miungu yote, kutumaini kuwa amewafanya watu wake. Wao pekee ndiyo walikuwa na nafasi ya kumfikia Mungu wa miungu. Sheria haikuwa namna gani Waisraeli walipata wokovu—ilikuwa ni namna gani walionyesha uaminifu kwa Mungu waliyemwamini. Wokovu kwa Muisraeli ilikuwa ni imani kwa ahadi na tabia za Mungu wa miungu na kuhusu kukataa kuabudu mungu mwingine. Ilikuwa inahusu imani na uaminifu toka moyoni, sio kupata sifa au kuthibitishwa kwa Mungu (Nahau).

Mfalme Daudi alifanya mambo mabaya kama kufanya zinaa na kupanga mauwaji (2 Sam. 11). Kulingana na sheria, alikuwa mvunja sheria na alistahili kufa kwa uhalifu wake. Hata hivyo, hakuyumba kamwe katika imani yake kwa Bwana kama Mungu aketiye Mahali pa Juu sana. Kamwe hakubadili

uaminifu wake kwa mungu mwingine. Na Mungu alikuwa na rehema kwake.

Ukweli ni huo huo katika Agano Jipya. Kuiamini injili inamaanisha kuamini kwamba Mungu wa Israeli alikuja duniani kama mtu, akajitolea kufa msalabani kama dhabihu ya dhambi zetu, na akafufuka tena siku ya tatu. Lazima tulishike hilo kwa imani na kuonyesha uaminifu wetu kwa Yesu kwa kuiacha miungu mingine yote. Haijalishi kile ambacho hao miungu wengine wanaweza kusema kuhusu wokovu wetu, Biblia inatuambia hakuna wokovu katika jina lingine lolote isipokuwa jina la Yesu (Mdo 4:12) na imani hiyo lazima ibakie wakati wote (Rum. 11:17–24; Heb. 3:19; 10:22, 38–39). Kushindwa kwa mtu binafsi sio sawa na kumchanganya Yesu na mungu mwingine—na Mungu anaweza kusema tofauti.

## Kwanini Hili ni Muhimu

Kuna mifano mingi ya kuvutia katika kutoka na kile kilichotokea pale Sinai. Sehemu ambayo Musa na wengine walikula chakula na Mungu katika umbo la mwanadamu pale Sinai linakamata umakini wetu mara moja. Kuna wazee sabini wako na Musa. Kama ukihesabu mataifa katika Mwanzo 10 ambayo Mungu aliyaacha baada ya tukio la kwenye mnara wa Babeli, unapata sabini. Mataifa hayo yalikabidhiwa kwa wana wa Mungu—miungu wengine wadogo—wakati Mungu wa Israeli alipoyahukumu mataifa. (Kumbukumbu 4:19–20; 32:8–9). Kwanini wazee sabini, wana wa Mungu sabini, na mataifa sabini yasiyorithiwa?

Mfanano huu una makusudi. Wakati Yesu alipoanza huduma yake duniani, aliwatuma wanafunzi sabini (Luka 10:1). Huu ulikuwa ni utangulizi wa Wito Mkuu . Namba hiyo ilileta ujumbe kuwa wanafunzi wa Yesu wangeyarejesha mataifa kwa utawala wa ufalme wa Mungu. ufalme huo ungefikia umbo lake la  mwisho katika siku za mwisho katika Edeni mpya ya ulimwengu Ufunuo 21–22. Marudio ya namba sabini ni

ujumbe: Familia mpya ya Mungu duniani, Israeli—wana wa Ibrahimu—ingekuwa ni njia ya kurejesha kile tulichopoteza.

lakini haikuishia hapo. Mtume Paulo aliandika katika Galatia 3 kwamba waamini wamerithi ahadi zilizotolewa kwa Ibrahimu. Kila anayemwamini Yesu ni mwana wa Ibrahimu kwa njia ya imani (Gal. 3:26–29). Hii ina maanisha mimi na wewe tumepewa kazi ya kuyarejesha mataifa toka kwa miungu. Ni kazi yetu kuwageuza watu toka kwenye utawala wa kiroho wa miungu mingine kwenda imani kwa Yesu. Sisi ni baraza jipya la Mungu duniani. Na tukisha tukuzwa, tutaungana na familia yake kimungu katika Edeni mpya..

Biblia inaonyesha mawazo haya katika maeneo mengi. Kitabu cha ufunuo kinaonyesha waamini wakirithi utawala wa mataifa pamoja na Yesu katika siku za mwisho (Ufunuo 3:21). Hii ina maanisha tutawaondoa wana wa Mungu ambao wameyatawala mataifa haya tangu Babeli. Hii ndiyo sababu Yohana anasema waaminio wana uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu (Yohana 1:12; linganisha na 1 Yohana 3:1–3); Kwa hakika tutawaondoa miungu-lakini wana wa Mungu wafanyao vita katika siku za mwisho.

Na hii pia ndiyo sababu Paulo, wakati akiwaandikia waaminio waache kupeleka mashauri yao kwenye mabaraza kusuluhisha migogoro, “Hamjui ya kuwa tutawahukumu mataifa?” (1Kor. 6:3). Tutakapofanywa miungu (tukuzwa) katika dunia mpya, *tutakuwa juu ya malaika*. siku moja tutafanywa kuwa kama Yesu (1Yohana 3:1–3; 1 Kor. 15:35–49) na kutawala pamoja naye juu ya mataifa (Ufunuo 2:26) yanayotawaliwa na miungu yenye chuki kwa sasa. Waaminio, uzao wa Ibrahimu wa kiroho, hatimaye watarejesha dhamana ya urithi wa mataifa pamoja na laana ya mauti iliyotokana na anguko la Edeni.

Tunapaswa kuishi kama vile tunaiamini hatima hii. Kila kitu katika Agano la kale mpango unatuelekea sisi. Fikiria nyuma pale Edeni.

Mungu alitaka familia zake mbili—moja ya kimungu, nyingine ya wanadamu—kuishi na kutawala pamoja katika Edeni. Mpango huu ulihujumiwa na uasi, lakini ukafufuliwa na kuwaokoa Israeli toka Misri. Kutoka katika watoto wa Ibrahimu angelikuja Masihi, ambaye angefuta kushindwa katika Edeni (Mwanzo 3:15). Bila Muisraeli, tusingekuwa na hatma..

Na hiyo ndiyo sababu hasa kwanini miungu na wafuasi wao wangejaribu kuifuta Israeli.

# SURA YA NANE

## Mahali Patakatifu

Waisraeli walitumia zaidi ya mwaka katika Mlima Sinai. Kwanini muda mrefu hivyo? Walikuwa tayari wameshaingia katika Agano na Mungu na kupokea Amri Kumi. Lakini bado walikuwa na mengi ya kujifunza. Ilikuwa ni kitu kimoja kuahidi kumwamini na kuwa mwamwinifu kwa Mungu wa Mababa zao, Ibrahimu, Isaka, na Yakobo. Ilikuwa ni kingine kujua Mungu alitarajia nini na yukoje.

### Wazo la Utakatifu

Sheria nyingi za ajabu na matendo ya Agano la kale zimetokana na mahitaji ya kuwafundisha watu kuwa Mungu ni *tofauti* na kitu kingine chochote. Katika asili na tabia yake, ni wa pekee: ni tofauti kabisa na ubinadamu na chochote kile. Kwa Israeli, huo ulikuwa ni ukweli ambao ulipaswa kuimarishwa nyakati zote. Vinginevyo, Mungu angeweza kufikiriwa kuwa wa kawaida.

Neno la Kibiblia la wazo la upekee wa Mungu ni *utakatifu*. Linamaanisha "kutengwa" au "kuwa tofauti" Wazo hili sio lazima liwe kuhusu maadili—kuhusu wazo kuwa tunapaswa kuishi namna fulani kuonyesha viwango tofauti vya maadili vya Mungu— japo hilo linapaswa kuwepo (Walawi 19:2).

Mungu hakufurahia tu kuwapa Waisraeli ufanunuzi wa kiakili wa utakatifu. Alitaka wazo la upekee wake lizame na kujaa maishani katika Israeli ya kale. Biblia inatuambia hili lilikamilishwa kupitia mila (matendo ya mfano) na kwa sheria za kukaribia maeneo matakatifu.

## Kwa jinsi gani Mungu ni "Mwingine"?

Jibu fupi kwa swali hili ni "kwa namna zote" lakini hilo ni la kawaida sana. Biblia ina maana zaidi duniani, na mila na kanuni kwa jamii ya Israeli inayoishi vinaonyesha hilo.

Kwa mfano, Biblia inatufundisha kwamba Mungu hakuwa tu chanzo cha uzima wa Israeli—*alikuwa* uzima. Mungu sio wa dunia hii, mahali ambapo kuna mauti, magonjwa, na kutokukamilika. Ulimwengu wake sio wa kawaida. Ulimwengu wetu ni duniani. Sehemu ya kidunia anayokaa inafanywa takatifu na *ulimwengu mwingine* kwa uwepo wake. Mahali tunapokaa ni pa kawaida. Mungu ni kinyume cha kawaida.

Katika Israeli zamani, mawazo haya yalitolewa kutokana na ukweli kwamba watu walipaswa kualikwa na kutakaswa ili waweze kukaa sehemu moja na Mungu. Sheria nyingi katika Agano la kale zinasimamia huu utakasaji.

Waisraeli wangeweza kukoseshwa sifa ("kunajisiwa") toka sehemu takatifu na shughuli mbalimbali na hali. Kufanya ngono, kupoteza damu, ulemavu wa aina fulani, na kugusa mwili uliokufa (wa mtu au mnyama) yote yalimfanya Muisraeli kunajisika. Waisraeli walikatazwa kula aina fulani za ndege zilizokula wanyama waliokufa (mfano, Tai, Mwewe; Walawi. 11:13–19) Au wanyama wale ambao wanaweza kukutwa kwenye mzoga au ndani ya mzoga (mfano, mjusi, panya; Walawi 11:24–40).

Katika matukio haya, unajisi haukuhusu maadili bali ulihusishwa na kupoteza maisha na kutokuendana na ukamilifu wa Mungu. Ingawaje mantiki ni rahisi, inaonekana kitu kigeni kwenye akili zetu za kisasa. Kupoteza damu na manii vilieleweka kama *upotevu* kile kilichotengeneza na kufanya uzima uwepo. Mungu hakupaswa kuhusishwa na kupotea kwa uzima bali na kuwa *mtoa* uzima. Kuhitaji "utakaso" baada ya kupoteza maji maji hayo ilikuwa ni ukumbusho wa asili ya Mungu. Vile vile "utakaso" ulihitajika

baada ya kunajisika kwa kugusana na kitu kilichokufa. Mtu pia angeweza kutengwa na maeneo matakatifu katika Israeli kutokana na kutokukamilika kimwili au jeraha, katika hili sababu yake ni kuwa kutokukamilika hakuendani na ukamilifu wa Mungu.

Sheria hizi zote zililenga kuleta mtazamo wa ulimwengu usio wa kawaida.

## Kurekebisha Tatizo la Unajisi

Kuwa "najisi" na kutofaa kusogelea sehemu takatifu lilikuwa ni suala kubwa kwa Waisraeli wa zamani. Wasingeleta dhabihu na matoleo kwenye eneo lililotakiwa kama walikuwa najisi. Suluhisho lilikuwa ni utakaso wa kimila, wakati mwingine ukihusisha sadaka yake yenyewe au kusubiri wakati.

Mantiki ya sadaka ya damu—Kupiga au kunyunyiza damu juu ya mtu au kitu kukifanya kiwe safi na halali kukaa mahali patakatifu—ni kigeni kwetu. Lakini dhabihu ya damu ilikuwa na kusudi la kitheolojia —zilitambulisha wazo la kubadilisha. Kwa kuwa damu ilikuwa nguvu ya uzima (Walawi 17:11), kuuchukua uhai wa mnyama kulifundisha somo kuwa kumkaribia Mungu kwa neno lolote isipokuwa lake ilimaanisha kifo. Damu ya dhabihu ilikuwa mbadala wa rehema ya kuondoa unajisi wa mwisraeli, au hali ya uchafu.

Hoja ya funzo ilikuwa kwamba Mungu alikuwa *anauhifadhi* uhai wa Mwisraeli kwa kuubadilisha na dhabihu. Uhai wa mwanadamu ulikuwa takatifu zaidi kuliko uhai wa mnyama kwa sababu wanadamu waliumbwa kwa sura ya Mungu (Mwanzo 1:26; 9:6). Waisraeli walimiliki kuwepo kwao kwa kusaidiwa na nguvu isiyo ya kawaida iliyokuwa ikiingilia ambayo ilimuwezesha Ibrahimu na Sarah kupata mtoto (Mwanzo 12:1–3). Lakini maisha ya mtu yalikuwa hatarini katika uwepo wa Mungu mtakatifu. Dhabihu iliwakumbusha kuwa Mungu alikuwa na mamlaka juu ya uhai na kifo—na Mungu alitaka kuwaonyesha rehema.

## Mbingu (na Kuzimu) Duniani

Kuelekeza umakini kwenye upekee wa Mungu (mwingine) ulikuwa umeelezea mawazo fulani—sio tu kuhusu Mungu, lakini pia kuhusu mipaka ya Kimungu. Wazo la "ulimwengu tofauti" ulikuwa msingi kwa mtazamo wa ulimwengu wa kimungu kwa Israeli. Kama pale ulipokaa uwepo wa Mungu palikuwa patakatifu, ardhi kwingine kote haikuwa—ilikuwa ama ya kawaida au mbaya na ovu.

Uwepo wa Mungu mwenyewe uliwekwa na kumbukumbu za Edeni. Alama nyingi za maskani na Hekalu zimebuniwa kuwafanya watu waifikirie Edeni, mahali ambapo mbingu na dunia vilikutana. Ngazi ya taa ya dhahabu ilinakishiwa na kupambwa kama mti. (Kutoka 25:31–40), mfano wa mti wa Uzima katika Edeni. Ilisimama kulinda mbele ya pazia lililofunga njia ya patakatifu pa patakatifu, mahali ambapo sanduku la agano liliwekwa, kifuniko kilichobuniwa kafanya kazi kama kiti cha enzi cha Mungu (Kutoka 25:10–22).

Makerubi ndani ya patakatifu pa patakatifu pia ni muunganiko wazi wa Edeni. Makerubi wa Edeni walisimama kulinda mahali pakukaa Mungu katika Edeni (Mwanzo 3:24). Makerubi ndani ya patakatifu pa patakatifu walilinda mfuniko wa kuelekea sanduku la Agano (Kutoka 25:18–20). Baadae, baada ya Sulemani kujenga hekalu, mpangilio wa hema la maskani ulihamishiwa ndani ya hekalu pamoja na makerubi wawili wakubwa waliingizwa juu ya Sanduku kama kiti cha Mungu akilifanya sanduku liwe sehemu ya kuweka miguu (1 Nyakati 28:2).

Hekalu pia lilipambwa kama bustani ya Edeni, likijazwa kwa picha uoto mzuri na wanyama (1 Wafalme 6–7). Maua, minazi, simba, na vinyago vilichongwa katika ubunifu wake. Ilikuwa ni kumbukumbu ya kuonekana ya mahali ambapo Mungu alifikia kwanza alipokuja duniani kuishi na familia yake ya ubinadamu.

Waisraeli walihitaji kukumbushwa upande wa giza wa jiografia ya ulimwengu pia. Ikiwa kambi ya waisraeli, na baadae taifa la Israeli, ilikuwa ardhi takatifu, makao ya Mungu na watu wake, basi nyika nje ya Israeli ilikuwa ardhi isiyo takatifu. Mungu alikuwa, muda mrefu kabla ya Sinai, ameyaacha mataifa mengine na kuyatoa kwa miungu wadogo (Kumbukumbu. 4:19–20; 32:8–9). Siku moja angeyarejesha mataifa, lakini wakatiwa siku za kibiblia, yalikuwa ulimwengu wa giza.

Mila moja ya Waisraeli ilifanya somo hili lieleweke kwa kuweka kumbukumbu zisizosahaulika. Siku ya hukumu (Yom Kippur) zilifanyika kila mwaka na kuonyeshwa katika Walawi 16, zilihusisha somo la kitu cha kuvutia kuwakumbusha watu kuhusu ardhi takatifu na isiyo takatifu.

Mbuzi wawili walihusishwa. Mmoja alitolewa dhabihu na damu yake kunyunyizwa juu ya mahali patakatifu ili kupatakasa na unajisi wa wanadamu kwa mwaka mwingine. Mbuzi wa dhabihu alikuwa "wa BWANA." Mbuzi mwingine hakuuawa—alipelekwa nyikani baada ya kuhani mkuu kwa ishara kuzipeleka dhambi za watu huko. Mbuzi huyo alikuwa "wa Azazeli"

"Azazeli" ni nani au nini? Baadhi ya tafsiri zinatumia neno mbuzi wa sadaka badala ya Azazeli.  Kwenye vitabu vya bahari ya Shamu, Neno la Kiebrania katika hili ni jina halisi—jina la pepo. Wakati wa safari ya jangwani kuelekea nchi ya Ahadi, Waisraeli walikuwa wakitoa dhabihu kwa mapepo. (Walawi 17:7), kwa sababu walihofia majeshi ya mwovu yangetishia kambi yao. Nyika, hata hivyo, ilikuwa nje ya kambi ya Israeli, na kwa hiyo ilikuwa ni mahali pa mamlaka za uovu. Tendo hili lilipaswa liachwe, na mbuzi wa Azazeli akakamilisha hilo. Mbuzi wa Azazeli hakuwa sadaka kwa miungu miovu—mbuzi huyu kamwe hakutolewa dhabihu. Badala yake, kumpeleka katika nyika ilikuwa ishara ya kuitakasa ardhi takatifu (kambi ya Israeli) toka dhambi.

## Kwanini Hili ni Muhimu

Mambo yalibadilika kwenye Agano Jipya, lakini bado yalibakia vilevile. Mungu bado ni *mwingine*. Utakatifu wake unataka tutakaswe ili kuingia uweponi mwake. Kwetu sisi, hili lilikwisha kamilishwa kwa kukiamini kile alichofanya pale msalabani.

Kila kitu alichofanya Yesu kwa niaba yetu kilikuwa na upatanisho wa Kimungu. Alienda nyikani—mahali ambapo tungetegemea kukuta majeshi ya mwovu— na kushinda majaribu ya shetani. Tukio hilo lilifuatiwa na kuanza kwa huduma yake, ambayo ilifikia kumshinda shetani, ambaye "ana nguvu ya mauti" (Ebrania 2:14). Yesu alisulubiwa *nje* ya mji mtakatifu (Ebrania 13:12). Alikuwa mchafu kwa sababu dhambi zetu zilikuwa juu yake, na Yerusalemu ilikuwa ardhi takatifu.

Kufa na kufufuka kwa Yesu kunatutakasa— kunatufanya tufae kwa uwepo wa Mungu. Dhambi zetu "*ziliwekwa mbali*" (Rum. 11:27; tazama pia 1 Yohana 3:5). Ingawa wadhambi tusiosafi, tu watakatifu kama tupo ndani ya Yesu. Ingawa sio wakamilifu, kutokukamilika kwetu hakuonekani kwa sababu ya Yesu. Ni rahisi hivyo, lakini bado ni muhimu.

Huwa tunafikiri Waisraeli kwa namna mbalimbali walikuwa na upendeleo wa Kiroho kuliko ilivyo kwetu. Baada ya yote, walikuwa na uwepo wa Mungu palepale katikati yao. Waliishi kwenye ulimwengu ambao miungu, jiografia ya ulimwengu ilikuwa *halisi*. Huwa tunafikiri tungekuwa wa kiroho zaidi, tunaomwelekea Mungu zaidi, kama tu tungekuwa na kile walichokuwa nacho, kama tu kule kukumbushwa mara kwa mara ingekuwa uhalisia wetu.

**Agano Jipya linasema *tunavyo*.**

Hatuhitaji maskani au hekalu kuashiria sehemu takatifu. Miili yetu *ni* sehemu takatifu. Paulo anaiita miili yetu ya kidunia "hema" (2 Kor. 5:4) kwa sababu tunakaliwa na uwepo

wa kimungu sawa na ule uliojaza patakatifu pa patakatifu katika maskani na hekalu (Rum. 8:9-11). Hatimaye mwili wetu, makao ya kidunia ya roho yetu,utakufa, nafasi yake kuchukuliwa na "nyumba isiyojegwa kwa mikono" (2 Kor. 5:1-3), makao ya mbinguni—Edeni mpya, mbingu ilirejea duniani (Ufunuo 22:1-3).

Kwa kuwa Mungu anawakalia waaminio leo kupitia Roho wake, kila kanisa—kila kusanyiko la waaminio—ni ardhi takatifu. Hii ndiyo sababu Paulo, wakati akiwaambia kwa huzuni Wakorintho kumtoa mkristo asiyetubu aliyekuwa anaishi katika dhambi, aliwaagiza "kumtoa mtu huyu kwa Shetani" (1Kor. 5:5). Kanisa lilikuwa ardhi takatifu. Nje ya ushirika wa waaminio lilikuwa ni eneo la Shetani. Ndipo ambapo dhambi na uharibifu wake unapokaa.

Ni wakati wa kujitazama sisi wenyewe kupitia macho ya Kimungu. Wewe ni mwana wa Mungu, anayefaa kwa mahali patakatifu, sio kwa sababu ya kile unachofanya au usichofanya, bali kwa kuwa uko ndani ya Yesu, uliyekubaliwa na Mungu (Rum. 8:15; Gal. 4:5). Mmetolewa katika ulimwengu wa nguvu za giza "akatuingiza ... katika ufalme wa mwana wa pendo lake" (Kol. 1:13).

Hatupaswi kamwe, sio kwa muda, wowote, kusahau sisi ni nani katika Kristo— na hiyo ina maana gani kwa ulimwengu.

# SURA YA TISA

## Vita Takatifu

Biblia ni kitabu chenye utata. Watu ambao hawakioni kama Neno la Mungu, mara nyingi hupinga kile inachosema. Lakini baadhi ya maeneo ya Biblia huwafanya hata Wakristo wawe na wasiwasi. Vita vya Israeli kushinda nchi ya ahadi ni eneo mojawapo.

Kwa nini? Hasa kwa sababu ya mauaji. Inaonekana kutokuchagua, na kutokueleweka pia. Kwanini ilikuwa muhimu kuua watu wote katika baadhi ya miji— wanaume, wanawake, watoto, na hata wanyama? Kwa nini kutowaacha wenyeji kujisalimisha? Haingekuwa vyema bora kuwahamisha kuliko kuwaua?

Kuna jibu kwa pingamizi zote hizo—lakini nimegundua kuwa jibu linaonekana kuwafanya Wakristo kuwa na wasiwasi kama ilivyo kwa tatizo. Unaweza tu kuelewa sababu na msukumo wa matukio ya ushindi wakati utakapoyatazama kupitia mtazamo wa ulimwengu wa kimungu kwa Israeli.

### Mantiki ya Kimungu ya Israeli

Vita vya nchi ya Ahadi vilisababishwa na mambo mawili, yote kina chake kikiwa katika uelewa wa Israeli wa ulimwengu wao wenyewe kwa kuwa sio tu kukaa katika makazi ya wanadamu bali pia gharama za vita vya kiroho katika ulimwengu usioonekana. Tumeshayazungumzia yote tayari, lakini hebu tupitie.

Sababu moja ni anguko kutoka katika matukio ya Mnara wa Babeli, wakati Mungu alipoamua, baada ya mataifa kumuasi, kwamba hakutaka kuwa na mahusiano ya moja kwa moja na watu wa mataifa hayo. Badala yake, aliwakabidhi wanachama wa baraza lake la kimungu, wana wa Mungu, kuyatawala (Kumbukumbu 4:19–20; 32:8–9). Baadae, alimwita Ibrahimu

na kumuwezesha yeye na mkewe Sarah kuwa na mtoto (Isaka), ambaye watu wa Israeli watatoka kwake.

Tulijifunza katika Zaburi 82 kwamba hawa miungu wadogo walipotoka. Waliruhusu uovu. Watu wakawa wanawaabudu wao badala ya Mungu aliye Juu. Hivyo, wakawa maadui wa Mungu na watu wake, Israeli. Baadhi ya mataifa hayo yalikuwa katika ardhi ya Kanaani, ambayo Mungu alikusudia kuwapa taifa lake Israeli baada ya kutoka, Musa na Waisraeli waliamini kuwa watu waliokuwa wakimiliki ardhi hiyo walikuwa maadui wao wa mauti na miungu yao ingefanya chochote inachoweza kuiharibu Israeli.

Sababu ya pili ilikuwa inatisha zaidi kwa Waisraeli. Inaelezeka vyema zaidi kwa kile kilichotokea wakati Waisraeli walipowasili katika mpaka wa Kanaani, Nchi ya Ahadi.

Musa alituma wapelelezi kumi na wawili katika nchi ya Kanaani walete habari kuhusu nchi na watu wanaoikalia. Wapelelezi walirudi na uthibitisho kuwa nchi ni nzuri—ina wingi wa maziwa na asali—kama vile tu Mungu alivyokuwa amekwisha waambia (Hesabu 13:27). Lakini walidondosha mabomu: "Ile nchi tuliyopita kati yake ili kuipeleleza, ni nchi inayowala watu wanaoikaa; na watu wote tuliowaona ndani yake ni watu warefu mno. Kisha huko tuliwaona Wanefili, wana wa Anaki, waliotoka kwa hao wanefili; tukajiona nafsi zetu kuwa kama mapanzi; nao ndivyo walivyotuona sisi." (Hesabu 13:32–33).

Tumezungumza kuhusu wanefili hapo kabla. Walikuwa ni wazaliwa wa Wana wa Mungu na binti za watu nyuma katika Mwanzo 6:1–4. Waanaki warefu ambao wapelelezi wa Israeli waliwaona walikuwa ni wazaliwa wao, na walikuwepo wengi wao waliotawanyika katika nchi yote ya Kaanani, miongoni mwa matatifa na miji ambayo Waisraeli walipaswa kuwashinda na kuchukua nchi (Hesabu 13:28–29). Kazi ya kuiteka nchi na miungu yake ilikuwa imeonekana ngumu hapo kabla; sasa

kulionekana kuzimu kusikowezekana. Sasa kuichukua nchi walipaswa kuwakabili wapiganaji wenye miili yenye ukubwa usio wa kawaida.

Ni wawili tu kati ya wapelelezi—Joshua na Kalebu—walioamini Mungu angewasaidia Waisraeli kuwashinda Waanaki. Waliosalia waliwaaminisha watu kuwa wangeshindwa. Badala ya kuamini kwamba Mungu— yuleyule, Mungu aliye mwangamiza Farao na na Jeshi lake vizuri kabisa— angeingilia na kuwapa ushindi, walilalama,"Hatuwezi kupanda tupigane na watu hawa; kwa maana wana nguvu kuliko sisi" (Hesabu 13:31).

Mungu akajibu, "Je, Watu hawa watanidharau hata lini? Wasiniamini hata lini? Nijapokuwa nimefanya ishara hizo zote kati yao?" (Hesabu 14:11). Kwa hakika, Mungu alikasirika sana kiasi kwamba alitishia kutowarithisha Israeli—kitu kilekile alichokuwa amekifanya kwa mataifa katika Mnara wa Babeli—na kuanza tena upya, wakati huu na Musa: "Nitawapiga kwa tauni, na kuwaondolea urithi wao, nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, kisha lenye nguvu kuliko wao" (Hesabu 14:12).

Musa alimuomba Mungu aghairi (Hesabu 14:13-19). Mungu alighairi, lakini hakuwaacha wasio na imani kati yao. Somo lilipaswa kujifunzwa.lingekuwa gumu. Alimwambia Musa:

> Mimi nimewasamehe kama neno lako lilivyokuwa; lakini hakika yangu, kama niishivyo, tena kama dunia hii nzima itakavyojawa na utukufua wa BWANA; kwa sababu watu hawa wote, ambao wameuona utukufu wangu na ishara zangu, nilizozitenda huko Misri, na huko jangwani, pamoja na haya wamenijaribu mara hizi kumi, wala hawakuisikiza sauti yangu; hakika yangu, hawataiona nchi niliyowaapia baba zao, wala katika hao wote walionidharau hapana atakayeiona;...

Mizoga yenu itaanguka katika jangwa hili, na wote waliohesabiwa miongoni mwenu, kama jumla ya hesabu yenu, tangu waliopata umri wa miaka ishirini na zaidi, hao walioninung'unikia, hakika yangu hamtaingia ninyi katika nchi, ambayo niliinua mkono wangu ya kwamba nitawaketisha humo, isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune, na Yoshua mwana wa Nuni. Lakini watoto wenu, ambao mlisema watakuwa mateka, ndio nitakaowaleta na kuwatia ndani, nao wataijua nchi ninyi mliyoikataa. (Hesabu 14:20-31)

""Mara kumi" ilikuwa ni tamathali za semi katika siku za biblia iliyomaanisha "mara kwa mara" (Mwanzo 31:7; Job 19:3). Hadi kufikia hapa, alikuwa amevumilia malalamiko ya watu hawa. Badala ya kuogopa kuendelea kuwa watumwa Misri walivikumbuka vyakula walivokuwa wakila (Hesabu 11:1-14; 31-35) na kuhusu kiongozi aliyechaguliwa na Mungu, Musa (Hesabu 12:1-16). Lakini uvumilivu wake ulikuwa umeondoka; wakati huu, kutokuamini kwao kungekuwa na gharama kubwa. Israeli wangetangatanga jangwani kwa miaka arobaini mpaka wale watu wazima wasioamini watakapokuwa wamekufa.

## Nafasi ya Pili

Israeli ingekuwa na nafasi ya pili katika kuichukua nchi ya Ahadi. Matukio ya Kumbukumbu 2-3 kwa vipi, wakati wa miaka yao arobaini ya kutangatanga, Waisraeli walijeruhiwa katika mpaka wa upande wa pili wa mto Yordani (ulioitwa "Transjordan"), mashariki mwa Nchi ya Ahadi. Ardhi ya ukanda wa Yordani ni Edomu, Moabu, na Ammoni, maeneo haya Mungu aliwapa wazaliwa wa Lutu, mpwa wa Ibrahimu, na Esau, nduguye Yakobo. Watu walioishi pale walikuwa ndugu wa Waisraeli ... wengi wao, hata hivyo. Lakini walikuwepo wengine.

Mungu alikuwa amemwelekeza Musa kwenda safari hii kwa kusudi maalumu. Ilikuwa sio kuwatembelea ndugu wa mbali. Waisraeli hatimaye wakashika njia yao kwenda eneo linaloitwa Bashani. Eneo hilo lilikuwa na sifa yenye kutisha. Katika maandiko ya kale nje ya Biblia, Bashani ilikuwa ikijulikana kama "mahali pa nyoka." Miji yake miwili mikubwa ya, Heshboni na Edrei, yote imetajwa kuhusiana na safari hii (Kumb. 1:4; Josh. 13:12), ilidhaniwa kuwa njia ya kwenda kwa ulimwengu wa wafu. Katika mazingira ya mtazamo wa kidunia wa Israeli kimungu, Mungu alikuwa amewapeleka Waisraeli kwenye malango ya kuzimu.

**Na haikuwa hiyo tu**

Mungu alikuwa amewapeleka Waisraeli pale kuwakabili wafalme wawili, Sihoni na Ogu. Wafalme hao wawili walikuwa ni Waamori (Kumb. 3:2–3; 31:4) na watawala wa wale Biblia inaowaita Waemi. Kama Kumbukumbu 2:11 kwa uangalifu inaeleza, Waanaki walikuwa "Wakihesabiwa kama Waemi pia." Mungu, kupitia Musa, aliwaongoza watu kwenda eneo lingine lililokuwa linakaliwa na majitu kama yale yale yaliyokuwa yamewatisha wapelelezi wa Israeli na kupelekea kutokuamini miaka ya awali (Hesabu 13:32–33), tukio ambalo lilisababisha miaka arobaini ya kutangatanga.

Kwanini Mungu aliwapeleka pale? Ni kwa sababu mapambano haya yalikuwa ni utabiri wa kile ambacho kingepaswa kufanyika wakati miaka arobaini itakapokuwa imeisha. Israeli hatimaye wangepaswa kuvuka Yordani ili kuimiliki nchi ambayo Mungu alikuwa amewapa. Mungu alikuwa akiwajaribu watu wake. Je, wangeamini na kupigana wakati huu? Kama ndivyo, ushindi ungewapa ujasiri na imani ya kile kilichokuwa mbeleni.

Waisraeli walikuwa wameshusha mkia miaka ya awali. Lakini wakati huu hadithi iliisha tofauti. Kama Musa alivyosema, "BWANA, Mungu wetu akamtoa [Sihoni] mbele

yetu, tukampiga yeye na wanawe, na watu wake wote.... Basi BWANA, Mungu wetu, akamtia mikononi mwetu na Ogu mfalme wa Bashani, na watu wake wote; tukampiga, asisaziwe chochote" (Kumb. 2:33; 3:3). Nabii Amosi, akielezea mapambano haya kwenye kitabu chake mwenyewe cha Biblia miaka mingi baadae, alionyesha matokeo yake hivi: "[Bwana] Lakini nalimwangamiza Mwamori mbele yao, ambaye urefu wake ulikuwa kama urefu wa mierezi, tena alikuwa na nguvu kama mialoni" (Amos 2:9).

Ilikuwa ni njia mbaya ya kuanza nafasi yao ya pili. Mungu aliamuru kuwa waikabili hofu yao— hofu ambayo ilikuwa imewagharimu miaka arobaini ya kutangatanga bila malengo. Walikuwa na Mungu ambaye alikuwa ameigawanya Bahari ya Shamu akiwa upande wao. Ulikuwa ni wakati walipolikumbuka hilo.

### "Kujitoa kwa Uharibifu"

Israeli walishinda siku hiyo dhidi ya Sihoni na Ogu. Na hapa ndipo tunapopata uelewa wetu wa kwanza wa kwanini ushindi wa Nchi ya Ahadi katika nyakati hizi ulihusisha uharibifu. Watu wote wa miji ambayo ilikuwa inakaliwa na majitu Waemi "walitolewa kwa uharibifu" (Kumb. 3:6). Lengo halikuwa kulipiza kisasi. Lengo lilikuwa kuhakikisha uzao wote wa Wanefili unaondoka. Kwa Waisraeli, ukoo wa uzao wa majitu ulikuwa wa kipepo, uliotokana na uasi, viumbe wa kimungu walioasi. Wasingeweza kukaa pamoja na urithi wa kipepo.

Muda ulipita, na kabla Waisraeli hawajavuka Yordani kuingia Kanaani, Musa alifariki. Uongozi ukawa kwa Yoshua. Aliongoza mapambano mengi ya kijeshi katika Israeli kushinda Nchi ya Ahadi, na harakati hizo ziliongozwa na sababu mbili nilizozielezea hapo awali katika sura hii: yaondoeni mataifa yenye uadui, na katika mchakato, ondoeni uzao wote wa majitu.

Ikitazamwa katika muktadha/mazingira hayo, uvamizi na utekaji wa nchi ya Ahadi ilikuwa ni vita takatifu—vita dhidi ya majeshi ya giza na maadui chini ya utawala wa miungu adui ambayo Biblia inasema ni vyombo halisi vya kiroho.

Mantiki ya kuvamia inaelezwa vyema katika Yoshua 11:21-22:

Wakati huo Yoshua akaenda na kuwakatilia mbali hao Waanaki watoke nchi ya vilima, kutoka Hebroni, na kutoka Debiri, na kutoka Anabu, na kutoka katika nchi yote ya vilima ya Yuda, na kutoka katika nchi yote ya vilima ya Israeli; Yoshua akawaangamiza kabisa na miji yao. Hawakusalia Waanaki hata mmoja nchi ya wana wa Israeli; isipokuwa katika Gaza, na katika Ashidodi walisalia.

## Kwanini hili ni Muhimu

Kampeni za Yoshua zilifanikiwa sana, lakini hazikuwa kamili. Majitu wachache walitoroka—na wakati hilo linaweza lisionekane muhimu sana,kilikuwa kivuli cha matukio yajayo. Baadhi waliingia Gathi. Gathi ikawa mji wa Wafilisti (Yosh. 13:3) na yalikuwa makao ya Goliathi wakati wa mfalme Daudi (1 Sam. 17:4). Goliati hakuwa jitu pekee katika Gathi, ama (1 Nyakati. 20:5-8). Sio wote wale waliokuwa wametolewa kwa uharibifu wakati wa kuiteka Nchi ya Ahadi" waliharibiwa kwa uhakika, na ukweli kwamba uvamizi wa Nchi ya Ahadi haukukamilisha maelekezo yake makuu, ilikuwa na madhara kwa Israeli ".

Kitabu cha waamuzi kinatuambia ushindi ulikuwa haujakamilika katika njia nyingine wakati Yoshua alipofariki. Haikuwa imetambuliwa kikamilifu. Waisraeli waliamua kuwa walikuwa wamefanya vyema vya kutosha na hawakutii agizo la Mungu la kuyaondoa mataifa mengine. Lakini kutii kwa sehemu ni kutotii.

Waisraeli wangetumia karne nyingi wakilipia madhara ya maamuzi yao ya kupuuza malengo ya Mungu. Kitabu cha Waamuzi kinaelezea mzunguko mbaya: Israeli ikizidiwa mara kwa mara na mataifa adui, na kuamini kuwa uaminifu kwa Mungu ulikaribia kuzimika. Mambo yaliimarika wakati Mfalme Daudi na mwanawe, Suleimani, lakini Suleimani alipokuwa ameondoka, Israeli iligawanyika katika vita vya wenyewe kwa wenyewe na ibada za sanamu.

Utukufu wa ushindi ulikuwa umefunikwa na habari za kushindwa. Kushindwa kulikuwa kumechukuliwa toka kwenye maneno/kelele za ushindi Utawala wa Ufalme wa Mungu—mpango wake wa urejesho wa Edeni—viliangukia motoni. Mtazamo wa Kimungu ulioibuka toka Babeli, na mataifa yasiyoamini chini ya utawala wa miungu miovu, ilibakia imara. Israeli walishindwa/pigwa na kutawanyika na Nchi yao ya Ahadi ikawa chini ya himaya ya miungu mingine na watu wao. Mtazamo huo huo wa ulimwengu unajitokeza kwenye Agano Jipya pia. Paulo anatumia maneno kama vile falme, mamlaka, viti vya enzi, na wakuu kuonyesha majeshi ya giza. Kila neno mojawapo lilitumikaa zamani kuonyesha utawala wa Kijiografia.

Sababu ya kushindwa kwa Waisraeli ilikuwa ni kutotii na kutokuwa na Imani kwa upande wa watu wa Mungu. Wanadamu ni dhaifu. Tunaweza kushangaa kwanini Mungu anahangaika na sisi. Lakini tukitazama nyuma katika Edeni, tunajua kwanini. Mungu alijitolea mwenyewe kwa mwanadamu. Sisi ni sura yake,na familia yake ya duniani. Mpango wake wa asili wa kuitawala dunia ulitujumuisha na sisi. Kwa Mungu kuweka kando ushiriki wa mwanadamu katika utawala wa baraza lake duniani ingepeleka ujumbe kuwa hakuwa na uwezo wa kuuwezesha kufanya kazi au lilikuwa ni wazo baya kuanza nalo. Mungu hashindwi kutimiza malengo yake mwenyewe. Na kama ilivyotajwa katika sura iliyotangulia, huwa hafanyi makosa.

Ulikuwa ni wakati wa kutumia mbinu mpya kwa tatizo la zamani la dhambi na kushindwa. Ubinadamu usingeaminika kwa kufufua utawala wa ufalme wa Edeni. Mungu pekee ndiye angeweza kufanya kile kilichotakiwa kufanyika. Mungu pekee ndiye angeweza kufikia majukumu ya maagano yake mwenyewe. Lakini ubinadamu usingewekwa kando. Badala yake, *Mungu alipaswa kuwa mwanadamu*. Mungu angetakiwa kutimiza Sheria na maagano yeye mwenyewe na kisha kuchukua juu yake adhabu ya kushindwa kote kwa mwanadamu. Lakini katika kuunganisha mpango huo usiofikirika ilimaanisha kwamba ulipaswa kufanywa siri kwa kila mmoja, wakiwemo viumbe wa kimungu wenye werevu wa uovu ambao ni maadui wa mpango wake. Hiyo isingekuwa rahisi

## SURA YA KUMI

## Imefichwa katika Uonekano Wazi

Tangu anguko, Mungu amekuwa akijaribu kufufua lengo lake la asili la Edeni: kuishi na wote, familia yake ya kimungu na ya wanadamu duniani. Mungu alikuwa amemwambia Adamu na Hawa kuzaa na kuongezeka, kueneza utawala mzuri wa Mungu katika maeneo yaliyosalia ya sayari. Mungu alitaka dunia yote iwe mahali ambapo mbingu na dunia vinakutana, ambapo ubinadamu ungefurahia uungu, na ambapo uungu ungefurahia dunia na ubinadamu. Tunajua vile hilo lilivyokwenda.

### Historia ya Anguko

Ubinadamu uliasi na kufukuzwa katika uwepo wa Mungu. Edeni ikafungwa. Adui wa kiungu, nyoka, alipigwa marufuku—alitupwa au kukatiliwa mbali—toka Uweponi mwa Mungu hadi duniani, mahali ambapo mauti inatawala, ambapo maisha si ya milele. Akawa bwana wa wafu, na kwa hiyo akawa na madai juu ya kila mwanadamu ambaye angeishi wakati wowote—kwa sababu wanafanya dhambi, na mshahara wa dhambi ni mauti. (Rum. 6:23).

Baada ya gharika, Mungu alikuwa amerejelea mpango wake wa Edeni kwa Nuhu na familia yake: Zaeni, Mkaongezeke. Ilikuwa ni kufanya upya. Badala yake, ubinadamu uliasi. Badala ya kumtii Mungu na kueneza maarifa na utawala wa Mungu kila mahali, wangejenga mnara mahali ambapo Mungu angewafuata.

Anguko tena, Mungu hangeweweza kulifuata. Alichanganya lugha za mataifa na kuyakabidhi mataifa kwa baraza lake la kimungu kuyatawala. Kisha akaamua kuanza upya na familia mpya ya wanadamu—kupitia Ibrahimu na Sara. Angeyarudia mataifa mengine—kupitia wazaliwa wa Ibrahimu—mara utawala wa ufalme utakapofufuliwa (Mwanzo 12:3).

Hili, pia, lilikuwa ni anguko. Hivyo lilikuwa jaribio la pili, kuwatoa Israeli katika Misri, kisha kuwapeleka Sinai, na hatimaye kwenda Nchi ya Ahadi. Israeli walishindwa. Hatimaye Mungu akamuinua Daudi, na kisha Suleimani. Lakini baada ya Suleimani kufa, Israeli walifuata miungu mingine na Waisraeli wakageukiana wao kwa wao. Mungu akalazimika kuwafukuza toka katika Nchi ya Ahadi kwenda uhamishoni.

Hadithi ya mwanadamu, mbali na uwepo wa Mungu, ni hadirhi ya kushindwa. Hii ni kwa sababu ubinadamu ulipotea tangu anguko. Wanadamu wote hawajakamilika na wametengwa na Mungu. Hakuna kiongozi mwanadamu angeweza kuaminiwa kuanzisha na kuendeleza ufalme wa Mungu. Wengeweza kupinga uaminifu kwa Mungu pekee. Wangeiendea njia yao wenyewe. Wanadamu wangetenda dhambi, wangeshindwa, na kuungana na bwana wa mauti, adui mkuu wa Mungu. Lakini maono ya Mungu ya kushiriki Baraka za kuwa wafalme-wawakilishi katika Edeni mpya isingeweza kutokea bila kuwepo kwa wanadamu. Na njia pekee ambayo wanadamu wangeweza kushikilia mpango wa Mungu ilikuwa ni kwao kufanywa upya tena. Laana ya Anguko lazima iondolewe.

Na kwa hiyo, Mungu alikuwa na mpango.

## Suluhisho—na Tatizo

Mungu alihitaji mtu ambaye alikuwa zaidi ya mwanadamu—mtu ambaye angeweza kushinda/kupinga majaribu, ambaye wakati wote angetii, ambaye angefaa kwa ufalme, ambaye angeweza kugeuza laana ya mauti kwa kufa na kufufuka kwa nguvu zake mwenyewe. Hayo yote yangeweza kutokea kwa njia moja tu: Mungu mwenyewe angekuwa mwanadamu. Mungu angelitimiza mpango wake yeye mwenyewe, *kama mwanadamu*, kwa ajili ya wanadamu wote, na kuirejesha Edeni. Wakati tu ambapo wanadamu walisamehewa na

kufanywa watakatifu kama Yesu kupitia nguvu ya ufufuo (1 Yohana 3:1–3) Edeni ingeweza kuwa halisi.

Lakini kulikuwa na tatizo. Kama mpango ungegundulika — kwamba mtu ambaye ni Mungu alikuwepo hapa afe na afufuke tena kuhakikisha kwamba lengo halisi la Mungu linarejeshwa—nguvu za giza zisingeanguka kwa hilo.

Hiki ndicho hasa kile Paulo alichosema katika waraka kwa kanisa la Korintho:

Bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu; ambayo wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja; maana kama wangaliijua, wasingalimsulubisha Bwana wa Utukufu. (1 Kor. 2:7–8 LEB)

Paulo anamzungumzia nani? Neno watawala kuelezea mamlaka za kibinadamu—kama vile Pontio Pilato na viongozi wa Wayahudi—bali pia Paulo anamtazamo wa kiungu, nguvu za kipepo (Efeso. 2:2). Maadui wa Mungu, wanadamu na miungu, walipaswa kuwa katika giza. Kila kitu kilitegemea kufa na kufufuka kwa Mungu-mtu .

Lakini unaitunzaje siri hiyo?

## Masihi wa Utata.

Mungu-mtu ambaye urejesho wa Edeni ulimtegemea alikuwa, kwa hakika, Masihi—Yesu wa Nazareti. Lakini ilikushangaza niliposema mpango wa kimasihi ulikuwa siri? Hatuwezi kusoma Agano la Kale na kuuona mpango wote? Hapana, hatuwezi.

Amini usiamini, hakuna mstari katika Agano la Kale unaotumia neno *masihi* kwa mtu ambaye alikuwa Mungu kweli ambaye angekufa kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Sio hata Isaya 53:11 na picha yake ya "Mtumishi anayetaabika." Neno *masihi* halitokei kamwe katika sura hiyo, na kwingineko kote

katika Isaya, "mtumishi" linamaanisha taifa la Israeli, na sio mwokozi mmoja(binafsi) (Isaya 41:8; 44:1-2, 21; 45:4; 48:20; 49:3). Na neno *masihi*, linalomaanisha "mpakwa mafuta" karibia wakati wote linamwelezea Daudi au mmojawapo wa wazaliwa wake aliyetawala kama mfalme baada yake.

Kwa hakika, uthibitisho wa hiki ninachokisema—kwamba maelezo ya Masihi wa Mungu ambaye angekufa na kufufuka tena ni vigumu kuyapata katika Agano la Kale—ni dhahiri katika Agano Jipya.

Fikiri jinsi ambavyo wanafunzi walimjibu Yesu wakati alipowaambia anakwenda Yerusalemu kufa. Tangazo hilo liliwasumbua na kuwachanganya (Mathayo 17:22-23; Marko 9:30-32). Hawakujibu kwa kusema, "Ah, sawa, tulilisoma hilo katika maandiko" Petro hata alimkemea Yesu kwa kusema hivyo (Mathayo 16:21-23).

Wanafunzi hawakuwa na ufahamu,wala wazo, la mpango huu mpya wa Mungu.walimfikiria Yesu kama mwana wa Daudi tu na mrithi halali wa kiti chake cha ufalme, mtu aliyefanya miujiza kama tu manabii wa agano la kale walivyofanya.

Hata *baada* ya ufufuko, wanafunzi walipaswa kuwa akili zao zimefunguliwa kwa njia ya *kimungu* ili kumuona Masihi anayeteseka. Baada ya Yesu kufufuka kutoka kwa wafu, aliwatokea na kuwaambia:

"Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi" Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko. (Luka 24:44-45)

"Mpango mpya" wa Mungu—kwamba angekufa na kisha kufufuka toka kwa wafu kuondoa laana ya anguko—si dhahiri kabisa katika Agano la Kale. Badala yake, vifungu vimetapakaa

katika Agano la Kale lote katika maeneo mengi. Kamwe hayajaonyesha katika sehemu moja. Ufafanuzi wa Kimasihi uko wazi tu kwa kuzingatia—na hasa kwa mtu yule anayejua anatafuta nini na ategemee nini.

Viumbe waovu werevu wa kimungu, bila shaka, walijua mwana wa Daudi aliyetabiriwa amefika (Mathayo 8:28–29; Luka 4:31–35). Hayo yote waliweza kuyaelewa kutoka katika Agano la Kale. Bali hakuna kitu walichosema mapepo kilichoonyesha kuwa walielewa kuwa Yesu alikuja duniani afe na kufufuka tena, kuondoa laana.

Kama Paulo alivyosema, kama wao na shetani wangelijua hilo, wasingewasukuma watu kama Yuda kumsaliti Yesu kwa wale waliomtaka afe. Shetani na wote waliokuwa upande wake wana mengi lakini sio wajinga. *Walidanganyika* kumuua Yesu, kama tu Mungu alivyokuwa amepanga. Walianzisha mlolongo wa matukio ambayo yangepelekea anguko lao wenyewe. Ulikuwa ni mpango wa Kimungu kuwakosesha mwelekeo.

## Sehemu za Maelezo

Katika marejeo, tunaweza kuona vipande vya maelezo ya kimasihi kwa uwazi zaidi kuliko wanafunzi walivyoweza. Wakati hakuna msitari ambao unaonyesha mwana wa Daudi wa Kimasihi wa Mungu akifa na kufufuka kuondoa laana, mtiririko huo unaonekana katika Agano lote la Kale. Baada ya kuona namna mpango ulivyofanya kazi, unaweza kutafuta mwanzo wa mtiririko na kuanza kufuatilia mpangilio/chati.

Kwa mfano, uliza, "Mwana wa Mungu ni nani?"Jibu sio "Yesu" katika Agano la Kale. Adamu alikuwa mwana wa Mungu—alikuwa mtu wa kwanza. Israeli inaitwa mwana wa Mungu (Kutoka 4:23; Hos. 11:1). Mfalme wa Israeli anaitwa mwana wa Mungu (Zaburi 2:7). Katika Agano Jipya Yesu ni "Adamu wa Pili" na "Mwana wa Mungu" (Rum. 1:4; 1 Kor. 15:45; 2 Kor. 1:19; Ebr. 4:4).

Tunaweza kuuliza, “Mtumishi wa Mungu ni nani?” Adamu alimtumikia Mungu (Mwanzo 2:15). Israeli iliitwa mtumishi wa Mungu (Isa. 41:8; 44:1–2, 21; 45:4; 48:20; 49:3). Daudi na Wafalme wengine wa Israeli katika kizazi chake waliitwa wana wa Mungu (2 Sam. 3:18; Zaburi 89:3; 1 Wafalme 3:7; 2 Nyakati 32:16). Yesu pia alikuwa Mtumishi (Acts 3:13; 4:30; Filipi. 2:1–8).

Je hawa wana wa Mungu na watumishi wa Mungu waliteseka? Je, uwepo wao duniani uliishia katika hatua fulani? Je, uwepo huo ulihuishwa? Je, wana nafasi katika Edeni mpya ijayo? Majibu yote ni ndiyo. Adamu, Israeli, Wafalme katika nafasi ya Daudi wote walifukuzwa katika uwepo wa Mungu—mahali katika dunia alipokaa (Edeni na Nchi ya Ahadi). Bado walikuwa na watakombolewa katika Edeni mpya kuishi na Mungu na Yesu mfufuka.

Wazo hapa ni kuwa wote hawa wanamwelekea Yesu kwa namna fulani, naye *anakamilisha mwelekeo*. Yeye ni umoja/muunganiko wa picha ambayo inaonekana wakati vipande vinapogunduliwa na kuwekwa kwenye nafasi zake zinazotakiwa. Kila kitu kilikuwa katika muonekano wazi, na bado haigunduliki bila kuzingatia.

## Kwanini hili ni Muhimu

Mwovu mwerevu—Shetani, mapepo, miungu wadogo wanao yatawala mataifa—hawajui kila kitu. Hawajui mawazo ya Mungu, wala hawawezi kuyachunguza. Huwa tunafikiri kwa kuwa ni miungu wanajua mambo yote. Sio kweli. Kuna mmoja tu anayejua mambo yote—Mungu. Na anatokea kuwa upande wetu.

Kwa sababu ya anguko, Shetani alikuwa na uhalali wa kisheria juu yetu sote. Namaanisha nini? Kwa sababu ya dhambi ya Adamu, “kifo kikaenea kwa wote” (Rum. 5:12). Nyoka alilaaniwa, akatupwa chini kutawala katika ulimwengu wa wafu—chini ya ardhi, au kile tunachoita kuzimu. Kwa

sababu ya anguko, kila mmoja hatma yake ni kufa na kwenda katika ulimwengu wa wafu—ambapo Ibilisi hutawala.

Hayo yote yalibadilika wakati Yesu alipokuja *mara ya kwanza* na kukamilisha mpango wa Mungu wa wokovu kwa kufa msalabani na kufufuka toka kwa wafu. Hatua ya kwanza ya kuirejesha Edeni ilikuwa ni kutoa njia ya mwanadamu kuiepuka laana ya mauti. Wote waaminio, ambao wamefanywa kuwa sehemu ya familia ya Mungu na Ufalme, hawako tena chini ya laana ya mauti na bwana wa mauti. Na hii ndiyo sababu Yesu, wakati alipokuwa akianza huduma yake ya kufufua ufalme (Luka 10:1–9), alisema: "Nilimwona Shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme" (Luka 10:18). Yesu alijua kufa kwake na kufufuka vingelipa deni la wenye dhambi, na kumwacha Shetani bila madai juu ya roho zetu. Ufalme ulikuwa ni mwanzo wa mwisho wa bwana wa mauti.

Lazima, tena, tukumbuke sisi ni nani—na utambulisho wetu unatoka wapi. Waaminio, kwa pamoja kama kanisa, wanaitwa ***mwili wa Kristo***. Na mwili wa Yesu ulifufuliwa. Tutafufuka kwa sababu amefufuka (1Kor. 15:20–23). Yeye ni *mzaliwa wa kwanza* wa wafu. Sisi ni "mkutano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni" (Ebrania 12:22–24). Kama Yohana alivyosema, "Bali wote waliompokea—ndio wale waliaminio jina lake—aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu" (Yohana 1:12LEB). *Shetani hana madai juu ya wana wa Mungu* kwa sababu watafufuka kutoka kwa wafu. Hakuna sababu ya kumtafuta aliye hai miongoni mwa wafu.

Mungu asingeonyesha mkono wake kwa yeyote—wawe ni wanadamu au miungu, waaminifu au wasiowaaminifu. Vitu maalumu vya jinsi ambavyo masihi angekamilisha kusudi la Mungu ilikuwa lazima viwe siri. Bali Mungu angewajulisha hilo pasipo shaka wakati Masihi alipotokea, angekuwa Mungu katika mwili wa mwanadamu, na urejesho wa Ufalme wa Edeni ulikuwa ni hitimisho. Kama tutakavyoona katika sura mbili zinazofuata, hayo yalikuwa ni maelezo ya kutosha kuwajengea

watu imani katika mioyo yao kwa haraka na kuzipumbaza nguvu za giza ili zitekeleze uharibifu wao wenyewe.

# SURA YA KUMI NA MOJA

## Dhamira ya Kimungu

Katika sura iliyopita, tuliona jinsi Agano la Kale linavyomuelezea Masihi kwa kumficha katika muonekano wazi. Ufunguo wa mpango wa Mungu kuirejesha Edeni na kuukomboa ubinadamu ilikuwa ni kwa Masihi, Yesu, kufa msalabani na kufufuka kutoka kwa wafu.

Ni kwa kuwa mwanadamu pekee, Mungu angeweza kuhakikisha kwamba mfalme mwanadamu kutoka katika msitari wa Daudi angewatawala watu wake bila kuanguka katika dhambi na kupotoka kiroho. Kama tu mfalme huyo angekufa katika nafasi ya watu wake na kufufuka kutoka kwa wafu Mungu angeweza kuihukumu dhambi kwa haki *na* kutoa wokovu vyote kwa wakati mmoja. Ni kwa kufa na kufufuka kwa Masihi pekee, ndio watu walioanguka bado wana nafasi katika familia ya baraza la Mungu, kutawala katika ufalme wa Edeni uliofufuliwa, kama ilivyopangwa hapo awali.

Lakini fikiri kuhusu yote yaliyohitajika: Yesu alipaswa kwa kiasi fulani kuhakikisha kuwa nguvu za miungu ya giza zinawafanya watu wamwue—bila kuelewa ni nini haswa walichokuwa wanafanya. Kama Paulo alivyosema kwa Wakorintho (1Kor. 2:6–8), kama wangejua matokeo yake yangekuwa ni yapi, kamwe wasinge msulubisha Bwana.

Maisha na huduma ya Yesu vinaweza kuwa na maana wakati vinapotazamwa kwa asili. Ni rahisi kwa wasomaji wa Agano Jipya, kwa mfano, kupata picha kuwa huduma ya Yesu kuelekea mpaka kwenye msalaba kwa kiasi fulani haikuwa na mpangilio. Baada ya yote, Injili haiwasilishi wakati wote sehemu hiyo hiyo—kwa mfano, kuzaliwa kwa Yesu kunapatikana katika injili mbili pekee (Mathayo na Luka), na ni moja pekee inayowataja mamajusi (Mathayo. 2). Wakati mwingine matukio huonekana katika mpangilio tofauti kidogo

katika injili tofauti. Lakini matendo hayo ya Yesu aliyowekwa kumbukumbu katika injili yanayopelekea mpaka kusulubiwa—kuwaponya wagonjwa, kuhubiri kuhusu ufalme wa Mungu, kusamehe dhambi, kukabiliana na unafiki—yalikuwa zaidi ya matendo yasiyo na mpangilio ya msafiri mwenye hekima ambaye mara kadhaa alifanya mambo ya miujiza; kuna mengi yanayoendelea katika habari za injili kuliko yale yanaoonekana. Kuna sehemu muhimu ya kile Yesu alichokuwa anakifanya.

## Kuushinda Uovu

Tukio ambalo lilionyesha mwanzo wa huduma ya wazi ya Yesu ni ubatizo wake. Ni hapo ambapo Mungu alimtambulisha Yesu hadharani kuwa ni mwanawe (Marko 1:11), na pale ndipo Yohana Mbatizaji alimtambulisha kuwa ndiye "aichukuaye dhambi ya ulimwengu" (Yohana 1:29). Tunaposoma maneno hayo kutoka kwa Yohana, kwa haraka tunafikiri kuhusu kusulubishwa. Bali wanafunzi wa Yohana hawakuwa wakifikiri kuhusu hilo. Kwa kweli, hakuna aliyekuwa anafikiri hivyo. Wakati, karibia mwisho wa huduma yake—zaidi ya miaka mitatu kutoka ubatizo wake—Yesu alianza kuzungumzia kifo chake, wanafunzi wake mwenyewe walilikataa wazo hilo (Mathayo 17:22–23; Marko 9:30–32). Kitu cha mwisho ambacho wangetarajia kusikia kutoka kwa Bwana wao ilikuwa ni kwamba angekufa muda sio mrefu. Hayo yalikuwa ni maneno ya ukichaa. Hawakuelewa kuwa kifo cha Yesu msalabani ulikuwa ni mpango kutoka mwanzo. Kwanini hawakuelewa? Kwa sababu kama tulivyojadili katika sura iliyotangulia, mpango mpango haukuwasilishwa katika Agano la Kale wazi wazi.

Baada ya ubatizo wa Yesu, alipelekwa nyikani na Roho ili akabiliane na shetani (Mathayo. 4:1; Marko 1:12; Luka 4:1–13). Kwamba Ibilisi alikuja kumjaribu Yesu inatuambia sisi kuwa Shetani alijua Yesu ni nani—alikuwa ni masihi katika mpango wa kurejesha "nyumbani utawala" wa Mungu duniani.

After all Baada ya yote, “mpakwa mafuta” (masihi) angekuwa mfalme katika kiti cha Daudi. Shetani, “mtawala wa dunia hii” (Yohana 12:31), alifahamu kuwa Yesu angechukua nafasi katika himaya ya shetani—mataifa ambayo Mungu aliyatupilia mbali katika mnara wa Babeli kabla ya kulianzisha taifa la Israeli (Kumb. 4:19–20; 32:8–9).

Wengi wetu tunakumbuka mazingira kati ya Yesu na Shetani. Shetani alimjaribu Yesu mara tatu (Mathayo 4:3–11). Mkakati wa tatu wa Shetani wa kumfanya Yesu aharibu uhusiano wake na Mungu ulikuwa ni kumpa Mwana wa Mungu mataifa ya ulimwengu (Mathayo 4:8–9), kitu alichokidhania sana ndicho Yesu alikuja kukikomboa:

> Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia, “Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia” (Mathayo 4:8–9)

Pendekezo la shetani lilikuwa ni werevu wa kubadili mpango wa Mungu. Ungeleta matokeo aliyoyataka Mungu—urejesho wa mataifa ambayo Mungu aliyaondolea urithi wa kuwa watu wake. Mpango ukakamilika. Alichotaka Shetani ni Yesu amwabudu yeye badala ya Mungu.

Ahadi ya shetani inadhihrisha kwamba alikuwa hajafahamu kuwa mpango wa Mungu *ulihitaji* kufa kwa Yesu. Aidha, Yesu hakumjulisha. Hakuelezea kukataa kwake. Alimwambia tu Shetani nenda zako. Mungu angerejesha kilicho chake kwa wakati na namna atakavyo. Mpango wa Yesu haukuwa tu unahusu kuyatawala mataifa yote. Ulikuwa unahusu kuijenga tena familia. Kujumuisha kwenye hiyo familia watu kutoka katika mataifa yote, sio Israeli pekee, ilimaanisha kwamba dhambi lazima itubiwe. Kama alivyopanga awali, utawala wa Mungu ungewahusisha watoto wake. Msalaba ulikuwa muhimu katika kuukomboa ubinadamu na kuuweka mpango wa

Mungu katika nafasi. Yesu asingelaghaiwa— bali Ibilisi angefanya hivyo, katika wakati uliopangwa.

### Ladha ya Edeni

Mara tu baada ya kujaribiwa nyikani, Yesu alifanya mambo mawili: aliita wanafunzi wake wa mwanzo (Petro, Andrea, Yakobo, na Yohana) na alimponya mtu aliyepagawa na mapepo (Marko 1:16–28; Luka 4:31–5:11). Vyote, kuita wanafunzi na uponyaji viliendelea,kutengeneza mwanzo wa mfano. Kadri alivyoita wanafunzi, aliwapa uwezo wa kutoa mapepo na kuwaponya watu magonjwa ya kila namna, walemavu, na hali zote (Luka 9:1–5).

Mwanzoni Yesu aliita wanafunzi kumi na wawili. Idadi hiyo haikuwa bahati mbaya. Inaendana na kabila kumi na mbili za Israeli. Yesu alianza mpango wa Ufalme akiwa na Israeli katika mtazamo. Hata hivyo, wao ni, sehemu Mungu, wamechaguliwa juu ya mataifa mengine. (Kumb. 32:8–9).

Baadae Paulo anatazama kuieneza injili kwa namna hiyohiyo—kuanzia kwa Wayahudi, kisha kwa Mataifa (Rum. 1:16–17)

Yesu hakuishia kwa wale kumi na wawili. Katika Luka 10 aliweka watu sabini zaidi kuponya na kutoa pepo (Luke 10:1, 9, 17). Idadi hiyo haikuwa ajali au bahati mbaya. Ni idadi ya mataifa yaliyoorodheshwa katika Mwanzo 10—mataifa ambayo Mungu aliyatupilia mbali katika tukio la Mnara wa Babeli na kuyaweka chini ya himaya ya miungu wadogo (Kumb. 4:19–20; 32:8–9). Baadhi ya tafsiri zina *sabini na mbili*, badala ya sabini, katika mistari hii. Hii ni kwa sababu baadhi ya maandiko ya kale ya Agano la Kale yanaonyesha majina ya mataifa hayo katika Mwanzo 10 kwa namna ambayo yameongezwa hadi sabini na mbili. kwa namna yoyote, hoja ni hiyo hiyo—kuwatuma watu kwa idadi ya mataifa Mwanzo 10. Kama tu ulivyokuwa wito wa wale kumi na wawili uliashiria kuwa ufalme

ulikuwa umekuja kwa Israeli, hivyo kutumwa wale sabini kuliashiria kuwa ufalme ungerejeshwa kwa mataifa.

Wakati wale sabini wanaporejea (Luka 10:17) Yesu anawaambia: “Nilimwona shetani akianguka kutoka mbinguni kama umeme” (Luka 10:18). Ujumbe ni mkubwa: Urejesho mkubwa ulikuwa unaendelea. Shetani asingelikuwa na madai kwa wanadamu mara wanapokuwa ndani ya Yesu. Nafasi yake kumfikia Mungu “kuwashitaki waaminio” (Rev.12:10GNT) ilikuwa imekwisha. Alikuwa ni mwendesha mashitaka asiyekuwa na kesi.

## Njoo na Unipate

Baada ya miaka mitatu ya kuhubiri kuhusu ufalme ujao wa Mungu, kuwaonyesha watu Upendo wa Mungu, na kudhihirisha maisha katika ulimwengu wa Edeni yangeonekanaje, Yesu alianza kuuandaa mwisho—kwa kusudi hili halisi.

Kabla tu ya ile ambayo ingekuwa safari yake ya mwisho kwenda Yerusalemu, Yesu aliwachukua wanafunzi kwenda mbali kaskazini mwa Israeli. Alihitaji kufanya asulubiwe. Asingekuwa amechukua nafasi bora kutupa mpango wa Miungu.

Yesu aliwachukua wanafunzi wake mpaka sehemu iitwayo Kaisari a filipi. Bali hilo lilikuwa ni jina lake la Kirumi. Katika nyakati za Agano la Kale eneo hilo liliitwa Bashani. Tumeshalizungumza hili hapo kabla katika sura ya 9. Bashani ilidhaniwa kuwa ni lango la kwendea kwenye ulimwengu wa wafu—malango ya kuzimu. Kaisaria filipi iko chini ya mlima Hermoni, mahali ambapo, katika mtazamo wa Kiyahudi, wana wa Mungu walifikia duniani katika uasi ulioelezwa katika Mwanzo 6:1–4. Kwa kifupi, katika nyakati za Agano la Kale Bashani na Hermoni zilikuwa zimezungukwa na nguvu za giza.

Ni mahali hapa ambapo Yesu aliuliza swali lake linalofahamika vyema, “Ninyi mwaninena mimi kuwa ni nani?” (Mathayo 16:15). Petro akajibu, “Wewe ndiwe Kristo mwana wa Mungu aliye hai” (ms. 16). Yesu akajibu, akamwambia:

> Heri wewe Simoni Bar-Yona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakwambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, wala milango ya kuzimu haitalishinda. (ms. 17–18)

Utambulisho wa “mwamba” aliozungumzia Yesu umejadiliwa kwa karne nyingi. Ufunguo wa kuelewa neno hilo ni jiografia ya eneo hilo. Kaisaria Filipi imekaa mbali kaskazini mwa eneo la Bashani. Katika nyakati za Agano la Kale,eneo hili lilifikiriwa kuwa na milango ya kuelekea katika ulimwengu wa wafu. Kaisaria Filipi iko chini ya mlima. “Mwamba” ni mlima huo. “Milango ya kuzimu” ilikuwa mahali pale pale ambapo Yesu na wanafunzi wake walikuwa wamesimama.

Yesu alikuwa anazipinga nguvu za giza. Katika anguko, ubinadamu ulipoteza maisha ya milele na Mungu na badala yake ulipata hatma ya mauti na kutenganishwa na Mungu milele. Bwana wa mauti—nyoka, anayejulikana kama Shetani na Ibilisi—alikuwa na madai juu ya ubinadamu. Kila mwanadamu angeungana naye katika ulimwengu wa mauti. Bali Mungu alikuwa na mawazo mengine. Mpango wa siri wa kumpeleka Yesu akalipie adhabu ya dhambi ya ubinadamu ingekuwa ni shambulio la mwanzo kwa milango ya kuzimu. Bwana wa mauti na majeshi yake wasingeweza kustahimili kukabiliana na Ufalme wa Mungu. Kiini,katika kifungu hicho cha Mathayo 16, Yesu anaenda kwenye mlango wa mbele wa Ibilisi na kupinga madai yake. Yesu alitaka kumuudhi Shetani. Kwa nini? Kwa sababu ulikuwa ni wakati wa Yesu kufa ili kufanikisha mpango wa siri wa Mungu.

Kama vile kupinga kwa maneno hukukutosha, Yesu aliendа hatua moja zaidi mbele. Mathayo, Marko, na Luka wote wanakubaliana kuwa tukio lililofuata katika huduma ya Yesu lilikuwa ni kubadilika sura. Marko 9:2–8 inasomeka:

> Hata baada ya siku sita Yesu akawatwa Petro, na Yakobo, na Yohana, akawaleta juu ya milima mirefu faraghani, peke yao, akageuka sura yake mbele yao, mavazi yake yakimeremeta, meupe mno, jinsi asivyoweza dobi duniani kuyafanya meupe. Wakatokewa na Eliya pamoja na Musa, nao walikuwa wakizungumza na Yesu. Petro akajibu, akamwambia Yesu, "Rabi, ni vizuri kuwako hapa. Na tufanye vibanda vitatu, kimoja chako wewe, kimoja na Musa, na kimoja cha Eliya. Maana hakujua la kunena, kwa kuwa waliingiwa na hofu nyingi. Kisha likatokea wingu, likawatia uvuli, sauti ikatoka katika lile wingu, huyu ni mwanangu, mpendwa wangu, msikilizeni yeye." Mara hiyo walipotazama huku huku hawakuona mtu pamoja nao ila Yesu peke yake. (GNT)

Kubadilika sura kunafanyika katika Mlima Hermoni. Yesu alichagua eneo hili kudhihirisha kwa Petro, Yakobo, na Yohana kuwa yeye ni nani haswa—alivyofanyika utukufu wa Mungu. Alikuwa anawatangazia Shetani na nguvu za giza : *Nimekuja ulimwenguni kuchukua kilichokuwa changu. Ufalme wa Mungu uko mkononi mwangu.* Maana yake: "Niko hapa—*sasa fanya kitu kwa ajili yake.*"

Haikuwa ajali au bahati mbaya mara baada ya kubadilika sura Yesu kugeuka kuelekea Yerusalemu na kuanza kuwaambia wanafunzi wake kuwa alikuwa anaenda kufa. Hawakutaka kulisikia. Bali Yesu alikuwa ameshamtega Shetani pamoja na nguvu nyingine za uovu kufanya tendo hilo. Hiyo ingekuwa ni hisia ya haraka ya kuachana naye. Na hicho ndicho Yesu alichotaka. Kifo chake kilikuwa ni ufunguo wa kila kitu.

## Kwa nini Hili ni Muhimu

Huduma ya Yesu ilikusudiwa. Alikuwa na mtazamo ulio wazi wa wajibu wake katika kufufua Ufalme wa Mungu duniani hivyo ungeendelea hadi siku atakayorejea, siku ambayo angetuelekeza katika Ulimwengu ambao ni Edeni.

Maisha yetu sio kielelezo kama yake, bali kila mmoja wetu kama mwanafunzi, anawajibu wa kweli wa kutimiza. Tunahitaji kuishi kama tunaoliamini hilo. Waaminio walioletwa kwenye baraza la familia ya Mungu, hawakuletwa kuwa watazamaji bali watendaji (Kol. 1:13).

Miongoni mwa malengo ya Yesu ilikuwa ni kuwaonyesha watu Edeni ilikuwaje, na maisha pamoja na Mungu yangekuwaje. Katika familia ya Mungu na utawala wa Mungu, kusingekuwa na magonjwa na kasoro kimwili. Pia kusingekuwa na mamlaka za adui. Ufalme wa mwisho wa Mungu ni mkubwa kuliko bustani, mpana kuliko Israeli. Ufalme utakuwa wa ulimwengu wote. Utajumuisha mataifa yote. Na utakuwa kila kitu kama ilivyokuwa Edeni—mbinguni duniani.

Jukumu letu ni kumuiga Yesu. Tunaweza, kama yeye, kujali vyote miili na nafsi za wenzetu ambao ni sura ya Mungu, kuwaelekeza kwenye imani kwa Mfalme na kuwaimarisha kutatua matatizo yao wawe waaminifu kwake. Sio lazima kila wakati itumike nguvu ya Kimungu "kuuganga moyo uliovunjika" na "kuwatangazia mateka uhuru wao" katika hatua za masihi (Isa. 61:1), bali haya ni matendo ya Kimungu katika kimsingi. Yanahitaji kupingana na giza na mikakati ya maono. Hakuna tendo jema ambalo litashindwa kutumiwa na Roho kuuelekeza moyo wa mtu. Hakuna tamko la Injili ambalo litakosa matunda. Wema wa Yesu ulilingana na ujumbe wake. Wala haukupunguza mwingine. Huu ni mfano ambao kila aaminie anaweza kuiga—na ni maelekezo ya kazi kwa maono ya ufalme.

Mwisho, tunakumbushwa tena kuwa uovu mwerevu sio tu kwamba una vikwazo, bali ni hatari kwa maono na matendo ya ufalme. Yesu tayari ameketi mkono ya kuume wa Mungu, na malaika, na enzi, na nguvu zikiisha kutiishwa chini yake" (1 Pet. 3:22). Tumekuwa "tayari lakini bado" watawala pamoja naye (Kol. 3:1; 2 Tim. 2:12; Ufunuo. 2:26; 3:21). Malango ya kuzimu hayataweza kustahimili maendeleo na ukamilisho wa Kanisa kama ufalme wa Mungu duniani. Uamuzi wa kushiriki katika mabadiliko haya makubwa ni wetu.

# SURA YA KUMI NA MBILI

## Ajaye na Mawingu

Nilifunga sura iliyopita kwa kugusia namna Yesu alivyoanza kuzungumzia kifo chake mara baada ya kuzifumba nguvu za giza katika malango ya kuzimu na Mlima Hermoni. Upinzani huo ulianzisha mtiririko wa matukio ambayo yangepelekea kujaribiwa kwa Bwana na kifo chake msalabani. Wakristo wamesoma kuhusu kujaribiwa kwa Yesu mara nyingi. Lakini kuna jambo la Kimungu ambalo mara nyingi linakosewa.

Kuelewa kile ambacho hatimaye kilipelekea hukumu ya kifo kutoka kwa mamlaka za Kiyahudi na kumhamishia Yesu kwa Pontio Pilato ili aitekeleze, tunapaswa turudi kwenye Agano la Kale kitabu cha Danieli—kwenye mkutano ambao Mungu alifanya na jeshi la mbinguni, baraza lake la kimungu.

### Mzee wa siku na Baraza lake.

Danieli 7 inaanza na maono ya ajabu. Danieli anaona wanyama wanne wakubwa wakitoka baharini (Dan. 7:1–8). Wote ni wa ajabu na wakutisha bali yule wa nne ni zaidi. Kwenye ndoto iliyotafsiriwa katika Agano la Kale, vitu na viumbe hai vyote wakati wote vinawakilisha kitu fulani, na kwenye ndoto hii, wanyama wanne katika maono ya Danieli ni tawala au falme nne. Tunalijua hilo kwa sababu maono yake yanaendana na ujumbe wa maono ya Nebukadreza katika Danieli 2, ambayo yalikuwa yanahusu Babeli na Falme nyingine tatu ambazo zingefuata. Lengo letu, hata hivyo, lipo kwenye kile Danieli anachokionyesha mbele:

> Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao. Mto kama wa moto ukatoka ukapita

> mbele zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake; hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa. (Dan. 7:9–10)

Tunajua Mzee wa Siku ni Mungu wa Israeli. Hiyo ni rahisi sana kuona au kutambua, hasa tukilinganisha muonekano wa kiti chake cha enzi na maono ya Ezekiel ya kiti cha enzi cha Mungu katika (Ezek. 1). Moto, magurudumu, na sura ya mwanadamu kwenye kiti cha enzi katika hayo maono ni sawa na ya Danieli.

Lakini, Je, umegundua kuwa sio kwamba kuna kiti cha enzi kimoja tu? Kuna viti vya enzi kadhaa kwenye maono ya Danieli (Dan. 7:9) — vya kutosha mahakama ya kimungu, baraza la Mungu (Dan. 7:10).

Baraza la mbinguni linakutana kuamua hatma ya wale wanyama—falme— katika maono. Inaamuliwa kuwa mnyama wanne lazima auwawe na wale wengine wakanyang'anywa mamlaka yao (Dan. 7:11–12). Wataondolewa na Mfalme mwingine na Ufalme mwingine. Na hapo ndipo mambo yanapokuwa ya kuvutia zaidi.

## Mwana wa Mtu Ajaye Mawinguni

Danieli anaendelea kusimulia maono yake:

> Nikaona katika njozi za usiku,na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbinguni akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa. (Dan. 7:13–14)

"Mwana wa Mtu" ni kifungu ambacho kimetumika mara nyingi katika Agano la Kale. Haishangazi kuwa kinazungumza

kuhusu mwanadamu. Mshangao ni jinsi huyu mtu anavyoelezewa tena kwenye kifungu hiki. Danieli 7:13 kinamwelezea mtu *ajaye mawinguni* kwa Mzee wa Siku.

Kwa nini hilo ni jambo kubwa? Kwa sababu kila mahali pengine maelezo hayo yalipotokea katika Agano la Kale, yalitumiwa *tu* kwa Mungu mwenyewe (Isa. 19:1; Kumb. 33:26; Zab. 68:32-33; Zab. 104:1-4). Bali katika Danieli 7, *Mungu tayari alikuwepo mahali pale* kama Mzee wa Siku. Ni kama vile, katika maono yake, Danieli anamuona "Mungu wa Pili" ambaye pia ni mwanadamu—kitu fulani kama namna Wakristo wanavyoamini kwa Mungu kuwa ni zaidi ya Nafsi moja.

Kwa uhakika hilo ndilo wazo lenyewe.

Wakati Yesu aliposimama mbele ya Kayafa katika majaribu kwenye Mathayo 26, maisha yake yakitegemea usawa, alipata ujasiri kwa kupendelea wazo hili:

> Basi wakuu wa makuhani na baraza yote wakatafuta ushuhuda wa uongo juu ya Yesu, wapate kumwua, wasiuone wangawa walitokea mashahidi wa uongo wengi. Hata baadaye wawili wakatokea, wakasema, huyu alisema, naweza kulivunja hekalu la Mungu, na kulijenga kwa siku tatu. Kisha Kuhani Mkuu akasimama akamwambia, hujibu neno? Hawa wanakushuhudia nini? Lakini, Yesu akanyamaza. Kuhani Mkuu akamwambia, Nakuapisha kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu. Yesu akamwambia, wewe umesema; lakini nawaambieni, tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu akija juu ya mawingu ya mbinguni. Ndipo Kuhani Mkuu akararua mavazi yake, akasema, Amekufuru; tuna haja gani tena ya mashahidi? Tazameni, sasa mmesikia hiyo kufuru yake; mwaonaje ninyi? Wakajibu, wakasema, imempasa kuuwawa. (Mathayo 26:59-66).

Katika kile kinachoonekana kama jibu lisilo na maana kwa swali ambalo liko wazi, Yesu alinukuu Danieli 7:13 katika kumjibu Kayafa. *Je, unataka kujua kwa hakika kuwa mimi ni nani, Kayafa? Sikiliza kwa makini.* Majibu ni ya haraka. Kayafa alitambua mara moja kuwa Yesu alikuwa anadai kuwa yeye ni mfano wa pili wa Mungu katika Danieli 7:13—mtu ambaye ameelezewa kwa namna ambayo ni Mungu pekee ameelezewa hivyo katika Agano la Kale. Alikuwa anadai yeye ni Mungu katika Umbo la mwanadamu. Hiyo ilikuwa ni kufuru—na sababu ya hukumu ya kifo.

Bali Yesu, kwa hakika, alililifahamu hilo. Hakuwa na sababu ya kujilinda. Alifahamu *lazima* afe ili kurejesha ufalme wa Mungu, kuwaleta waaminio katika familia ya Mungu, na kuyarejesha mataifa kutoka katika mamlaka za uovu na nguvu zilizo yatawala mataifa Mungu aliyo yakataa pale Babeli.

Na kufa alikufa. Zaburi 22, inajulikana vyema kwa jinsi inavyoelezea madhara ya kimwili ya kusulubiwa kupitia maneno ya Daudi, yanatupa mtazamo wa hofu isiyoonekana pale msalabani. Mwimba zaburi kwa mateso na huzuni anasema:

Wote wanaoniona hunicheka sana;
hunifyonza, wakitikisa vichwa vyao.
Husema "Umemtegemea bwana".
Na amponye, na amuokoe sasa
Maana amependezwa naye,
mbona hakukusaidia? ...

Maadui wengi wamenizunguka kama mafahali;
walio hodari wa Bashani wamenisonga
Wamefumbua, vinywa vyao kama Simba apapuraye
Na kunguruma.

Nguvu zangu zimeyeyuka
nimemwagika kama maji ardhini.
Mifupa yangu yote imetenguka. (Zaburi. 22:7–14 GNT)

Sehemu ya kuogofya ya maelezo haya ni mafahali wakali *kutoka Bashani.* Kama tulivyoona hapo awali, katika nyakati za Agano la kale, Bashani ilikuwa ni ardhi au sehemu iliyozingirwa na miungu ya kipepo na ulimwengu wa wafu. Eneo hilo lilikuwa linaongoza na ndilo lilikuwa kitovu kwa kumwabudu Baali, anayewakilishwa na mafahali na ng'ombe. "Mafahali kutoka nchi ya Bashani" ni rejea ya kuonyesha mapepo, nguvu za giza. Katika wakati wetu, Taswira au picha ilijumuishwa yote katika hofu ya kukataliwa na C. S. Lewis katika Simba (*The Lion), Mchawi (the Witch), na Kabati (and the Wardrobe).* Hakuna mtu ambaye amesoma kitabu hicho au kuona filamu hiyo ambaye anaweza kumsahau Aslan kwa unyenyekevu akisalimisha maisha yake kwa kundi pendwa la Mchawi Mweupe kwenye Meza ya Jiwe.

Na kama vile Yesu alivyomfumba Shetani kabisa, Aslan alikuwa amemchezea Mchawi Mweupe kuwa mjinga. Kile ambacho mwovu alielewa kinyume kuwa ni wakati wa ushindi kiligeuka kuwa kushindwa kwake mwenyewe.

## Ninyi ni Miungu, bali Mtakufa kama Wanadamu

Shetani kupoteza uhalali wa madai yake juu ya maisha ya wana wa Adamu sio kitu pekee alichopoteza pale msalabani. Washirika wake katika uasi, miungu (*elohim*) ya mataifa, wangeona himaya zao zikianza kutoweka.

Miungu isiyo ya kawaida ilikabidhiwa mataifa hayo na Mungu Aliye Juu wa Israeli (Kumb. 4:19–20; 32:8–9). Hatuambiwi ni lini walikuwa maadui wa Mungu, lakini walikuwa. Walikuwa wamewageuza watu wa Mungu mwenyewe, Israeli, mbali wasimwabudu yeye na badala yake wawatolee wao sadaka (Kumb. 17:1–3; 29:26–27; 32:17). Zaburi 82, zaburi tuliyoitazama katika sura ya 2 inayotambulisha baraza la kimungu, inatuambia hawa *elohim* walitumia vibaya madaraka yao na kuwakubali waovu. Hawakuijali sheria ya Mungu au haki:

Mungu asimama katika kusanyiko la Mungu;

Katikati ya miungu anahukumu (elohim):

“Hata lini mtahukumu kwa dhuluma;

Na kuzikubali nyuso za wabaya?!

Mfanyieni hukumu masikini na yatima,

Mtendeeni haki aliyeonewa na fukara.

Mwokoeni masikini na mhitaji, mwopoeni mikononi mwa wadhalimu.

“Hawajui wala hawafahamu, hutembea gizani,

Misingi yote ya nchi imetikisika”.

(Zaburi 82:1–5 GNT)

Sehemu iliyosalia ya zaburi hii inatuambia kuwa Mungu aliitisha mkutano huu wa baraza la mbinguni kuiambia miungu kuwa nafasi yao katika wakati ujao iko hatarini. Utawala wa kigaidi ungekoma wakati Mungu atakapoamua kuyarejesha mataifa:

“Mimi nimesema, ndinyi miungu;

‘na wana wa Aliye Juu, nyote pia.’

Lakini mtakufa kama wanadamu;

mtaanguka kama mmoja wa wakuu.”

Ee Mungu, usimame, uihukumu nchi;

maana wewe utawarithi mataifa yote.” (Zaburi 82:6–8 GNT)

Je ni wakati gani Mungu angeyarejesha mataifa? Tulisoma jibu mapema katika Danieli 7:14 (GNT):

Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na mataifa yote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, haitapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa.

Ujumbe wa Danieli 7:13–14 uko wazi—wakati Mwana wa Adamu akipokea ufalme, utakuwa mwanzo wa mwisho wa nguvu za miungu ya giza. Yesu aliupokea ufalme katika ufufuko wake. Mungu "alimfufua Yesu kutoka mautini na kumweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho. Yesu anatawala hapo juu sana kuliko ufalme wote,na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; (Efeso 1:20–21 GNT).

## Kwa nini Hili ni Muhimu

Kabla ya msalaba, Shetani alikuwa na madai ya milele juu ya nafsi zetu. Watu wote walikufa—na hivyo, kwenda kwenye ulimwengu wa wafu, *himaya yake*. Na tungesalia hapo—isingelikuwa ni Yesu kujitoa sadaka na kufufuka kwake. Kwa njia ya imani kwa kazi yake msalabani, tumefufuliwa pamoja naye. Kama tulivyoona katika sura iliyopita, Shetani alifukuzwa kutoka katika Uwepo wa Mungu wakati ufalme ulipoanza duniani (Luka 10:18). Mungu asingekuwa na mashitaka yake zaidi dhidi ya waaminio. Hakuwa na haki tena juu ya nafsi zetu.

### Kwa nini, bado, tunaishi kama vile anayo?

Wokovu haupatikani kwa ukamilifu wa nafsi ya mtu. Ni kipawa kinachokuja kwa neema, kwa njia ya imani (Efeso 2:8–9). Hiyo kwa upande mwingine ina maanisha kuwa wokovu hauwezi *kupotezwa* kwa kutokuwa na ukamilifu wa nafsi. Kile ambacho hakikupatikana kwa jitihada hakiwezi kupotezwa kwa kuwa na jitihada kidogo. Wokovu unahusu kuamini *uaminifu*—kutumaini kile alichokifanya Yesu kuyashinda madai ya

Shetani na kugeuka kutoka kwa miungu mingine yote na mifumo ya imani ambayo ni sehemu yake.

Huo ni ujumbe wa ufalme wa Mungu tuliotumwa kuyaambia mataifa (Mathayo 28:19–20). Na kadri tunavyotii, nguvu za miungu adui, mamlaka na nguvu, zinapungua—nafsi kwa nafsi, wakati kwa wakati. Malango ya kuzimu, ulimwengu wa wafu, *havistahimili* ufufuko, na *havitaweza* kustahimili kuendelea kwa injili.

Wakati wa kusulubiwa kwa Yesu, ingawa, hakuna hata kimoja kati ya hivi kilionekana kweli kwa wanafunzi. Lakini wangepata ujumbe punde kwa njia ya ajabu, isiyosahaulika.

## SURA YA KUMI NA TATU

### Urejesho Mkuu

Mbali na habari za Yesu kwenye Injili—kama vile habari za kuzaliwa kwake, kifo, na Mahubiri yake mlimani—huenda kifungu kinachofahamika zaidi katika Agano Jipya ni Matendo 2, ambapo Roho Mtakatifu alitembea kwa kasi juu ya wafuasi wa Yesu katika siku ya Pentekoste. Ni alama ya uzinduzi wa kanisa lenye mbawa na mwanzo wa uinjilisti wa kimataifa katika jina la Yesu.

Kama vile kifungu kinavyojulikana, kuna mengi yanayoendelea ndani yake kuliko wengi wanavyojua. Matendo 2 kwa hakika imebuniwa kuendesha kampeni ya kurejesha jiografia ya ulimwengu baada ya Babeli katika Agano la Kale, ambapo mataifa mengine isipokuwa Israeli yalikuwa chini ya utawala wa miungu wadogo. Kilichotokea siku ya Pentekoste ilikuwa ni vita ya kuyafikia mataifa yote yaliyoachwa na Mungu pale Babeli kwa injili ya Yesu—mkakati wa zamani wa vita ya kiroho.

### Pentekoste

Kile ambacho Matendo 2 inaelezea kuwa kinatokea katika siku ya Pentekoste kwa hakika hakikuwa cha kawaida:

Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafla toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukaenda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyika, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka. Na walikuwako Yerusalemu wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu. Basi sauti hiyo iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja

aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe. Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, tazama, hawa wote wasemao si wagalilaya? Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo?" (Matendo 2:1–8 LEB)

Baadhi ya vitu ambavyo vinatupeleka kwenye mtazamo wa ulimwengu wa kimungu katika Agano la Kale katika kifungu hicho cha ajabu haviko wazi sana katika tafsiri za kiingereza. "upepo uendao kasi" unaohusishwa na kuwasili kwa Roho ni maelezo yanayofahamika ya uwepo wa Mungu katika Agano la Kale (2 Wafalme 2:1, 11; Ayubu 38:1; 40:6). Moto pia ni kitu kilichozoeleka katika taswira za Mungu (Ezek. 1:4; Isa. 6:4, 6; Dan. 7:9; Kutoka 3:2; 19:18; 20:18).

Ni wazi kutoka kwenye rejea hizo kuwa Mungu alikuwepo kwenye tukio na nyuma ya kile kilichokuwa kinaendelea. Lengo lake lilikuwa ni kuanzisha kampeni ya kuyarejesha mataifa kutoka kwa miungu wadogo aliowaweka juu ya mataifa (Kumbukumbu 4:19–20; 32:8–9) bali ni nani walikuwa maadui wake (Zaburi 82).

Chombo cha Mungu cha kulifanya hilo yalikuwa ni maneno ya wanafunzi—hivyo picha za ndimi (yaani kunena kwa lugha). Mungu aliwezesha wafuasi wa Kiyahudi wa Yesu kuzungumza na Wayahudi wengine waliokusanyika katika Pentekoste—ambao waliishi kwenye mataifa *yote* chini ya utawala wa miungu adui. Waliposikia injili na kuamini, wangerudi kwenye mataifa yao na kuwaambia wengine kuhusu Yesu.

## Pentekoste na Babeli

Tukio la Mnara wa Babeli ndio kitu kilichopelekea maamuzi ya Mungu kuyatawanya mataifa na kuyaweka chini ya utawala wa miungu mingine (Kumb 4:19–20; 32:8–9). Katika mtazamo wa kwanza hapaonekani sana kuwa uhusiano kati ya tukio hilo na kile kilichotokea kwenye Matendo 2. Lakini katika lugha halisi, kuna mahusiano wazi kati ya matukio hayo mawili.

Mambo mawili muhimu katika Matendo 2 yanaunganisha matukio yake na Babeli. Kwanza, ndimi za moto zinaelezwa kama "zimegawanyika,"na pili, kusanyiko, lililokuwa na Wayahudi kutoka mataifa yote, wanasemekana "kuchanganyikiwa." Kwa kiingereza, hilo haliwezi kuonekana kushawishi. Luka anaandika kwa Kigiriki, na maneno ya kigiriki aliyoyatumia hapa yametafsiriwa kama "zilizogawanyika" na "wakashikwa fadhaa" yanatoka kwenye Mwanzo 11:7 na Kumbukumbu 32:8, yote yanaelezea mgawanyiko wa lugha na mataifa pale Babeli na kuchanganyikiwa kuliko tokea.

Luka, mwandishi wa Matendo ya Mitume, alikuwa ni mtu wa mataifa. Aliweza tu kusoma Kigiriki. Hivyo, alikuwa anatumia tafsiri za Kigiriki za Agano la Kale zilizojulikana sana wakati ule (na hata sasa) kama tafsiri ya kale ya Biblia ya Kiebrania kwenda kwenye Kigiriki (Septuagint). Lilikuwa ni Agano la Kale la kanisa la mwanzo, kwa kuwa watu wachache waliweza kusoma Kiebrania. Luka alikuwa anafikiria tukio la Babeli wakati alipoandika Matendo 2.

Lakini kwa nini kuhusianisha? Fikiri kuhusu kile kilichotokea wakati wa Pentekoste. Roho alikuja kama Mungu alivyokuwa anakuja mara nyingi kwenye Agano la Kale, kwa upepo uvumao kasi na moto. Kuchanganyikiwa kwa uwepo wa lugha nyingi (ambazo ni matokeo ya Babeli) kuliondolewa wakati ndimi za moto zilipowawezesha wanafunzi kunena kwa lugha za Wayahudi kutoka sehemu zote za dunia waliokusanyika Yerusalemu kwa ajili ya sherehe. Elfu tatu kati yao waliamini ujumbe kuhusu Yesu (Matendo 2:41).

Waumini hao wapya ambao walimpokea Yesu kama Masihi wangepeleka ujumbe huo kwenye nchi zao—mataifa yaliyotawanywa pale Babeli. Nyuma kwenye Mwanzo 11, Mungu alikuwa amegeuza uso wake mbali na mataifa haya ya watu, na baada ya hapo, katika Mwanzo 12, alimwita Ibrahimu kuanzisha taifa jipya la Mungu, na watu wa Mungu. Sasa

alikuwa anaenda kuwakusanya watu kutoka kwenye mataifa hayo yote aliyokuwa ameyakataa na kuwaleta kwenye familia yake ya waaminio pamoja na waumini wa Kiyahudi walio uzao wa Ibrahimu. Kwa wakati, Ufalme wa Mungu ungeenea kuliko ufalme wa miungu adui.

Sehemu ya ajabu ya haya yote ni orodha ya mataifa katika Matendo 2 na mpangilio yalivyowekwa. Kama ukiyatazama kwenye ramani, ungesogea kutoka mashariki, ambapo Wayahudi walikuwa uhamishoni mwishoni mwa Agano la Kale katika Babeli na Uajemi, upande wa magharibi hadi sehemu ya mbali iliyojulikana wakati huo. Walichukua umbali sawa na eneo kama mataifa yaliyo orodheshwa kwenye Mwanzo 10—yale yaliyowekwa chini ya miungu wadogo.

## Vita Vyetu Sio Juu ya Damu na Nyama

Sehemu kubwa ya kitabu cha Matendo ya Mitume ni kuhusu safari za kitume za Paulo. Paulo alikuwa mtume wa Mataifa—mtu ambaye mwanzoni alitumwa na Mungu kuanzisha makanisa katika mataifa nje ya Israeli. Hali ya safari na maisha ya Paulo, kama vile kukamatwa na Warumi, vilimpeleka wakati wote upande wa magharibi.

Kwenye nyaraka zake za Agano Jipya, Paulo mara nyingi alizungumzia kuhusu majeshi ya kiroho yaliyokuwa yakipinga huduma yake na kuenezwa kwa injili. Msamiati wake wa majeshi ya uovu ambayo himaya zake alizivunja kwenye uamsho wa Pentekoste unaonyesha kuwa alielewa mazingira ya Jiografia ya Agano la Kale. Je, umegundua mtiririko wa maneno yanayofanana katika maneno ya Paulo (yametolewa kwenye toleo halisi la biblia ya awali.(ESV) kwa majeshi ya giza yasiyoonekana?

- Falme/ mamlaka (Ef. 1:20–21; 6:12; Kol. 2:15)
- Mamlaka (Ef. 1:20–21; 3:10; 6:12; Kol. 2:15; 1 Kor. 2:6)

- Nguvu (Ef. 1:20–21; 3:10)
- usultani (Kol. 1:16)
- wakuu (Ef. 1:20–21; 1 kor. 8:5)
- enzi (Kol. 1:16)

Maneno haya yote yanaonyesha *tawala za kijiografia*. Kwa hakika, maneno kama haya haya yanatumika kwenye Agano Jipya na maandiko mengine ya Kigiriki ya watawala wa kisiasa. Lugha ya Paulo ni ile ya utawala wa eneo au himaya. Inaakisi namna Agano la Kale linavyoonyesha uhusiano wa ulimwengu wa roho na ulimwengu wa wanadamu: mataifa yaliyowekwa kando na Mungu chini ya utawala viumbe wa kiroho walio adui kwake na kwa watu wake

**"Nitakwenda Spania"**

Kitabu cha Matendo kinaishia kwa safari ya Paulo huko Rumi. Paulo alikuwa mfungwa, na alikuwa anaenda Rumi kwa sababu mbili: kujionyesha kwa Kaisari na kueneza injili. Lakini Paulo alijua kuyarejesha mataifa yaliyo chini ya miungu adui, alipaswa kufika hadi mwisho wa ulimwengu uliojulikana kwa wakati huo. Wakati wa Agano la Kale, sehemu hiyo ilikuwa ikiitwa Tarshishi. Katika siku za Paulo, liliitwa Spania. Paulo alipaswa kufika Spania kukamilisha huduma yake. Maneno yake kwa Warumi kabla ya kifungo chake yanatuambia alikusudia kabisa kufika Spania—upande wa magharibi hadi mwisho wa dunia kwa wakati wake—kulirejesha kila taifa kwa Yesu:

> Wakati wowote nitakaosafiri kwenda Spania [nitakuja kwenu]. Kwa maana natarajia kuwaona ninyi katika kusafiri kwangu, nakusafirishwa nanyi, moyo wangu ushibe kwenu kidogo. Basi nikiisha kuimaliza kazi hiyo, na kuwatilia muhuri tunda hilo nitapita kwenu, kwenda Spania. (Rum. 15:24, 28)

Paulo alipata motisha kwa kutambua kuwa mpango wa Mungu kurejesha ufalme wake ulikuwa umezinduliwa katika wakati wa maisha yake mwenyewe. Aliamini kuwa wakati "mataifa watakapokuwa wameingia kikamilifu" basi "Israeli yote itaokolewa" (Rum. 11:25–26). Alifikiri kuwa alipaswa kumalizia kile pentekoste ilichoanzisha.

## Kwa nini Hili ni Muhimu

Paulo alikuwa na mtazamo wa kimungu kwenye maisha yake yeye mwenyewe. Alijiona yeye mwenyewe kama chombo cha Mungu. Na ndivyo alivyokuwa. Lakini hivyo ndivyo walivyokuwa waumini wengine wasiotajwa ambao, baada ya Pentekoste, walitangulia mbele yake kutoka Yerusalemu kupenya ngome za kipepo pale walipoishi.

**Na hivyo sisi ni.**

Kama *sis*i ni vyombo vya Mungu kwa namna ile ile Paulo alivyokuwa chombo cha Mungu, basi kwa nini alikuwa na ushawishi mkubwa sana na ufanisi? Tofauti moja ni kuwa Paulo *alielewa* maisha yake yanahusu nini. Aliamini kuwa nguvu zilizokuwa na utawala juu ya dunia ni halisi—na kwamba nguvu iliyo nyuma yake na ndani yake ilikuwa ni kubwa.

Je, unaamini vitu hivyo? Biblia inaviweka mbele kama vilivyotolewa. Hivyo ndivyo Paulo alivyovichukulia katika maisha yake mwenyewe. .

Paulo hakujua kwa uhakika kuwa ulimwengu ulikuwa mkubwa kiasi gani. Hakujua kuhusu Amerika ya Kaskazini,Amerika ya Kusini, China, India, Norway, Australia, Iceland, na maeneo mengine mengi. Mungu alijua. Mungu alijua kazi ya kuieneza injili kwa ulimwengu wote hatimaye ingekuwa kubwa kuliko ambavyo Paulo angeweza kuelewa. Mungu alijua kuwa wengine wangepaswa kufuata lengo la Paulo kwa yeye mwenyewe kama injili ilitakiwa kufikia kila sehemu ya dunia. Kama hatujaribu kwa nguvu kukamilisha

kazi,hatufanyi kile ambacho tupo duniani kukifanya. Kama tunamtaka Mungu tu ili aje kwetu na kukutana na mahitaji yetu, basi tunakuwa zaidi kama watu wa Babeli kuliko tulivyo kama Yesu, wale kumi na wawili, na Paulo.

Kidokezo kingine cha kifungu cha maandiko tuliyoyaangalia ni kuwa mtazamo wa ngome za kipepo ni wa Kibiblia. Hatupewi maelezo ya kamili ya maeneo ya kipepo au mistari ya mipaka, au mpangilio wa vyombo vya kiroho vya upande wa giza. Tunaambiwa, hata hivyo, kwamba nguvu zisizoonekana zinaiona dunia kama himaya yao. Tunaambiwa nguvu hizo zinapinga ufalme wa Mungu na hazitaki watu wawe sehemu ya mpango wa Mungu kueneza utawala wake mzuri kila mahali. Hiyo inamaanisha tunapaswa kutegemea upinzani usioelezeka na mantiki au ushahidi dhahiri na hatuwezi hatuwezi kuzishinda sisi wenyewe. Mungu ametupa Roho na mawakala wasiooneka wake mwenyewe kutusaidia ili kuendeleza kusudi lake (1 Kor. 3:16; 6:19; Ebr. 1:13; 1 Yohana 4:4).

Swali halisi la kujiuliza sisi wenyewe ni hili: maisha yetu yangekuwaje kama tungeamka kila siku tukiwa na mtazamo wa ulimwengu na ushawishi wake wa kimungu ambao unalingana na wa Paulo? Ingekuwa vipi, kila siku, maisha yetu yangepangiliwa kulingana na maarifa yetu ya hadhi yetu kama sehemu ya familia ya Mungu, tuliopewa kazi ya kuwatoa ndugu zetu kutoka gizani? Vipi kama tukiishi kwa malengo, tukijua kuwa kila maamuzi tunayofanya na kila neno tunalozungumza hatusemi tu bila makusudi? Vipi kama, badala yake, tungeamini werevu wasioonekana na vyote vinavyotuzunguka vingetumia maamuzi yetu, matendo yetu, maneno yetu kuwashawishi watu wengine—kwa wema au ubaya—kwamba tunawaona au kuwajua au hatuwaoni wala kuwajua? Kazi zetu, pato letu, vipawa vyetu, hata matatizo yetu hayana athari wakati inapokuja suala kujua sisi ni nani *haswa,* na tutakavyokuwa, na kwanini tuko hapa. Hatuwezi kuona ulimwengu wa kimungu—

wala hatuwezi kuona ulimwengu wa darubini—bali haiepukiki kuwa sehemu ya vyote.

Waumini wa mwanzo walifikiri namna hii. Kama tutakavyoona kwenye sura inayofuata, waliamini kuwa ulimwengu uliowazunguka unatumikishwa na giza ambalo siku moja lingetoa mavuno. Licha ya ukweli kuwa vita kawaida ilikuwa yao dhidi ya ulimwengu adui na nguvu zake, kimya kimya walizalisha kitu cha ulimwengu wote tunachoita Ukristo, na Mungu na mawakala wake wasioonekana wanaofanya kazi pamoja naye. Waliamini kuwa mgogoro wa kiroho ulikuwa ni dhahiri na kwamba, hatimaye, wasingeweza kushindwa. Tunauishi uthibitisho ambao hawakuwa nao.

# SURA YA KUMI NA NNE

## Sio wa Ulimwengu Huu

Katika maombi ya Yesu yanayofahamika sana kwenye bustani ya Gethisemane kabla hajakamatwa kwenda kujaribiwa, alisema kuhusu wafuasi wake kuwa, "Wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu" (Yohana 17:16). Waaminio kwa hakika *walikuwa* ulimwenguni, hasa wakiwa wamepewa jukumu la kuipeleka injili kwa kila taifa (Mathayo 28:19–20), bali hawakuwa *wa* ulimwengu. Kitendawili—kuwa ulimwenguni lakini sio wa ulimwengu—kiliwasilishwa kwa kanisa la mwanzo kwa njia mbalimbali za kukumbukwa.

### Mahali patakatifu, Ardhi Takatifu, na Uwepo wa Mungu

Kwenye sura ya 8 tulizungumza kuhusu dhana ya mahali patakatifu. Kwa Waisraeli wa Agano la kale, Mungu alikuwa *mwingine* kabisa. Sehemu iliyokaliwa na uwepo wake ilitengwa kutoka kwenye sehemu nyingine. Hiyo ilikuwa siyo pingamizi kuwa Mungu yupo kila mahali—sehemu zote kwa nyakati zote. Badala yake, ilikuwa ni njia ya kuwekea alama mipaka ya mahali alipopachagua kukutana na watu wake. Hilo lilikuwa moja ya makusudi ya kuwa na hema na hekalu. Wazo la sehemu takatifu halikuwa tu msingi wa sheria nyingi za Israeli na ibada, bali pia lilisisitiza wazo la mgawanyo wa kijiografia—namna ambavyo ulimwengu ulivyokuwa umegawanywa miongoni mwa miungu wadogo na Mungu Aliye Juu Sana, Mungu wa Israeli.

Dhana ya sehemu takatifu inaletwa kwenye Agano Jipya kwa njia ya Ajabu kabisa. Tunachotakiwa kuuliza ni, "Uwepo wa Mungu uko wapi sasa hivi?" wakati Mungu yupo kila mahali, kipekee kabisa anakaa *ndani ya kila mwamini* . Amini usiamini, *wewe* ndiyo sehemu takatifu. Paulo kwa uwazi kabisa aliandika kuwa "mwili wako ni hekalu la Roho Mtakatifu" (1 Kor. 6:19).

Kitu hicho hicho ni kweli kuhusu ardhi ambayo waamini wanakusanyika kama kundi. Akiliandikia kanisa la Korintho, Paulo aliwaambia kwa pamoja, "Ninyi ni Hekalu la Mungu" (1 Kor. 3:16). Aliwaambia waamini wa Efeso kuwa walikuwa "watu wa nyumbani mwa Mungu…hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye ninyi nanyi mnajegwa mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho" (Ef. 2:19, 21–22).

Vidokezo vinashangaza. Wengi wetu tunaifahamu kauli ya Yesu, "walipo wawili au watatu wamekusanyika kwa ajili ya jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao" (Mathayo 18:20LEB). Lakini kwa kuitazama kwa muktaza au mazingira ya Agano la Kale wa wazo la sehemu takatifu, kauli hiyo ina maana kuwa popote waamini wanapokusanyika, ardhi ya kiroho waliyopo inatakaswa kukiwa na nguvu za giza.

Sehemu ya mwisho ya Yahwe iliyochaguliwa kukaa katika Agano la Kale ilikuwa ni Israeli—hekalu la Yerusalemu. Israeli ilikuwa ardhi takatifu kwa sababu hapo ndipo Uwepo wa Mungu ulipokaa. Lakini ardhi hiyo takatifu ilikuwa inatishwa au kuhatarishwa na mataifa yaliyoizunguka na miungu yao adui. Kwa namna ile ile, waamini leo wapo katika vita ya kiroho. Sisi sasa ni Hekalu la Mungu, mahali maalumu Roho wa Mungu anapokaa,sehemu ya nuru ya uwepo wake—na tumetawanyika kote ulimwenguni katika utumwa wa nguvu za giza.

### Kuwatoa kwa Shetani

Wazo hili limeelezewa vyema na mtazamo wa Paulo kwenye utakatifu wa Kanisa. Kila mwili wa mwamini ulikuwa ardhi takatifu, hakuna nafasi ya dhambi isiyotubiwa.

Katika sura ya 8 tulitazama namna kambi ya Israeli ilivyoshughulika na dhambi kuhifadhi utakatifu wa kambi—sehemu yake takatifu. Tulizungumza kuhusu Siku ya Upatanisho (Walawi 16), ambapo dhambi ya taifa kiibada ilihamishiwa kwa mbuzi—yule wa "Azazeli" (Walawi 16:8, 10).

Azazeli ni kundi la kipepo linalodhaniwa kukaa nyikani. Waisraeli walipeleka mbuzi nyikani, akizichukua dhambi zao. Tendo hilo kiishara kilipeleka dhambi za watu mahali ambapo zinamilikiwa—huko nyikani, sehemu ya giza la kiroho.

Paulo anawataka Wakorintho kushughulikia dhambi kwa njia inayofanana—kuipeleka ambapo ni sehemu yake.

Katika 1 Wakorintho 5, Paulo aliandika kwa Wakorintho kuhusu mtu aliyeishi kwa zinaa ambaye anatakiwa kutubu. Aliagiza "Kumtolea Shetani mtu huyo" (1 Kor. 5:5GNT). Hoja ya msingi iko wazi—dhambi haina nafasi kwenye ardhi takatifu. Waamini walipaswa kumuondoa mwamini asiyetubu kanisani (1 Kor. 5:9–13). Kufukuzwa kutoka kanisani ilikuwa ni kuzamishwa kwenye ulimwengu wa Shetani, nje katika ulimwengu.

Paulo aliamini matokeo kwa mtu asiyetubu ni "mwili uadhibiwe, ili na roho iokolewe katika siku ya Bwana Yesu" (1 Kor. 5:5). (Kinachorejelewa hapa sio kufa kimwili, bali kufa kwa tama ya mwili inayomsumbua mtu huyo [Gal. 5:24; 1 Kor. 11:32–33]).

## Ubatizo kama Vita ya Kiroho

Msimamo wa Petro kwenye jambo hili ni sawa na wa Paulo—waamini walitengwa dhidi ya nguvu za giza. Mawazo yake ya vita yanapatikana katika moja ya vifungu vyake vigeni katika Agano Jipya, 1 Petro 3:14–22:

> Lakini mjapoteswa kwa sababu ya haki mna heri. Msiogope kutisha kwao, wala msifadhaike; bali mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu. Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu. Nanyi mwe na dhamiri njema, ili katika neno lile mnalosingiziwa, watahayarishwe wale wautukanao mwenendo wenu mwema katika Kristo. Maana ni afadhali kuteswa kwa kutenda mema, ikiwa ndiyo

mapenzi ya Mungu, kuliko kwa kutenda mabaya. Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili ya wasio haki, ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa, ambayo kwa hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri; watu wasiotii hapo zamani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane, waliokoka kwa maji. Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo. Naye yupo mkono wa kuume wa Mungu, amekwenda zake mbinguni, malaika na enzi na nguvu zikiisha kutiishwa chini yake. (LEB)

Nina uhakika umegundua vitu vya ajabu kwenye kifungu hiki. Je, Safina, Nuhu, na roho waliokaa kifungoni vina kazi gani na ubatizo? Na je, hiki kifungu kinasema ubatizo unatuokoa?

Kitu anachofanya Petro hapa kinafanana na kitu fulani anachofanya Paulo kwenye Warumi 5. Paulo alizungumza kuhusu Yesu katika kifungu hicho, lakini akiwa na Adamu akilini vilevile. Mfikirie Yesu kama, kwa namna fulani kinyume cha Adamu. Hii ndiyo sababu Paulo anasema vitu kama "kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja [Adamu] watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja [Yesu] watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki (Rum. 5:19). Petro ana Henoko, badala ya Adamu, katika akili wakati anapoandika kuhusu Yesu kwenye 1Petro 3. Lakini kwa Petro, Henoko, na Yesu hawakuwa kinyume. Henoko anatumika kama kiungo cha hoja Petro anayotaka kutoa kuhusu Yesu.

Unaweza kushangaa, "Hoja gani?", Hata hivyo, kuna msitari michache kuhusu Henoko kwenye Agano la Kale. (Mwanzo 5:18–24). Tunachojifunza tu hapo ni kwamba aliishi kabla ya

gharika kuu na kwamba "Henoko aliendа pamoja na Mungu; naye akatoweka, maana Mungu alimtwaa" (Mwanzo 5:24 NIV). Hiyo mistari kwa kweli haina uhusiano wowote na anachokisema Petro katika 1 Petro 3 kuhusu Yesu.

Kuelewa kwa nini kitu alichofanya Henoko kilimkumbusha Petro, kuhusu Yesu, tunahitaji kuelewa kwamba Petro alisoma kuhusu Henoko kwenye vitabu vya Wayahudi nje ya Agano la Kale. Hususani, Petro alikuwa anafahamu kitabu cha kale cha Wayahudi kilichokuwa na mengi ya kusema kuhusu Henoko. Kilipewa jina, inavyotabirika, Henoko 1. Kitabu hicho kilijaa undani kuhusu kilichotokea wakati wa gharika, hasa tukio la Mwanzo 6:1–4, ambapo wana wa Mungu (Henoko anawaita waangalizi) walizaa watoto (Wanefili majitu) na wanawake wanadamu. Wakati wote Petro na Yuda wanaandika kuhusu malaika waliasi katika siku za Nuhu (2 Pet. 2:4–5; Yuda 6), walikuwa wanadokeza mawazo ya kwenye Henoko 1 ambayo siyo sehemu ya habari za kibiblia za gharika. Tukio la gharika la Mwanzo, kwa mfano, kamwe halituambii kwamba wana wa Mungu wa kimungu walikuwa kifungoni katika ulimwengu wa wafu chini ya dunia mpaka siku za mwisho, bali 1 Henoko inasema (1 Henoko 6:1–4; 7:1–6; 10:4, 11–13).

Kitu fulani kilichotokea kwa hawa "roho kifungoni"kwenye kitabu cha Henoko 1 kilimpa Petro ufahamu kwa Yesu. Katika habari ya Henoko 1, Henoko aliota ndoto ambapo roho zilizofungwa zilimuomba afanye maombezi kwa Mungu kwa niaba yao. Baada ya yote, Henoko aliendа na Mungu—nani bora kumwomba Mungu kwa toba na kuachiliwa kwao? Henoko alifanya hivyo, lakini alipata habari mbaya. Jibu la Mungu lilikuwa kwa msisitizo *Hapana*. Henoko baadae alipaswa kuwapa jibu hilo—alishuka kwa roho zilizokuwa kifungoni. Aliziambia kuwa bado zilikuwa chini ya hukumu.

Petro alitumia hadithi hiyo kama ulinganisho kwa Yesu. Hoja aliyotaka kuileta ni kuwa wakati Yesu alipokufa, alishuka kwenye ulimwengu wa wafu na alikuwa na ujumbe wa viumbe

wa kimungu walioanguka pale. Wakati walipomwona Yesu akiingia sehemu ya wafu, wangeweza kufikiri pepo mwenzao ameshinda na wangetoka kifungoni punde. Badala yake, Yesu aliwaambia wasingemwona kwa muda mrefu—angefufuka tena. Hiyo yote ilikuwa sehemu ya mpango wa Mungu. Walikuwa hawajashinda—*bado walikuwa chini ya hukumu na wamepotea milele*. Hii ndiyo sababu kifungu hichi cha ajabu kinaishia jinsi kilivyoishia, na Yesu "kwenda mbinguni" na kukaa "mkono wa kuume wa Mungu, na malaika na enzi na nguvu zikiisha kutiishwa chini yake (1 Pet. 3:22).

Kwa nini Petro anayaunganisha haya yote na ubatizo? Kwenye akili ya Petro, Kufa na kufufuka kwa Yesu—vinakamilishwa na tangazo kwa nguvu za kipepo la ushindi wake—ilikuwa ni ishara ya ubatizo. Ubatizo unaashiria, kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu (Rum. 6:1–11).

Kwa Petro, ubatizo "unahusiana" na haya yote kwa sababu ni "Itikio kwa Mungu ya dhamiri njema kwa njia ya ufufuko wa Yesu Kristo" (1 Pet. 3:21). Neno la Kigiriki "Itikio" linamaana ya ahadi mtu anayoweka. Neno la kigiriki la "dhamiri" mara nyingi linamaanisha uwezo wa kusema kilichosahihi toka kisichosahihi. Lakini hoja siyo hiyo hapa. Kujua tofauti kati ya kilicho sahihi na kisicho sahihi havina uhusiano mahususi na kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu. Neno la Kigiriki linaweza pia kuonyesha kuweka agano—na aliye mwema, sio na mpumbavu. Hicho ndicho Petro anachokielekea katika 1 Peter 3. Kwa kina, *ubatizo ulikuwa kiapo na ujumbe kwa nguvu za kipepo* (pamoja na watu wowote waliopo) wa upande wowote uliokuwa katika vita ya kiroho. Wakristo wa mwanzoni walilielewa hili vyema kuliko sisi wa leo. Ibada ya Ubatizo wa kanisa la mwanzo ilijumuisha kukataliwa Shetani *na malaika wake* kwa sababu ya kifungu hiki.

### Kwa nini Hili ni Muhimu

Kwanza, elewa kwamba waamini ni ardhi takatifu, mahali panapokaa uwepo wa Mungu—utukufu wa Agano la Kale. Je, tunaishi ivyo? Waisraeli na waamini wa Yesu leo waliohisi uwepo daima wanapaswa kuwa tofauti na wasioamini. Lengo sio kukusudia kuwa wa ajabu ili wasioamini waepuke mahusiano. Israeli ilikuwa iwe "ufalme wa makuhani" na "taifa takatifu" (Kutoka 19:6). Kuishi namna Mungu alivyotaka watoto wake waishi kunapelekea kuzaa matunda, uzalishaji, maisha ya furaha. Waisraeli walipaswa kuwavutia watu walio katika utumwa wa miungu adui kurejea kwa Mungu wa kweli.

Wakati mtizamo wetu wa kidunia unapoungana na mpango wa Mungu kuwaokoa watu toka kila taifa, kuwafanya wawe sehemu ya familia ya Mungu, sisi si wa dunia hii. Kuwa wa dunia hii ni kumezwa na mambo ya dunia na kuishi ipasavyo. Wasioamini wanapaswa kuweza kueleza kutoka kwenye kauli zetu, tabia, maadili, na nia yetu kwa wengine kuwa sio wabaguzi, wabinafsi, au wakatili— kuwa msisitizo wetu sio kusonga mbele au kuwatumia watu. Hatupaswi kuishi kwa kujifurahisha wenyewe. Tunapaswa kuwa kinyume cha mambo haya. Kwa maneno mengine, tunapaswa kuishi kama Yesu alivyoishi. Watu walitaka kuwa karibu naye *kwa sababu* hakuwa kama wengi wengineo.

Pili, vile tunavyovifanya makanisani mwetu vinapaswa kumwinua Mungu na Yesu. Katika wakati wa biblia, kutembelea hemani au hekaluni kulihimiza mawazo ukamilifu wa Mungu, upekee—na upendo kwa watoto wake. Vitu hivyo vinaenda bega kwa bega.kwa nini Mungu ambaye hahitaji kitu na ni mkuu kwa kila kitu atake familia ya wanadamu? Kwa nini Mungu huyo hangaike kuanzisha familia mpya baada ya kuyaweka kando mataifa pale Babeli, kuyaweka kwa miungu mingine? Kwa nini asiachane huko? Kwa sababu anatupenda.

Ni kwa sababu tunajua Mungu angefanya kitu kingine bali hakufanya kwamba upendo wake unaendelea kuwa na maana. Wakati kanisa linazungumzia tu upendo wa Mungu bila kuonyesha kejeli ya upendo huo wakati unapowekwa dhidi ya sifa za tabia nyingine za Mungu, waamini wataupuuza huo upendo. Unaweza kuonekana rahisi, kwa mfano, kwa watu wasiojua utakatifu wa Mungu.

Kidokezo cha tatu cha kile tulichojadili katika sura hii ni kwamba nguvu za giza zinajua tuko upande wa nani kwa tabia zetu. Wao sio wajinga. Wanaona uaminifu wetu kwa Mungu, na wanatuona tukitekeleza maamuzi yetu ya kumfuata Yesu kupitia vitu kama ubatizo na kukataa dhambi. Bali pia wanatuona tunapokosa uaminifu kwa Mungu kwa Mungu, na wanaelewa ni hatari gani hilo linaleta kwenye maisha yetu. Kwamba tunaamini au hatuliamini, tunatazamwa—*na pande zote* za vita vya kiroho.

Ukweli huu ni rahisi kuuelewa kuliko kuuishi. Ingawa tumekombolewa, tumeanguka. Kuuishi ukweli huu, tunahitaji akili zetu na mioyo yetu kuelekezwa kwa nini tuko hapa, tukiishi kama wageni katika ulimwengu wetu wenyewe. Kama alivyo Yesu, sisi si wa ulimwengu huu—tukiwa ndani yake, lakini sio wa huo (Yohana 8:23; 1 Yohana 4:4). Tofauti hiyo, na hadhi yetu, itakuwa kali zaidi mara tutakapokuwa tumeshika nini maana ya kuwa watoto wa Mungu.

## SURA YA KUMI NA TANO

## Washirika wa Tabia ya Uungu

### J*e, unajua wewe ni nani*?

Niliuliza swali hili mwanzoni, lakini ni wakati wa kuliibua tena. Ndiyo, tupo ulimwenguni lakini sio wa ulimwengu. Kweli, tumeokolewa kwa neema kwa njia ya imani katika kile alichofanya Yesu msalabani (Ef. 2:8–9). Lakini huo ni mwanzo tu wa kuelewa Mungu amekuwa akitaka nini.

Dhamira halisi ya Mungu ilikuwa ni kuunganisha familia yake ya kibinadamu na familia yake ya kimungu, wana wa Mungu wa mbinguni ambao walikwepo kabla ya uumbaji (Ayubu 38:7–8). Hakuuacha mpango huo wakati wa anguko. Mkristo, utabadilishwa kuwa wa kimungu, kama mmoja wa wana wa Mungu *elohimu,* kama Yesu mwenyewe (1 Yohana 3:1–3).

Wanatheolojia wamelipa wazo hilo majina mengi. Ambalo linafahamika sana ni *kutukuzwa.* Petro analiita wazo hilo kama kuwa "warithi wa tabia ya Uungu" (2 Pet. 1:4). Yohana analiweka hivi: "Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; *na ndivyo tulivyo"* (1 Yohana 3:1, msisitizo umeongezwa). Katika sura hii tutatazama jinsi Biblia inavyo wasilisha ujumbe huo.

### Wana wa Mungu, Uzao wa Abramu

Wakati Mungu alipoyaachilia mataifa ya ulimwengu kwa miungu wadogo pale Babeli, alifanya hivyo akijua ataanza upya na familia mpya ya kibinadamu yake mwenyewe. Mungu alimwita Abramu (Mwanzo 12:1–8) mara tu baada ya Babeli (Mwanzo 11:1–9). Kupitia Abramu na mkewe Sara, Mungu angerejea kwenye mpango wa mwanzo wa Edeni.

Watu wa Mungu, wana wa Abramu, Waisraeli, hatimaye walishindwa kurejesha utawala mzuri wa Mungu duniani. Bali mmoja wa hao wana *angefanikiwa*. Mungu angekuwa mtu katika Yesu, uzao wa Daudi, Abramu, na Adamu. Na ilikuwa ni kupitia Yesu ambapo ahadi ya Mungu ya kuyabariki mataifa yote aliyo yaadhibu pale Babeli ilitimizwa. Paulo aliandika kuhusu hilo maeneo kadhaa. Hapa zipo mbili:

Ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo, kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache. Kwa hayo, myasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo. Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho. Ya kwamba mataifa ni warithi pamoja nasi wa urithi mmoja, na wa mwili mmoja, na washiriki pamoja nasi wa ahadi yake iliyo katika Yesu kwa njia ya Injili." (Ef. 3:3-6LEB)

Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Yesu. Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu na warithi sawasawa wa ahadi. (Gal. 3:26-29LEB)

Kama nilivyoeleza kwenye sura za zilizotangulia: katika Agano lote la Kale, watu wote ambao walikuwa sio Waisraeli waliishi kwenye maeneo yaliyokuwa yamewekwa chini ya utawala wa miungu wadogo ambao Mungu aliwakabidhi mataifa hayo pale Babeli. Pale Babeli, mataifa mengine tofauti na Israeli yalikuwa yametengwa kutoka kwenye uhusiano na Mungu wa kweli. Israeli na ni Israeli pekee ilikuwa "sehemu" ya Mungu (Kumbukumbu 32:9) ya kibinadamu. Waisraeli waliwaita watu wa mataifa yaliyotengwa kwa majina mengi. Kulikuwa na utambulisho wa Kijiografia au Kikabila (mfano, Wamisri, Wamoabi, Waamaleki) lakini maelezo

yanayoeleweka katika wakati wa Agano Jipya ilikuwa ni mataifa, jina linalotokana na neno la Kilatini "Mataifa" (*gens"-'watu ambao ni ndugu'*). Kama wewe sio Myahudi, wewe ni mataifa.

Habari ya Agano Jipya ni kwamba uzao wa Ibrahimu—Yesu—alikufa na akafufuka tena kuwakomboa sio tu uzao wa Ibrahimu (Waisraeli/Wayahudi) bali watu wote miongoni mwa mataifa ambayo hapo awali yalitengwa na Mungu wa Kweli. Kwenye mistari iliyonukuliwa hapo juu, Paulo aliita ujumuisho wa mataifa kwenye familia ya Mungu siri. Ilimshangaza kwamba watu kutoka katika mataifa ambayo Mungu aliyatupilia mbali, na ambayo yalikuwa chini ya utawala wa miungu mingine, wangeweza kurithi ahadi iliyotolewa kwa Ibrahimu.

Katika Kristo, *wote* wanaoikumbatia injili ni wana wa Yahweh, Mungu wa kweli, Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo (Yohana1:12; Gal. 3:26; Rum. 8:14). Hii ndiyo sababu Agano Jipya linazungumza kuhusu waaminio kwa kutumia maneno ya kifamilia (wana, watoto, warithi) na lugha ya "kufanywa" wa Mungu (Rum. 8:15, 23; Ef. 1:5; Gal. 4:4). Lugha ya urithi ni kioo au kiashiria wazi na ina makusudi. Inatuambia sisi ni nani: familia mpya ya kiungu-ya wanadamu wa Mungu. Hatima ya waaminio ni kuwa kile Adamu na Hawa walikuwa awali: wa milele, sura iliyotukuzwa ya Mungu, kuishi katika uwepo wa Mungu.

Lakini hata hiyo haielezi kwa ukamilifu sisi ni nani. Sehemu ya kushangaza zaidi ni jinsi Yesu anavyotuona sisi.

## Muunganiko wa Familia Tena

Sura mbili za mwanzo za kitabu cha Waebrania, kinatupa picha ya ajabu ya familia ya Mungu iliyounganishwa pande mbili—ya kimungu na ya wanadamu. Kwangu mimi, ni moja ya vifungu vinavyosisimua zaidi katika biblia.

Waebrania 1 inaleta hoja kuwa Yesu ni "bora sana kuliko malaika" (mst. 4LEB). Hakuna aliye juu katika baraza la Mungu la mbinguni kuliko Yesu. Pamoja na yote, yeye ni Mungu. Kwa hakika, mwandishi anajenga hoja kuwa, kwa kuwa hakuna malaika aliyestahili kuwa mtu na kurithi ufalme, malaika wanapaswa kumwabudu Yesu (mst. 5–6LEB). Yesu ni mfalme.

Chakushangaza, wakati Yesu alipokuwa mtu, kwa muda mfupi alikuwa chini kuliko malaika. Alikuwa mmoja wetu. Wanadamu ni viumbe wa chini kuliko viumbe wa kimungu kama malaika. Mwandishi wa Waebrania anauliza:

Mwanadamu ni nini hata umkumbuke, Ama mwana wa binadamu, hata umwangalie? Umemfanya mdogo punde kuliko malaika. Umemvika taji ya utukufu na heshima, Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; Umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake. Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake hakusaza kitu kisichowekwa chini yake. Lakini sasa bado hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake, ila twamona yeye aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, yaani, Yesu, kwa sababu ya maumivu ya mauti, amevikwa taji ya utukufu na heshima ili kwa neema ya Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu. (Ebr. 2:6–9).

Matokeo ya alichofanya Yesu ni nini? Tunaweza kusema ni *wokovu*. Hiyo inaweza kuwa sawa, lakini inakosa kile mwandishi wa Waebrania anachotaka sisi tujue. Kwa sababu Mungu alifanyika mtu katika Yesu Kristo, wafuasi wake walio katika hali ya kufa watafanyika kuwa miungu—na watu wa familia moja.

Siku moja, kama ni katika mauti yetu au kurudi kwake duniani katika mfumo wa mwisho wa ufalme duniani, Edeni mpya, Yesu atatutambulisha katika baraza la kimungu, na atalitambulisha baraza kwetu. Alifanyika kama tulivyo, hivyo twaweza kuwa kama alivyo:

Kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyote vimekuwapo, akileta wana wengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso. Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake; akisema

"Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu;

Katikati ya kanisa nitakuimbia sifa.

Na tena, Nitakuwa nimemtumaini yeye.

Na tena, Tazama mimi nipo hapa na watoto niliopewa na Mungu"

(Ebr. 2:10–13 LEB)

Badala ya kuaibishwa mbele ya *elohimu* wa baraza la Mungu kwa kuwa mwanadamu—kuwa mdogo kuliko walivyo—Yesu anafurahia katika hilo. Hayo yote yalikuwa sehemu ya mpango mkuu. Kusimama katika baraza ("katika kusanyiko") alituwakilisha: *Tazama—niangalieni mimi, na watoto Mungu alionipa. Sote kwa pamoja sasa—milele*. Na huo ulikuwa ni mpango toka mwanzo.

Kuingia kwetu katika familia ya kimungu, iliyotukuzwa ni hatma yetu. Paulo analiweka vizuri kwenye Warumi 8:18–23:

Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu. Kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu. Kwa maana viumbe vyote pia vilitiishwa chini ya ubatili; kwa kuwa viumbe vyenyewe navyo vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata viingie katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu. Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vinautungu pamoja hata sasa. Wala si hivyo tu; ila na sisi wenyewe tulio na malimbuko, ya

Roho, sisi pia tunaugua katika nafsi zetu, tukikutazamia kufanywa wana, yaani, ukombozi wa mwili wetu.

Paulo aliwatia moyo waaminio kwa ujumbe sawa na huo. Aliwaambia Warumi waaminio walikuwa “amewachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi” (Rum. 8:29LEB). Aliliambia kanisa la Korintho, “Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.” (2 Kor. 3:18), na kwamba utu wetu utabadilishwa, “maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, na huu wa kufa uvae kutokufa” (1 Kor. 15:53). Kwa Petro, kuungana na baraza la familia ya Mungu ina maanisha kuwa, “washirika wa tabia ya Uungu” (2 Pet. 1:4). Yohana alisema kwa urahisi zaidi: “Tutafanana naye” (1 Yohana 3:2).

## Kwa nini Hili ni Muhimu

Kama Wakristo, huenda tumesikia mara nyingi kuwa tunapaswa kufanana na Yesu. Kwa hakika tunapaswa kuwa hivyo. Lakini tunapolisikia hilo, huwa tunatafakari *tu* kwa msingi wa kuwa mwema, au “ubaya kidogo.” Tunageuza kuwa kile ambacho kinakaribia kuwa wazo lisiloeleweka—kwamba siku moja tutafanana na Yesu ni—wajibu wa utendaji.

Badala ya kuhisi hatia kuhusu namna tusivyofanana na Yesu, na kuahidi katika mioyo yetu “kufanya vyema,” tunapaswa kuiachia Baraka ya kile alichofanya, na atafanya, abadilishe namna tunavyofikiri kuhusu kuwa kama yeye. Tunaweza kubadilisha kuwa kama Kristo kuwa wajibu ambao lazima tuufanye ili Mungu asitukasirikie, bali hiyo ni theolojia mbaya. Inageuza neema kuwa wajibu. Au tunaweza kufurahia kwamba siku moja tutakuwa kile Mungu alichofurahia

kutufanya—kile kilichokuwa toka asili (Rum. 8:29)—na kuishi kwa namna ambayo watu wanaotumikishwa na nguvu za giza watatamani kujiunga nasi katika familia ya Mungu. Mtazamo mmoja unatazama ndani; mwingine unatazama mbinguni.

Maisha ya Mkiristo *sasa* sio kuhusu hofu kwamba tutashindwa kumfurahisha Yule aliyetupenda tulipokuwa tungali tukitumikishwa na nguvu za giza. Maisha ya Mkristo hasa ni kuhusu kuelewa mambo mawili: kufanywa kwetu kuwa familia ya Mungu—ambayo ina maanisha Yesu ni kaka yetu, na kwamba Mungu anatupenda kama anavyompenda Yesu—na kusudi letu katika mpango wa Mungu ni kurejesha ufalme wake duniani. Tuko, na tutakuwa, *Baraza Jipya la kimungu la Mungu* . Yeye ni Baba yetu, sisi tu watoto wake, waliokusudiwa kuishi anapoishi milele. tu watenda kazi pamoja naye, tuliopewa kazi ya kumsaidia kuwatoa wale ambao bado wanamilikiwa na bwana wa mauti na kushikiliwa mateka na nguvu za giza zisizoonekana.

*Hicho* ndicho Biblia inahusu, kutoka Edeni kwenda Edeni. *Hiyo* ni hatma yako. Maisha yako sasa hayahusu kutafuta nafasi katika familia ya Mungu. Hiyo haiwezi kutafutwa. Ni zawadi. Maisha yako sasa ni kutambua kufanywa kwako kuwa mwana, furahia, na kuwaleta wengine kushiriki pamoja na wewe.

# SURA YA KUMI NA SITA

## Kutawala Juu ya Malaika

Ni muhimu kwa imani yetu kwamba tunaelewa sisi ni nani kama Wakristo. Sisi ni wana wa Mungu wa kiume na wa kike, baraza la Mungu lililofanywa upya ambalo tayari linashiriki katika ufalme wa Baba yetu. Lakini kuna mengi zaidi ndani yake kuliko hilo. Ndiyo, sisi ni baraza la familia ya Mungu—lakini kwa mwisho upi?

Wakati tayari tukiwa katika ufalme (Kol. 1:13), hatujaona kwa ukamilifu ufalme huo ukifunuliwa—hatujaona ulimwengu ukiwa Edeni. Hii "tayari, lakini bado" ni kitendawili ambacho kinapita katika Biblia kwa njia nyingi. Katika sura hii, nataka kuwapa mtazamo wa "bado" hiyo inajibu swali "Kwa mwisho upi?"

### Ushiriki katika Ufalme sasa

Ushiriki wetu katika ufalme wa Mungu haujapangwa kabla, katika mtazamo huu: sisi sio maroboti tu yanayofanya kazi yaliyopangiwa. Hiyo inakiuka wazo zima la kuwa sura ya Mungu, wawakilishi wake. Tuliumbwa tuwe kama yeye. Yuko huru. Kama hatuna uhuru halisi, hatuwezi kuwa kama yeye—kwa ufafanuzi, tusingeweza kuwa kama yeye. Tuko huru kutii na kuabudu, au kuasi na kujifurahisha wenyewe. Na tutavuna tulichopanda. Kupanda kwetu hakujapangwa.

Lakini Mungu ni mkubwa kuliko tulivyo. Alikuwa na mpango na utakuja kupita. Mafanikio yake hayategemei wala kulazimisha kushikamana na uhuru wa mwanadamu. Hatuwezi kuudhofisha sisi —wala viumbe wa Kiungu ambao nao pia wana uhuru wa kuchagua.

Fikiri kuhusu mkutano wa baraza la mbinguni niliokuonyesha kwenye sura ya 1. niliuliza kama unaamini vitu Biblia inavyosema, na kisha kukupeleka kwenye mkutano wa

Mungu na baraza lake la mbinguni katika 1 Wafalme 22. Mungu alikuwa ameamuru (kwa hiyo lazima itokee) kwamba ulikuwa ni wakati wa mwovu Ahabu kufa. Lakini Mungu aliruhusu viumbe wa kiroho kwenye baraza lake kuamua namna ya kulikamilisha hilo (1 Wafalme 22:19–23).

Kuchaguliwa tangu zamani na uhuru vinafanya kazi bega kwa bega katika utawala wa ufalme wa Mungu. Makusudi yake hayawezi kamwe kupinduliwa au kuzuiliwa. Ana uwezo wa kuchukua dhambi na uasi na bado akakamilisha—kupitia wawakilishi wengine huru—kile anachokitaka. Kama C. S. Lewis alivyowahi kusema kuhusu Mungu (kwenye kitabu *Perelandra*), "Chochote ufanyacho, atakifanya kuwa kizuri. Lakini sio uzuri aliokuwa ameuandaa kama ungelimtii."

Kwa matokeo yapi, hapa na sasa, Je, sisi ni famila ya baraza la Mungu? Kushirikiana na Mungu katika kuwakomboa watu kutoka gizani. Kuwaonyesha watu jinsi ya kuishi kwa haki na rehema—kumuiga Mungu kwa wote wanaohitaji mfano. Kutetea na kueneza ukweli kuhusu Mungu wa kweli katika ulimwengu adui chini ya himaya ya miungu werevu wenye wivu. Wafurahie maisha kama Mungu alivyokusudia yawe.

Wito wote huu ni mafunzo ya ufalme ujao. Kama Paulo alivyowauliza Wakorintho, ambao walikuwa na uelewa mkubwa wa Mungu wakati wakigombana kuhusu mambo madogo ya dunia hii, "Hamjui ya kuwa tutawahukumu malaika?" (1Kor. 6:3). Alikuwa ana maanisha. Paulo alikuwa anakifikia kitu mahususi kwenye kauli hiyo.

## Kuwekwa Juu ya Mataifa

Muonekano wa mwisho wa ufalme unakuja. Utakapokuwa umekuja, nguvu za giza zitashindwa. Miungu ya kipepo itapoteza utawala wao juu ya mataifa milele—*nafasi yao ikishikwa na familia ya wanadamu iliyotukuzwa na baraza la Mungu*. Tazama alichosema Yesu kwenye kitabu cha ufunuo:

Ila mlicho nacho kishikeni sana, hata nitakapokuja. Na yeye ashindaye, na kuyatunza matendo yangu hata mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa, naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, kama vyombo vya mfinyanzi vipondwavyo, kama mimi nami nilivyopokea kwa Baba yangu. Nami nitampa ile nyota ya asubuhi. (Ufunuo 2:25–28)

Wakati Yesu atakaporudi kuchukua kiti chake cha enzi kwenye dunia mpya—Edeni mpya ya ulimwengu wote—atashiriki pamoja na ndugu zake. Falme na nguvu zitatupwa kutoka kwenye viti vyao vya enzi, na sisi tutachukua nafasi zao. Himaya zao hazitatolewa kwa malaika waaminifu kwa Mungu—*tutakuwa juu ya malaika* katika ufalme wa Mungu wa mwisho wa Edeni. Yesu atawaweka kaka na dada zake wa kibinadamu watawale.

Je, umefumbwa na kauli ya mwisho katika Ufunuo 2:28? "Nami nitampa ile nyota ya asubuhi"? Inaonekana ya ajabu, bali inazungumzia ushirika wa utawala wetu na Yesu juu ya mataifa baada ya nguvu za uovu kuondoshwa. "Nyota ya asubuhi" inatumika kuonyesha viumbe vya kiungu (Ayubu 38:7). Pia ni neno la kimasihi. Kwa kuwa masihi ni Mungu, "lugha ya nyota" ni kitu kilichotumika kuelezea utawala wake ujao. Hesabu 24:17 inasema "Nyota itatokea katika Yakobo. Na fimbo ya enzi itainuka katika Israeli" (LEB). Katika kitabu cha Ufunuo, Yesu anajielezea mwenyewe hivi: "Mimi ndimi niliye Shina na Mzao wa Daudi; ile nyota yenye kung'aa asubuhi" (Uf. 22:16LEB).

Maneno ya Ufunuo 2:25–28 yana nguvu. Sio kwamba tu Yesu *anasema* yeye ni nyota ya asubuhi ya kimasihi, bali *anatupa* nyota ya asubuhi—anashiriki utawala wake wa kimasihi pamoja nasi. Ufunuo 3:20–21 inaenda hatua moja mbele hivyo waaminio msipoteze hoja hapa:

Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula

pamoja naye, na yeye pamoja nami. Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nillivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi. (Uf. 3:20–21LEB)

Kwa mwisho upi ambao tumefanywa washirika wa tabia ya Uungu? Kwa nini Yesu anatutambulisha sisi katika baraza kama kaka na dada zake? *Ili kwamba Mungu aweze kutupa utawala juu ya dunia alivyokusudia toka awali.* Mbingu zitarejea duniani katika Edeni mpya ya ulimwengu wote.

## Edeni ya Milele

Kutoka sura za kwanza za mwanzo, Edeni ilikuwa kituo cha mpango wa Mungu kwa mwanadamu, wengine ambao ni sura yake, na ufalme wake. Kwa hiyo sio kama ni mshangao au bahati kwamba sura ya mwisho ya kitabu cha ufunuo inaturejesha Edeni:

Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwana Kondoo, katikati ya njia kuu yake. Na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda, aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi; na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa. Wala hapatakuwa na laana yoyote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwamo ndani yake. Na watumwa wake watamtumikia; nao watamwona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao. Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele. (Uf. 22:1–5)

Je, umeona kwamba Mti wa Uzima huwaponya mataifa? Mataifa, ambayo yalitawaliwa na falme na nguvu, yatatawaliwa

na wana wapya wa Mungu, wakike na wakiume— *wewe na mimi*.

Hii haikuwa mara ya kwanza Mti wa Uzima kujionyesha katika Ufunuo. Akizungumza na wale waaminio kuhusu mwisho, Yesu alisema katika Ufunuo 2:7, 11, "Nitawapa kula matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya Mungu ... Hawatapatikana na madhara ya mauti ya pili." Kumbukumbu ya Mti wa Uzima ni wazi kuwa ni wa Edeni. Mauti ya kwanza ina maanisha mauti ya kimwili, iliyoletwa na dhambi ya Adamu na kufukuzwa kutoka Edeni. Kwa kuwa wanadamu wote, waaminio na wasioamini sawa sawa, watafufuliwa kabla ya hukumu, mauti ya pili ni hukumu ya mwisho (Uf. 21:8). Wale wanaoendelea kuishi na Mungu katika Edeni mpya hawapatwi na mauti ya pili.

## Kwa nini hili ni Muhimu

Wakristo wengi wana mtazamo duni wa maisha yajayo. Maandiko hayatuambii kila kitu kuhusu vile itakavyokuwa, bali baadhi ya mambo ni bayana. Hatuendi kupiga vinubi au kuimba bila ukomo huku tukielea mawinguni. Hatutakuwa tukikaa tu kwenye viti vya enzi tukizungumza na wapendwa wetu waliotutangulia au waaminio wanaofahamika vyema kutoka zamani.

Badala yake, tutakuwa tukiishi maisha Edeni iliyotoa—tutakuwa na shughuli ya kufurahia na kujali kile Mungu alichofanya, hapa kwa hapa na viumbe wa Kimungu waliobakia waaminifu kwake. Mbinguni na duniani hazitakuwa tena sehemu zilizotenganishwa.

Kwa kujua kuwa hatma yetu inapaswa kujenga kuwaza kwetu hapa na sasa. Kama Paulo alivyosema, "Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao." (1 Kor. 2:9GNT). Kujua matokeo haya ya kushangaza, ya utukufu inasaidia kuweka mazingira ya

hali yetu katika mtazamo. Baada ya Paulo kuandika maneno tuliyoyasoma tu hivi punde, alisema haya katika waraka wake wa pili kwa Wakorintho:

Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote; atufarijiye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo tunazofarijiwa na Mungu. Kwa kuwa kama vile mateso ya Kristo yanavyozidi kwetu, vivyo hivyo faraja yetu inazidi kwa jina la Kristo. Lakini ikiwa sisi tu katika dhiki, ni kwa ajili ya faraja yenu na wokovu wenu; au ikiwa twafarijiwa, ni kwa ajili ya faraja yenu; ambayo hutenda kazi yake kwa kustahimili mateso yale yale tuteswayo sisi. Na tumaini letu kwa ajili yenu ni imara, tukijua ya kuwa kama vile mlivyo washiriki wa yale mateso, vivyo hivyo mmekuwa washiriki wa zile faraja. Maana ndugu, hatupendi, msijue habari ya dhiki ile iliyotupata katika Asia, ya kwamba tulilemewa mno kuliko nguvu zetu, hata tukakata tamaa ya kuishi. Naam, sisi wenyewe tulikuwa na hukumu ya mauti katika nafsi zetu; ili tusijitumainie nafsi zetu, bali tumtumainie Mungu, awafufuaye wafu.(2 Kor. 1:3–9, msisitizo umeongezwa)

Mungu anaweza kutuhifadhi katika maisha. Bali hata katika mauti, tutafufuliwa tukae pamoja na Yesu kwenye kiti chake cha enzi (Uf. 3:21).

Ni ama tunaishi na mtazamo wa kule tunakokutarajia au hatuna. Na ufahamu wa hatma yetu unapaswa kubadili tabia zetu. Kama ungejua siku moja utashirikiana nyumba au kufanya kazi kwenye ofisi moja kama yule unayemkosoa, kumbugudhi, na wakati mwingine kuonyesha jeuri, ungewekeza jitihada kidogo katika kuwa mpatanishi, mfariji, na pengine hata rafiki kwa huyo mtu. Hii ikoje kwamba tunamchukulia muumini mwenzetu vibaya hivyo, kisha? Hii ikoje kwamba hatutumii nguvu kubwa kumsogeza asiyeamini

kwa Yesu kama tunavyofanya tunapokabiliana naye kama adui? Ama tuna umilele katika mtazamo au hatuna.

Ni mamlaka kiasi gani Yesu anatakiwa kushiriki na wewe kukufanya uwe na furaha? Swali linaweza kuonekana la ajabu, kwa kuwa kipawa *chochote* kama hicho kutoka kwa Yesu kingekuwa maridhawa. Kwa nini, kisha, Je, tunagombana na waaminio kwa ajili ya hadhi? Kwa nini tunagombana sisi kwa sisi kwa faida, tahadhari, na manufaa binafsi? Je, sisi sio bora kuliko Wakorintho, ambao Paulo alipaswa kuwakumbusha juu ya hatma yao? Ama tunafurahia kutawala na kumiliki na yeye, au hatufurahii.

Mkristo, ni wakati wa kuishi kama unajua wewe ni nani na unajua mipango Mungu aliyonayo kwa ajili yako.

# Hitimisho

Tumefikia mwisho wa safari yetu. Lakini huenda ni vyema kusema ndio tu tumeanza. Tumetafakari baadhi ya maswali ya msingi: *Je, miungu mingine ipo? Kama wapo, je, hiyo inaleta tofauti kubwa katika namna tunavyoielewa Biblia? Ina maanisha nini kwa imani yetu kama tukiamini kuwa ulimwengu usiooneka ulioelezewa katika Biblia ni halisi kweli—sio tu sehemu zinazofahamika na kukubalika, bali sehemu zisizokuwa za kawaida na zinazopuuzwa-mara nyingi?* Mara nilipoanza kushika mwelekeo wa maandiko wa Nguvu Isiyo ya kawaida, niligundua kuwa natakiwa kufikiri tofauti kuhusu vitu tofauti. Bali naweza kuyajumuisha yote katika maneno mawili: *utambulisho na kusudi.* Naamini umepata changamoto ya maeneo yote hayo kadri ulivyosoma kitabu hiki.

## Utambulisho wetu—Tuna makao katika Familia ya Mungu

Kilichojadiliwa na kitabu hiki kina umuhimu mkubwa wa namna tunavyoelewa ina maanisha nini kuwa Mkristo—kuwa "ndani ya Kristo," kama ambavyo Agano Jipya linavyoweka mara nyingi. Mara tutakapo tambua kuwa miungu wa Agano la Kale ni halisi, ndipo maana ya amri ya Mungu ya kutokukuwa na miungu mingine mbele za Bwana (Yahweh), Mungu wa Israeli, itakuja katika mtazamo. Amri hii haihusu kutokutoa kipaumbele kwa fedha au boti au magari. Ni kuhusu wivu wa upendo wa Mungu kwa watu wake. Kwa maneno mengine, *amri hii kwa hakika ina maanisha kile inachosema.* Gadhabu ya kuwa mwaminifu (utii) kwa mungu mwingine yeyote tofauti na Mungu wa miungu yote ni vigumu kuikosa.

Ubaya wa kuishi na athari za namna Mungu alivyowahukumu miungu na watu wao ("mataifa") uko wazi kabisa pia. Tulikuwa *tumetengwa,* watumwa wa rushwa na unyonyaji wa miungu mingine. Tulikuwa, kama Paulo alivyosema, mlikuwa mmefarakana na Mungu na wageni wasio

wa maagano ya ahadi ile (Ef. 2:12). Tulikuwa tumepotea, tukitumikishwa katika matendo ya giza, maadui wa Mungu katika huduma ya miungu wenye mamlaka wasioonekana (Ef. 4:18; Kol. 1:21).

Baada ya kuwa na ufahamu wa hali hiyo inafanya dhana ya mafundisho kama *kufanywa wana* na *urithi* kuwa na maana zaidi. Unayapa muktadha. Mungu hakukusudia kuuacha mpango wake wa kuishi duniani na familia yake, kuufurahia ulimwengu ulioumbwa ambao ulitoka katika mikono yake yeye mwenyewe. Ndiyo, pale Babeli aligeuza uso wake mbali na wanadamu, bali muda mfupi baadae, alimwita Abramu kuanza familia mpya—na kuwa kiungo ambacho kupitia yeye wale waliofarakana nae wangepata njia ya kurejea kwake (Matendo 10:26–27).

Kuushikilia uhalisia wa kiungu wa ulimwengu  wa roho wa Biblia ni muhimu kwa kuielewa Biblia. Inaelezea kwa nini, kadri Agano la Kale linavyosonga mbele, dhambi ya kuabudu sanamu haitakuwa tu kama dhambi nyingine yoyote. Itakuwa dhambi. Israeli iliumbwa kuwa uaminifu kwa Mungu; wakati alipowageukia miungu wengine badala yake,alipelekwa uhamishoni (utumwani), kutupiliwa mbali kama mataifa mengine. Hii ndiyo sababu kuu kwa nini wokovu katika Biblia wakati wote unaelezewa kwa *imani*. Mungu hatimaye haangalii tabia bora. Anaangalia imani—kwa *kuamini uaminifu*. Wakati tunapochagua kuielekeza mioyo kwa Mungu wa miungu, atatuokoa. Wakati tunapochagua mwingine, tunapanda kile ambacho siku moja tutavuna.

Kwetu sisi leo, kuamini uaminifu ina maanisha kukubali kile alichofanya Yesu msalabani, kwa sababu alikuwa Mungu katika mwili. Mienendo yetu na tabia (kazi zetu) haihusu kuwa waaminifu vya kutosha ili Mungu atukubali. Tunafuata maagizo yake kwa sababu tumekwisha kumchagua. Na maagizo yake yatatuletea furaha na raha kwa sababu yatatuelekeza mbali na uharibifu wa nafsi na mwingine.

Yanatoa mtazamo wa maisha katika amani na Mungu na wengine wa familia yake—familia yetu—inayoonekana na isiyoonekana, katika ufalme wake, Edeni mpya.

Kusudi Letu—Sote tuna wajibu katika Mpango wa Mungu wa Kuirejesha Edeni

Kuwa mwanafamilia katika familia ya Mungu kuna sharti moja tu: imani isiyotetereka kwa Mungu wa miungu, aliyekuja kwetu kama mtu kupitia Yesu Kristo. Huo uanafamilia sio tu unahifadhi upendeleo wa ajabu, bali pia unatupatia kusudi lililo wazi katika maisha.

Wanafamilia wa familia ya Mungu wana kazi: kuwa mawakala wa Mungu katika kurejesha utawala wake mzuri duniani na kukuza uana familia wa familia yake. Sisi ni njia ya Mungu ya kueneza urejesho mkuu ulioanza katika Matendo 2, kuzaliwa kwa kanisa, mwili wa Kristo, hadi wakati Bwana atakaporudi. Kadri uovu ulivyosambaa kama ugonjwa wa kuambukiza kwa wanadamu baada ya kushindwa kwa Edeni ya kwanza, hivyo injili inaenea kama kiuasumu kwa mwathirika yuleyule. Sisi ni *wabeba* ukweli kuhusu Mungu wa miungu, upendo wake kwa mataifa *yote*, na shauku yake isiyobadilika ya kuishi na familia yake katika makao ya duniani aliyoyataka tangu kuumbwa kwake. Edeni *itaishi* tena.

Ni ukweli wa kisayansi kwamba mabara ya dunia yanasogea mbali zaidi kila mwaka. Bali maendeleo ya “mjongeo wa mabara” hauwezi kugundulika kwa fahamu au akili za mwanadamu. Tunajua tu kuwa unatokea kwa sababu ya uchunguzi tunaoweza kufanya baada ya ukweli. Hivyo ni pamoja na uthabiti, kuenea kwa kasi kwa ufalme wa Mungu. Hatuwezi kuona kwa macho matupu ni kwa vipi kila siku unadhoofisha falme za miungu, nguvu za giza, au namna injili inavyokomboa, mmoja kwa mmoja, wale walioshikiliwa chini ya falme. Bali ni *Uhakika usioweza kueleweka* (*upitao ufahamu wa mwanadamu*)

Mwongozo wa kujiona sisi wenyewe katika picha hii ni kwa uthabiti kuelewa kwamba Mungu bado anaufanyia kazi mpango wake hata wakati ambao hatuwezi kuona. Hatuwezi kwa kweli kudai kuwa tunaamini katika yasiyooneka, ulimwengu wa kiroho wakati hatuamini maandalizi ya baadae ya Mungu ni thabiti katika maisha yetu na maswala ya historia ya mwanadamu. Mungu anatutaka tuishi kwa kusudi/ lengo—tukiamini kuwa mkono wake usioonekana na wawakilishi wake wasioonekana walio waaminifu kwake na kwetu (Ebr. 1:14) wanahusika katika hali zetu, pamoja, lengo la Mungu la Edeni ya ulimwengu wote lisonge mbele bila kuzuilika.

Kila mmoja wetu ni muhimu kwa njia ya mtu fulani kwenye ufalme na ulinzi wa ufalme huo. Kila siku inatuwezesha sisi kuwasiliana na watu walio chini ya ufalme wa giza na fursa ya kutiana moyo katika kazi ngumu ya kutimiza kusudi letu katika ulimwengu usio mkamilifu. *Kila kitu tunachofanya na kusema ni muhimu,* ingawa tunaweza tusijue kamwe kwa nini au kwa vipi. Bali kazi yetu sio kuangalia—ni kufanya. Kutembea kwa imani sio ubatili— ni kusudi.

## Maombi ya Msamaha (Toba): Zawadi ya thamani

Maombi ya msamaha (toba) ni kitu ambacho sote tunakitafuta katika wakati fulani maishani. Msamaha (toba) ni zawadi ya thamani ambayo haipatikani kwa urahisi, wala kutolewa kwa urahisi. Msamaha (Toba) ni muhimu kwa maisha; inatuweka huru kutoka kwenye makosa yaliyopita na kutupa tumaini la wakati ujao. Ni kwa ajili ya msamaha Yesu alikuja duniani ili afe kwa ajili ya mwanadamu.

**Maombi ya Msamaha: Yamewezeshwa na Yesu Kristo** Maombi ya msamaha ni maombi yanayoombwa kwa Mungu. Ingawa tunaweza kuumizana (kukwazana) mtu na mtu moja kwa moja, makosa yetu yote hatimaye yanamkwaza Mungu. Unaweza kushangaa hili linawezekanaje. Ni kwa namna gani mapungufu yetu yanaweza kumkwaza muweza wa yote Muumba wa ulimwengu? Je, Mungu anajali? Katika mwanzo 6; Tunaona kwamba Mungu mwenyewe kwa hakika alihuzunika juu ya mabaya ambayo watu walifanyiana wao kwa wao: *"Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya siku zote. Bwana akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo"* (Mwanzo 6:5-6)

Ajuaye yote, Mungu huhuzunika hata kwa mawazo tu ya uovu. Hivyo, msamaha wa mwisho lazima pia utoke kwa Mungu. Hata hivyo, kwa sababu ya haki yake, msamaha hauwezi kutolewa bure. Kila kosa lazima liadhibiwe ili Mungu awe Mwamuzi wa Haki. Yesu Kristo alikufa msalabani pale kalvari badala yetu ili kwamba dhambi zetu zisamehewe. Mateso yake yalilipia makosa yetu. *"Kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi"* (Mathayo 26:28).

Katika Upendo Wake, Mungu alijua kwamba ufahamu wetu unahitaji kuwekwa huru kutoka kwenye hatia na laumu. Alijua kuwa msamaha wa dhambi ndilo lilikuwa hitaji letu kuu. Katika tendo la mwisho la upendo, Mungu sio tu kuwa aliumizwa na makosa yetu, bali pia alilipia gharama zao ili kwamba msamaha uweze kutolewa kwetu tutakapofanya dhambi. Tunachohitajika tu kufanya ni kuikubali zawadi yake ya bure ya msamaha.

**Maombi ya Msamaha: Muombe kwa ajili ya Msamaha** Huenda umeangukia kwenye ukurasa huu wa tovuti ukitafuta maombi ya msamaha yaifariji nafsi iliyoumizwa. Au labda unapambana na kujaribu kumsamehe mwingine kwa kukuumiza sana. Kwa wote wanaomkubali Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao, msamaha umetolewa bure. Kama tunayatambua makosa yetu na kuomba msamaha, Mungu atatusamehe- hakuna maswali yanayoulizwa: *"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote"* (1 Yohana 1:9).

Kama tukimkataa Yesu, maana yake, tumeikataa zawadi ya Mungu ya msamaha. Kwa hakika tunakuwa tunasema, hatutaki kupatanishwa na Mungu (1 Yohana 1:10). Ingawa ni chaguo letu huru kutokukubali msamaha kutoka kwa Mungu, hatimaye tutawajibika kwa dhambi zote tulizozifanya katika mwisho wa maisha haya. Ni shauku ya kina ya Mungu kupatanishwa na wewe. *"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele"* (Yohana 3:16). Kama unatamani kweli kusamehewa, fikiria kile alichosema Yesu na kumkubali kwa dhati kama Bwana na Mwokozi wako. Utasamehewa na Mungu ataanza kazi ya kuyabadilisha maisha yako.

**Maombi ya Msamaha: Pokea Maisha Mapya**, Maombi ya msamaha (toba) yanatupa tumaini jipya na mwanzo mpya. Dhambi zetu zote zinafutiliwa mbali na Mungu. *"Kwa sababu nitawasamehe maovu yao, Na dhambi zao sitazikumbuka tena"* (Ebrania 8:12).

Kama unaelewa kuwa wewe ni mwenye dhambi, na unaamini kuwa Yesu Kristo alikuja kama Mkombozi pekee wa dhambi, basi unafahamu maombi ya msamaha (toba). Swali ni – Je, uko tayari kuyatendea kazi maombi haya, kwa kupokea zawadi ya Mungu ya Mwanawe, Yesu Kristo? Kama ndivyo, mwamini Yesu, tubu dhambi zako, na yakabidhi maisha yako yaliyosalia kwake kama Bwana:

> ***"Baba, najua kuwa nimevunja sheria zako na dhambi zangu zimenitenga na wewe. Nazijutia kweli, na sasa nataka kugeuka mbali na maisha yangu ya zamani ya dhambi nikugeukie wewe. Naomba unisamehe, na unisaidie nisitende dhambi tena. Naamini kuwa mwanao, Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zangu, alifufuka kutoka kwa wafu, yuko hai, na anasikia maombi yangu. Namkaribisha Yesu awe Bwana wa maisha yangu, atawale na kumiliki moyoni mwangu tangu leo na kuendelea. Naomba umtume Roho Mtakatifu anisaidie kukutii Wewe, na kufanya mapenzi yako kwa kipindi chote kilichosalia cha maisha yangu. Katika jina la Yesu ninaomba, Ameni."***

"Tubuni, mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu" (Matendo 2:38).

Kama umeamua kumpokea Yesu leo, karibu kwenye familia ya Mungu. Sasa, kama njia ya kuwa karibu Naye, Biblia inatuambia tufuatilie ahadi yetu.

- Ubatizwe kama ilivyoagizwa na Kristo.
- Mwambie mtu mwingine yeyote kuhusu imani yako mpya katika Kristo.

- Tumia muda (kaa) na Mungu kila siku. Sio lazima kiwe kipindi cha muda mrefu. Jenga tu tabia ya kila siku ya kumwomba na kusoma Neno Lake. Mwombe Mungu aizidishe Imani yako na uelewa wako wa Biblia.
    - Kutafuta ushirika na wafuasi wengine wa Yesu. Kuendeleza kundi la marafiki waaminio kujibu maswali yako na kukusaidia.
    - Tafuta kusanyiko la karibu ambapo unaweza kumwabudu Mungu.

Je, umekuwa mfuasi wa Yesu leo? Tafadhali bonyeza

NDIYO au HAPANA

Je, tayari wewe ni mfuasi wa Yesu? Tafadhali bonyeza hapa

UNAFIKIRIA NINI? - Sote tumetenda dhambi na kustahili hukumu ya Mungu. Mungu, Baba, alimtuma Mwanawe wa pekee akawe fidia ya hukumu hiyo kwa wale wamwaminio. Yesu, muumbaji na Mwana wa Mungu wa milele, ambaye aliishi maisha yasiyo na dhambi, anatupenda sana kiasi ambacho alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, akiichukua adhabu tuliyoistahili, alizikwa, na kufufuka kutoka kwa wafu kulingana na Biblia. Kama utamwamini kweli na kulitumaini hilo moyoni mwako, ukimpokea Yesu pekee awe Mwokozi wako, na kukiri, "Yesu ni Bwana, "utaokolewa kutoka kwenye hukumu na kukaa milele na Mungu huko mbinguni.

Mwitikio wako ni upi?
Ndiyo, leo naamua kumfuata Yesu
Ndiyo, mimi tayari ni mfuasi wa Yesu
Bado nina maswali

## Ombi kutoka kwa Mwandishi

*Nguvu Isiyo ya Kawaida* ni ufupisho wa kitabu changu cha kitaaluma, kilichosheheni mambo mengi, *Ulimwengu Usioonekana: Kurejesha Mtazamo wa Dunia wa Mungu wa Biblia* (Lexham Press, 2015). *Ulimwengu usioonekana* kinapatikana kwa Kiingereza kwenye Amazon. com.

Natumaini umekuta *Nguvu Isiyo ya Kawaida* kiroho kinainua. Ninaweza kukitoa kitabu hiki kwa sababu michango ya ukarimu ya watu wanaojali kuhusu maudhui. Tafadhali fikiria kutoa kwa Miqlat kupitia ama miqlat.org au nakedbible.org ili kufanya maudhui zaidi yapatikane.

Kwa mafundisho zaidi ya kibiblia, tafadhali tembelea ukurasa wangu, drmsh.com, na usikilize vipande vyangu vya sauti vya Biblia wazi katika nakedbiblepodcast.com. jina " Biblia Wazi" linaakisi shauku yangu ya kufundisha vifungu vya Biblia pekee bila usiochujwa na tamaduni za kisasa, madhehebu, na chujio nyingine za kidini.

Kadri utakavyogundua kwenye ukurasa wangu, Pia huwa ninaandika sayansi ya kubuniwa kama njia ya kuwatambullisha watu kwenye theolojia ya Biblia. Riwaya zangu (kwa sasa, *The Façade (Sura)* na its sequel (Mwisho Mwema), *The Portent*) zinapatikana tu kwa Kiingereza kupitia Amazon.com.